Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

EQUIPPING CHURCH LEADERS
• EAST AFRICA •

WAGALATIA

na

Jonathan M. Menn

B.A., University of Wisconsin-Madison, 1974
J.D., Cornell Law School, 1977
M.Div., Trinity Evangelical Divinity School, 2007

Equipping Church Leaders-East Africa
3701 N. Gillett St., Appleton, WI 54914
(920) 731-5523
jonathanmenn@yahoo.com
www.eclea.net

Kimetafsiriwa na Michael Nyangusi mn6094@gmail.com

2020

Kitabu hiki cha Wagalatia kiliandikwa na mtume Paulo na huenda kilikuwa ndicho kitabu chake cha kwanza alichoandika. Kitabu hiki kinafanya mambo matatu muhimu: (1) Kinathibitisha utume wa Paulo; (2) Ni utetezi wa "injili" wanye ushawishi mkubwa—lile fundisho kuu la Kikristo ya kwamba watu wanaokolewa kwa neema ya Mungu tu kwa njia ya imani katika Yesu Kristo—na hii huifanya familia yote ya Kikristo (Wayahudi na Mataifa pia) kuwa moja; (3) Kisha kinajadili ile maana hasa ya huu msimamo wa wokovu kwa ile jamii mpya: watu wanapaswa kuishi maisha mapya kwa imani inayotiririka kutoka katika kazi za Roho Mtakatifu aliye ndani yao. Kitabu hiki, labda zaidi ya kinginecho, huelezea upekee wa Ukristo: kila dini nyingine yoyote dunia kimsingi ni orodha ya sheria na amri za kufuata ambazo huwatumikisha watu. Ukristo ni tofauti: ndani ya Kristo tumewekwa huru kutoka utumwani mwa sheria na mwili; hii haimaanishi kwamba Wakristo hawana sheria. Badala yake, Wakristo wana "sheria ya Kristo" ndani yao, na kupitia uongozi wa ndani wa Roho Mtakatifu aliye ndani yao wanabadilishwa waishi kama Kristo.

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

YALIYOMO

I. Utangulizi…….....2
A. *Mwandishi, tarehe, na walioandikiwa*……..2
B. *Mazingira ya tukiona kusudi*…….....2
C. *Muhtasari*……...3

II. Maoni kuhusu Wagalatia……....4
A. Gal 1:1-5—Salamu ……..4
B. Gal 1:6-9—Sababu ya kuandika……7
C. Gal 1:10-2:21—Huduma na ujumbe wa Paulo…….....8
D. Gal 3:1-4:31—Utofautishaji wa imani/sheria……..19
E. Gal 5:1-6:10—Uhuru ndani ya Kristo…….....36
F. Gal 6:11-18—Muhtasari na hitimisho……..51

BIBLIOGRAFIA……53

MWANDISHI…….57

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

I. Utangulizi

A. *Mwandishi, tarehe, na walioandikiwa*

Kitabu cha Wagalatia kiliandikwa na *"mtume Paulo"* (**Gal 1:1**). Kuna mjadala wa wanazuoni kuhusiana lini waraka huu uliandikwa. Mtazamo wa walio wengi (na labda ulio na usahihi zaidi) ni kwamba Pengine Wagalatia kiliandikwa mnamo mwaka 48 BK kabla tu ya Baraza la Yerusalemu (**Matendo 15**); mtazamo mwingine huamini waraka huu uliandikwa baada tu ya Baraza la Yerusalem, labda katika kipindi cha tatu cha safari ya kimisheni ya Paulo mnamo miaka ya 50 BK (ona Carson and Moo 2005: 461-64; Marshall, Travis, and Paul 2002: 56-59; McClelland 1989: 998-1001). Ikiwa tarehe ya awali ilikuwa sahihi, inaonyesha wazi kuwa Wagalatia ni waraka wa kwanza wa Paulo na pengine ni waraka wa kwanza kuandikwa katika AJ (Yakobo anaelekea kuwa ni mhusika mwingine).

Galatia lilikuwa mojawapo ya majimbo ya Dola ya Kirumi. Ilikuwa ipo kati ya jimbo la Asia na Kapadokia ndani ya eneo la kati la Uturuki ya sasa. Katika safari ya kwanza ya kimisheni ya Paulo (**Matendo 13-14**) alitembelea miji ya Likaonia, Listra na Derbe katika Galatia ya kusini. Alirudi Galatia wakati akiwa katika safari yake ya kimisheni ya pili (**Matendo 16:1-6**) nay a tatu (**Matendo 18:23**). "Ni kitu kilicho dhahiri kusadiki kwamba makusanyiko yaliyokuwa katika miji hii ya kusini mwa jimbo la Galatia ndiyo yaliyoandikiwa waraka huu" (Marshall, Travis, and Paul 2002: 54).

B. *Mazingira ya tukio na kusudi*

Matendo 13-14 inatuambia ya kwamba Paulo na Barnaba walikuwa wameshahubiri kusini mwa jimbo la Galatia. Baada ya kuondoka, baadhi ya Wakristo wa Kiyahudi walikuja katika eneo lile. Kwa kawaida watu hawa huitwa "Wayahudishaji." Wale Wayahudishaji "waliidhofisha injili ya Paulo kwa kudai kwamba mamlaka ya Paulo ilikuwa ni ya kiwango cha chini ikilinganishwa na ile ya mitume wengine kama Petro na Yakobo, ambao walikuwa wanahusiana kwa karibu zaidi na Kanisa la Yerusalemu na Dini ya Kiyahudi ([Gal] 1:1; 6:17). Lakini udanganyifu halisi waliokuwa wakiueneza katika makanisa yale yote ulikuwa kwamba waongofu wa Mataifa lazima waishi kama Wayahudi na watahiriwe na watekelezi baadhi ya mambo ya sheria ya kidini, ili waokoke kutoka katika ghadhabu pamoja na kumuamini Yesu Kristo kama Masihi. . . . Hivyo, mtu ni lazima aongeze kitu katika imani ndani ya Kristo kama Masihi, vile tunavyoviita 'nishani' au 'nembo' ya taifa la Israeli, ambazo ni kukubali kutahiriwa, kufuata sheria fulani za kula, katika karamu za sherehe za Kiyahudi, na kuelewa kuendelea kuitii sheria ya Musa kama kitu kilicho lazima ili kuendelea kuwa na nafasi katika jamii ya agano." (Riddlebarger 2017: n.p.)

Hatari ya hili fundisho la uongo iko katika ile hali ya ugumu katika kulitambua. David Platt na Tony Merida anaonyesha kwamba "sehemu kubwa ya mafundisho ya Wayahudishaji yalikuwa yako sawa na mstari, tukisema kibiblia. Walimkubali Yesu kama Masihi, na hata walikubali kifo chake msalabani. Walidai kuwa waliiamini kweli yote ambayo iliaminiwa na Wakristo wengine, na kwa hakika hawakuwaambia watu kwamba waliikataa injili. Badala yake, walikuwa wakiiongezea ubora, wakiongezea masharti na viwango kutoka katika agano la kale kwenda katika agano jipya. Lakini uhalisia ni kwamba mara tu utakapoongeza chochote kwenye neema, unaipoteza neema moja kwa moja. Hakuna mahali pa katikati." (Platt and Merida 2014: 10) Paulo aligundua kwamba fundisho hili potofu limekwenda katika kiini cha injili na ule usawa katika Kristo wa kila kabila, lugha, na taifa. Waraka kwa Wagalatia ndilo jibu lake.

Wagalatia ni chenye "fokasi" zaidi ya nyaraka nyingine nyingi za Paulo. Pia ni cha mjadala zaidi (m.y., hoja ya kuunga mkono au kupinga maoni au fundisho). Kimsingi kitabu hiki hufanya mambo matatu: (1) Kinathibitisha utume wa Paulo; (2) Ni utetezi wa "injili" wanye ushawishi mkubwa—lile fundisho kuu la Kikristo ya kwamba watu wanaokolewa kwa neema ya Mungu tu kwa njia ya imani katika Yesu Kristo—na hii huifanya familia yote ya Kikristo (Wayahudi na Mataifa pia) kuwa moja; (3) Kisha kinajadili ile maana hasa ya huu msimamo wa wokovu kwa ile jamii mpya: watu wanapaswa kuishi maisha mapya kwa imani inayotiririka kutoka katika kazi za Roho Mtakatifu aliye ndani yao.

Kitabu hiki, labda zaidi ya kinginecho, huelezea upekee wa Ukristo: kila dini nyingine yoyote dunia kimsingi ni orodha ya sheria na amri za kufuata ambazo huwatumikisha watu. Ukristo ni tofauti: ndani ya Kristo tumewekwa huru kutoka utumwani mwa sheria na mwili; hii haimaanishi kwamba Wakristo hawana sheria. Badala yake, Wakristo wana "sheria ya Kristo" ndani yao, na kupitia uongozi wa ndani wa Roho Mtakatifu aliye ndani yao wanabadilishwa waishi kama Kristo.

Fokasi ya kitabu hiki inaonekana katika maneno makuu na mawazo ambayo Paulo anayatumia kwa kurudiarudia na mambo mbalimbali yatayotofautiana:

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

Sheria—mara 31 Mwili—mara 16 Kutahiriwa/waliotahiriwa—mara 13	Imani/uaminifu—mara 22 Roho/warohoni—mara 19 Injili—mara 11 Ahadi—mara 11 Huru/uhuru—mara 10

C. ***Muhtasari***

Tukiwa na haya matatu ambayo Wagalatia hufanya—(1) kinathibitisha utume wa Paulo; (2) utetezi wa "injili"; na (3) kujadili namna watu wanavyotakaswa kwa kutii kwao kutokanako na imani yao na kutiririka kutoka kwa utendaji wa Roho Mtakatifu aliye ndani yao—muhtasari wa kitabu ni kama ifuatavyo:

1:1-5—Salamu

1:6-9—Sababu ya kuandika: Ikiwa mtu awaye yote anahubiri "injili" isipokuwa niliyohubiri, na alaaniwe milele.

1:10-2:21—Huduma ya Paulo na ujumbe: Wayahudi na Mataifa sawasawa wanahesabiwa haki kwa imani katika Kristo peke yake, si kwa sheria.

- **1:10-12—**Paulo alivyoipokea Injili.
- **1:13-14—**Maisha ya Paulo kabla ya kubadilika kiimani.
- **1:15-16a—**Kubadilika kiimani kwa Paulo.
- **1:16b-24—**Maisha ya Paulo mara tu baada ya kubadilika kiimani na mkutano wake wa kwanza na uongozi wa Yerusalemu.
- **2:1-10—**Mkutano wa pili wa Paulo na uongozi wa Yerusalemu.
- **2:11-21—**Kweli ya injili iko juu ya umuhimu wa watu binafsi na urithi wake mtu:
    - **2:11-14—**Paulo anauweka hadharani unafiki wake Petro kuhusiana na jinsi alivyowatandea waamini wa Mataifa.
    - **2:15-21—**Hata Wayahudi huhesabiwa haki kwa imani, si kwa sheria.

3:1-4:31—Utofautishaji imani/sheria: Hili ni la msingi na huturudisha nyuma tangu wakati wa Ibrahimu.

- **3:1-5—**Swali kuu: Je unakamilishwa kwa mwili (sheria), au kwa Roho (imani)?
- **3:6-9—**Ni wale tu walio wa imani (wawe Wayahudi au Mataifa) ndio watoto wa kweli wa Ibrahimu.
- **3:10-14—**Hakuna anayehesabiwa haki kwa sheria ispokuwa yuko chini ya laana.
- **3:15-24—**Makusudi ya sheria:
    - **3:15-18—**Sheria haiwezi kuweka agano na Ibrahimu kila mwaka.
    - **3:19-22—**Sheria huifunua hali yetu ya dhambi.
    - **3:23-24—**Sheria ilikuwa mwangalizi aliyetuongoza kwa Kristo.
- **3:25-4:7—**Ndani ya Kristo sisi si watumwa tena au watoto walio chini ya mwangalizi, lakini tumekombolewa, tumeasiliwa, wana na warithi wa Baba.
- **4:8-20—**Akiwasihi Wagalatia:
    - **4:8-11—**Ombi kwa mujibu wa hadhi yao katika Kristo.
    - **4:12-20—**Ombi kwa mujibu wa mahusiano binafsi.
- **4:21-31—**Muhtasari: Utofautishaji wa sheria/ahadi yote uko kwa muhtasari kwa njia ya mfano ndani ya Hajiri (Ishmaili) na Sara (Isaka); kwa kushangaza, Israeli ni Ishmaili na Wakristo ni Isaka!

5:1-6:10—Uhuru ndani ya Kristo: Mliitwa katika uhuru, hivyo enendeni kwa Roho.

- **5:1-26—**Mliitwa katika uhuru, hivyo msijiweke tena chini ya utumwa wa sheria au mwili lakini enendeni kwa Roho.
    - **5:1-6—**Msiwe chini ya sheria ya kutahiriwa, ambayo huonyesha kwamba umeiacha neema ya Roho kwa ajili ya utumwa wa sheria.
    - **5:7-12**—Msiwafuate wale ambao mafundisho yao hayatoki kwa Bwana.
    - **5:13-15—**Msiugeuze uhuru wenu kuwa fursa ya mwili; badala yake, mpendane ninyi kwa ninyi (ambalo huitimiza sheria).
    - **5:16-26—**Matendo ya mwili na tunda la Roho hupingana.
- **6:1-10—**Matumizi bayana ya *"imani itendayo kazi kwa upendo"* na *"kuendenda kwa Roho."*

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

- **6:1-5—**Mchukuliane mizigo.
- **6:6-10—**Unavuna kile upandacho, hivyo na tuwatendee watu wote mema kwa namna tunavyoweza.

Gal 6:11-18—Muhtasari na hitimisho: Wale wanaotaka kutahiriwa ni wanafiki na hawafanyi hayo kutoka katika nia njema kamwe; rehema na neema ya Mungu iwe juu ya wale ambao husikia kutukuka katika msalaba wa Kristo tu.

II. Maoni kuhusu Wagalatia

A. Gal 1:1-5—Salamu

- **1:1-2:** ***[1]Paulo, mtume, (si wa wanadamu, wala kutumwa na mwanadamu, bali na Yesu Kristo, na Mungu Baba aliyemfufua kutoka kwa wafu), [2] na ndugu wote walio pamoja nami, kwa makanisa ya Galatia;***

  Wakati Paulo akiandika, njia ya kawaida ya kuanza kuandika barua ilikuwa ni kwanza kujitambulisha mwenyewe (**mst. 1**), pili kuwataja wale anaowaandikia (**mst. 2**), tatu kuendeleza salami kwa wale anaowaandikia (**mst. 3-5**). Paulo analifanya hili katika nyaraka zake nyingine vilevile. Hata hivyo, kwa mazingira na muktadha wa waraka wa Wagalatia, **mst. 1-2** kwa hakika imeshiba maana. Utume wa Paulo ulipingwa na Wayahudishaji. Kwa hiyo, haanzi waraka huu kwa yeye kujiita "mtumwa" wa Kristo kama anavyofanya katika **Rum 1:1, Filp 1:1,** na **Tito 1:1,** au "mfungwa" wa Kristo kama anavyofanya katika **Flm 1:1**. Badala yake, anajiita "mtume," lakini tena anafanya zaidi ya hilo: anaweka mkazo kwamba utume wake *"hakutumwa na wanadamu wala si wa wanadamu, bali na Kristo na Mungu Baba, aliyemfufua kutoka kwa wafu."* Ni wazi kuwa anaitambua mamlaka yake mwenyewe kwa kusisitiza kwamba nafasi yake kama mtume haikuja kwake kupitia wanadamu lakini ilikuja moja kwa moja kutoka kwa Yesu Kristo na Mungu Baba.[1] Ataendelea kudai na kuuelezea utume wake katika sehemu kubwa inayoendelea ya **sura 1** na **2**. Zaidi ya hayo, katika **mst. 2** Paulo anaweka mkazo kwamba hayuko peke yake lakini anawataja "*ndugu wote walio pamoja nami."* Kwa kuwekea mkazo hili anawaambia walimu wa uongo na waaminio wa Galatia kwamba mafundisho yake ya (kweli) yanaungwa mkono na wengine wengi. Hivyo, hata katika mistari ya kwanza ya waraka huu Paulo anatengeneza hoja.

Neno "mtume" lenyewe humaanisha mtu ambaye amepewa agizo fulani na kutumwa akiwa na mamlaka kwa ajili ya kusudi maalumu. Ni aina ya jina la neno la Kiyunani *apostellö* ("kutuma"). Maana iliyo muhimu ya mtume" inaelezwa na maneno kama "balozi," "mwakilishi," au "mjumbe."

1. AJ hutambua aina mbili za msingi za mitume: (A) mitume *walio msingi*; na (B) mitume *waagizwao na kanisa*. Mitume "Walio msingi" ni wale mitume ambao walikuwa pamoja na Yesu, walioshuhudia ufufuo, na ambao waliitwa bayana kuwa mitume na mashahidi wa Yesu (ona **Math 10:1-5; Marko 6:7, 30; Luka 6:13; Yohana 15:27; Matendo 1:21-22**). Walijitoa wao wenyewe kwa maombi na huduma ya neno (**Matendo 1:14; 6:4**); walichagua mitume wa kuziba nafasi (**Matendo 1:21-26**); walifundisha na kuhubiri (**Matendo 2:42; 4:31, 33; 5:19-21; 6:4; 8:25; 10:42**); walifanya ishara, maajabu na kuponya (**Math 10:1-8; Marko 6:7; Matendo 2:43; 3:7; 5:15-16; 2 Kor 12:12**); waliitisha na kufanya mikutano ya kusanyiko (**Matendo 6:2**); waliagiza mashemasi (**Matendo 6:6**); walituma mitume na wapanda makanisa kwenye maeneo ya kimisheni (**Matendo 8:14; 11:22**); waliombea na kuwekea mikono waongofu wapya, ambao walipokea Roho Mtakatifu (**Matendo 8:15-17**); walisimulia maono kwa kanisa wakiwa katika nafasi ya mamlaka (**Matendo 11:1-18**); waliandika nyaraka kwa makanisa (**Mathayo, Yohana, 1-2 Petro, 1-3 Yohana, Ufunuo**); na walikuwa mamlaka yenye uamuzi wa mwisho kuhusiana na mabishano ya kitheolojia (**Matendo 15:1-29; 16:4**). Mitume wa msingi walikuwa ndio viongozi wa kanisa la kwanza na "msingi" wa kanisa lenyewe (**Efe 2:19-20**). Kama ilivyo, wale ambao walikuwa na mamlaka ya mitume wa msingi hawapo tangu mitume wa kwanza wafe (ni msingi mmoja tu unaweza wekwa kwa ajili ya jengo). Paulo alikuwa mtume wa msingi. Ingawaje hakuwa pamoja na Yesu (lakini, kwa kweli, alikuwa amelitesa kanisa), Kristo alimtokea (**Matendo 9:3-6, 17, 27; 1 Kor 9:1**), alikuwa

[1] Fahamu pia kwamba Paulo anautaja ufufuo wa Yesu Kristo bayana. Ufufuo ni jambo la hakika la kihistoria lililo kiini, kwa kuwa linadhihirisha kwamba Yesu yu zaidi ya mwanadamu lakini yu Mwana wa Mungu (m.y., Mungu aliyefanyika mwanadamu); pia unadhihirisha kwamba Mungu Baba aliikubali dhabihu ya Yesu ya yeye mwenyewe msalabani. Maana na ushahidi wa ufufuo vimejadiliwa kwa undani katika Menn 2015-2020: 30-40.

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

ameitwa kimahususi na Mungu kwa ajili ya huduma yake (**Matendo 13:2; Gal 2:2**), Kristo alikuwa amempa yeye ile injili kwa njia ya ufunuo maalum wa kiungu (**Gal 1:12**), na mamlaka yake yalikuwa yametambuliwa na wale viongozi wa kanisa katika Yerusalemu (**Gal 2:9**).

Mitume "walioatumwa na Kanisa" ni wale wanaume na wanawake ambao wamepewa jukumu na kanisa kutoka na kuhubiri injili, kupanda makanisa mapya, na kulijenga kanisa (ona **Matendo 13:1-3; 14:14; Rum 16:7; 1 Kor 9:5-6; 12:28; 1 Thes 1:1; 2:6**). Lile *kusudi* ambalo kwalo Kristo aliwapa baadhi ya watu vipawa na nafasi za uongozi (mfano, mitume, manabii, wainjilisti, na mchungaji-walimu) ni *"kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe"* (**Efe 4:12**). Kwa maneno mengine, wale ambao ni mitume (pamoja na manabii, wainjilisti, na mchungaji-walimua) wanapaswa kuhusika na washirika wa kanisa, na wanapaswa kuwafunza na kuwaimarisha washirika wa kanisa ili kwamba na wao wawe mitume, manabii, wainjilisti, na mchungaji-walimu. Hii inamaanisha kwamba, wakati ambapo Roho Mtakatifu anagawa karama za kiroho *"akimgawia kila mtu peke yake kama apendavyo yeye"* (**1 Kor 12:11**), na si wote ni mitume, manabii, walimu, n.k. (**1 Kor 12:29**), vipawa na uwezo wa mitume, manabii, wainjilisti, na mchungaji-walimu watu wanaweza kufundishwa na kuwa navyo na inabidi watu watamani kuwa navyo (ona **1 Kor 12:31; 14:1**).

Aina zote mbili za mitume ziko pamoja kwa mtu kama Paulo (ona **Matendo 9:1-16; 13:1-3; 1 Kor 9:1; 15:6-10; Gal 1:11-17; 1 Tim 2:7**). Mitume waliotumwa na Kanisa wanaweza wasiwe na mamlaka zaidi ya ile ya kule kutumwa na kanisa. Kanisa ni mwili wa Kristo duniani (**1 Kor 12:27; Efe 1:22-23; 4:15-16; Kol 1:18**). Kanisa ni hekalu la Roho Mtakatifu (**1 Kor 3:16-17**). Kristo ameliweka kanisa wakfu na kulipa mamlaka Yake (**Math 16:18-19**). Kwa hiyo, Kristo anaweza kutarajiwa kutenda kazi kupitia kanisa Lake, si bila ya hilo. Kwa kuwatuma mitume, kanisa pia huwapatia namna ya kuaminika na kuwajibika, kwa upande wa kanisa lenyewe na katika macho ya dunia.[2]

2. <u>Yesu akiwa amelianzisha kanisa kwa msingi wa wanafunzi 12/mitume 12 ambao ilikuwa ishara kwamba alikuwa anaanzisha Israeli mpya, ya kiroho.</u> Uchaguzi wa Yesu wa wanafunzi 12/mitume 12 (**Math 10:1-2; Marko 3:13-19; Luka 6:12-26**) ni ishara ya makabila 12 ya Israeli. Kwa kweli, katika malango kumi na mbili ya Yerusalemu Mpya yameandikwa *"majina ya kabila kumi na mbili za Waisraeli"* (**Ufu 21:12**), na mawe kumi na mbili ya msingi ya Yerusalemu Mpya ni *"majina kumi na mawili ya wale mitume kumi na wawili wa Mwana Kondoo"* (**Ufu 21:14**).[3] Mitume wenyewe walielewa umuhimu wa "Kumi na mbili." Katika **Matendo 1:12-26** walihitimisha kwamba ilikuwa ni lazima kuijaza nafasi ya Yuda Iskariote kama mtume. Ingawaje Paulo alikuwa mtume (**Rum 1:1; 1 Kor 1:1; 9:1**), AJ (na Paulo mwenyewe) hutambua utofauti uliopo kati ya utume wa Paulo na "wale Kumi na mbili" (ona **Matendo 6:2; 1 Kor 15:5, 8**). Hili linaweza kuhusiana na ukweli kwamba huduma ya Paulo kimsingi ilikuwa kwa Mataifa (**Matendo 9:15; 13:46; 18:6; Rum 11:13; Gal 1:16; 2:7**) na kwamba Paulo hakuwa pamoja na Yesu (lakini, kwa kweli, alilitesa kanisa), wakati ambapo Petro, kiongozi aliyekuwa dhahiri na mnenaji wa wale Kumi na mbili, kimsingi alikuwa mtume kwa Wayahudi

---

[2] Kanisa linahitaji kuwapima watu ambao hujiita "mitume" ili kuthibitisha kama wao ni mitume kweli au ni waongo (**1 Yohana 4:1-6;** ona pia **2 Kor 11:3-4, 13; Ufu 2:2**). Watu wengi leo wanapenda kujichagua wao wanyewe kama "mitume." Jambo hili linapingana na utaratibu wa AJ (Mitume wa AJ hawakujichagua wenyewe). Wengi wa hawa "mitume" wanaojichagua wenyewe hudai kwamba wanatenda miujiza. Hata hivyo, hata utendaji wa miujiza *sio* lazima iwe ni ushahidi kwamba mtu ameitwa na Mungu (**Math 7:15-23; 2 Tim 3:1-9** [ona **Kut 7:10-12, 20-22; 8:6-7, 16-19**]). Katika Afrika, "kuzuka kwa mitume na manabii wa Kiafrika kumewezesha kubainishwa kwa usawa kati ya watu weusi na weupe katika imani na huduma (Gal 3:28; Kol 3:11). Pia imeweka kanuni ya msingi ya kutenganisha imani ya Kikristo kutoka katika mahusiano yote ya siasa ya kikoloni." (Ouedraogo 2006: 1434) Kilicho kibaya, hata hivyo, "wengi kati ya mitume na manabii wa Kiafrika hawaichukulii Biblia kama ndio msingi wa imani yao na mwenendo. . . . Wanachukulia [kile wanachodai kuwa ni ufunuo wa moja kwa moja kutoka kwa Mungu] kuwa ni nyongeza ya Biblia. Hata hivyo, Biblia inaonya dhidi ya kufanya nyongeza hata ndogo katika Neno (Ufu 22:18-19). . . . Manabii na mitume wengi wa Kiafrika pia hupendelea kuabudiwa. . . . Hata wengine hudai kuwa wao ndio wamechukuwa nafasi ya Kristo au Kristo mwingine. Madai ya namna hiyo huwafanya wao kuwa ndio wakuabudiwa. Chakusikitisha, wengi wao wamechukuwa nafasi ya kutawala kabisa sehemu kubwa ya fahamu za wafuasi wao. AJ linatuonya dhidi ya watu kama hao (Math 24:11; Yuda 4-16)." (Ibid.) "Mitume" wa nyakati hizi yahitajika wapimwe kwa mafundisho yao (ona **Matendo 17:11; 1 Tim 6:3-5**) na mtindo wa maisha yao (ona **Math 20:25-28; Marko 10:42-45; Luka 22:24-27; Yohana 13:12-17; Matendo 18:3; 1 Kor 9:11-18; 2 Kor 11:7; 12:13**). Kanuni za kuwapima mitume na manabii na namna ya kukabiliana na manabii na mitume wa uongo zimejadiliwa katika Menn 2017: 40-42.

[3] "Cha kufaa kuzingatia katika kuangalia katika [Ufu] 21:14 ni kwamba mitume ni sehemu ya msingi, wakati ambapo makabila ni sehemu ya malango katika ukuta uliojengwa juu ya msingi. Mtu angetarajia kielelezo cha tofauti kwa kuwa Israeli ililitangulia kanisa katika historia ya ukombozi. Lakini kielelezo hicho kilicho kinyume hutambulisha ukweli kwamba utimilifu wa ahadi za Israeli hatimaye umetimizwa ndani ya Kristo, ambaye pamoja na ushahidi wa kitume katika kuitekeleza kazi yake, anaweka msingi wa hekalu jipya, kanisa, ambalo ni Israeli mpya." (Beale 1999a: 1070)

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

(ona **Gal 2:7-8**). Paulo anatambua kwamba kuokoka kwake na utume wake yalikuwa matendo ya neema ya kiungu. Kwa sababu Kristo alikuwa amemtokea na kumuita ingawaje alikuwa amelitesa kanisa, Paulo alijiita mtume *"aliyezaliwa si kwa wakati wake"* (**1 Kor 15:8**) na *"mdogo katika mitume"* (**1 Kor 15:9**).

- **1:3-5:** ***[3] Neema na iwe kwenu, na amani zitokazo kwa Mungu Baba, na kwa Bwana wetu Yesu Kristo; [4] ambaye alijitoa nafsi yake kwa ajili ya dhambi zetu, ili atuokoe na dunia hii mbovu iliyopo sasa, kama alivyopenda Mungu, Baba yetu. [5] Utukufu una yeye milele na milele, Amina.***

"Neema na amani" ni maneno ya salamu za Paulo (ona **Rum 1:7; 1 Kor 1:3; 2 Kor 1:2; Efe 1:2; Filp 1:2; Kol 1:2; 1 Thes 1:1; 2 Thes 1:2; Tito 1:4; Flm 1:3).** Ingawaje mistari hii ni sehemu ya utangulizi wa Paulo, inafanya mambo kadhaa. Ukiwa una muktadha wa mafundisho potofu ya Wayahudishaji, mistari hii ni tamko lenye nguvu kuhusiana na kile ambacho Mungu amekifanya. Kwa maneno mengine, wokovu wetu na maisha mapya msingi wake ni mapenzi ya Mungu peke yake (si ya kwetu), Neema ya Mungu (si matendo yetu), na kile ambacho yeye (ndani ya Yesu Kristo) amekitimiza msalabani. Wakati ambapo neema (m.y., upendeleo wa Mungu tusiostahili, tusioutendea kazi tunaopewa kama zawadi) ndio msingi wa wokovu wetu, Amani ni matokeo ya wokovu wetu. Kwa sababu wokovu wetu na maisha mapya hutoka kwa Mungu tu, *"utukufu una [yeye] milele"* (**mst. 5**).

Mistari hii miwili hasa inatupa muhtasari mfupi wa injili.[4] Neno "injili' humaanisha "habari njema." Kwa mahususi, "neno la Kiyunani 'injili' . . . lilikuwa habari za tukio kuu la kihistoria, kama vile ushindi katika vita au kuinuka kwa mfalme mpya, ambazo ziliibadilisha hali ya msikilizaji na zilidai mwitikio wa msikilizaji. Kwa hiyo injili ni habari za kile ambacho Mungu amekifanya kutufikia sisi. Sio ushauri kuhusu kile ambacho sisi tunatakiwa kukifanya ili tumfikie Mungu." (Keller n.d.: 1) Injili ni habari njema ya kuwa Mungu amefanya kwa ajili yetu kile ambacho kamwe tusingeweza kukifanya kwa ajili yetu wenyewe. Mungu alifanyika mtu ndani ya Yesu Kristo. Yesu aliishi yale maisha ambayo sisi tungepaswa kuishili *kama mtu*; alimtii Mungu Baba bila kukose katika kila kitu; *"alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi"* (**Ebr 4:15**). Hilo linamstahilisha yeye kuwa mwakilishi wetu, aichukue dhambi yetu juu yake na kulipia adhabu kwa ajili ya dhambi yetu vinginevyo tungelazimika sisi kulipa lakini tusingeweza (**Rum 8:1-4; 2 Kor 5:21; Gal 3:13; Kol 2:13-14; 1 Tim 2:5-6; 1 Pet 2:24**). Wakati huo huo, Yesu Kristo alikuwa Mungu. "Mungu hakumwadhibu mtu mwingine, kwa hiyo, bali badala yake pale Msalabani alichukua maumivu, mateso, na uovu wa dunia juu yake mwenyewe. . . . Kwa nini Yesu *alilazimika* kufa ili atusamehe? Lilikuwepo deni la kulipa—Mungu mwenyewe alililipa. Ilikuwepo adhabu iliyotakiwa kuchukuliwa—Mungu mwenyewe aliichukua. . . . Msalabani haikosekani haki wala rehema—vyote viwili hutekelezwa kwa wakati mmoja. Kifo cha Yesu kilikuwa cha lazima ikiwa Mungu angeitilia maanani haki na bado awe anatupenda." (Keller 2008: 192-93, 197)[5] Injili ni habari njema" kwa sababu ni kile ambacho Mungu katika Yesu Kristo alikifanya kwa ajili yetu, si kile ambacho sisi tunapaswa kufanya; kwa hiyo, kamwe hatutahitaji kuwa na shaka kwamba "tu wema vya kutosha."

Tamko katika **mst. 4** kwamba Kristo alijitoa ili *"atuokoe na dunia hii mbovu iliyopo sasa"* ladokeza katika athari za injili kwa ulimwengu. Biblia ina muundo wenye taarifa za kutosha za kitheolojia kwa habari za matukio ya nyakati za mwisho. Ule muundo ni zile "zama mbili" (Kiyunani = *aiōn* ["zama"]): *"zama hizi,"* na zile *"zama zijazo."* Kuna *utofauti wa ubora* kati ya zama hizi na zama zijazo. "Agano Jipya huziweka Zama Zijazo katika upinzani ulio dhahiri dhidi ya Zama Hizi. . . . Tunapouliza ni nini kile ambacho Maandiko yanakifundisha kuhusu sifa ya zama hizi mbili, tunapata utofauti mkubwa sana. Zama hizi zimetawaliwa na uovu, ufisadi, na uasi dhidi ya mapenzi ya Mungu, wakati ambapo Zama Zijazo ni za Ufalme wa Mungu. . . . Katika Zama Hizi kuna kifo; katika Ufalme wa Mungu, uzima wa milele. Katika Zama Hizi, wenye haki na waovu wako mahali pamoja; katika Ufalme wa Mungu, uovu wote na dhambi vitaharibiwa. Kwa wakati huu, Shetani anatazamwa kama 'mungu wa zama hizi;' lakini katika zile Zama Zijazo, Ufalme wa Mungu, utawala wa Mungu utakuwa umemharibu Shetani, na haki itachukuwa nafasi ya uovu." (Ladd 1959: 31, 28, 34) Pia kuna *tofauti ya wingi* kati ya zama hizi na zile zama zijazo. Zama hizi ni za muda mfupi, zenye ukomo, na zitafikia mwisho (**Math 13:39, 40, 49; 24:3; 28:20; Ebr 9:26**); zama zijazo zitakuwepo kwa kuendelea, pasipokuwa na mwisho (**Luka 1:33; 2 Pet 1:11; Ufu 11:15**). Mwisho, zama hizi mbili hujumuisha wakati wote, na zama zijazo huendelea mara baada ya zama hizi. **Efe 1:21** inasema kwamba Kristo yuko *"juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka, na nguvu, na usultani, na kila jina litajwalo, wala si ulimwenguni humu tu, bali katika ule ujao pia."*

[4] Mara nyingi Biblia ina mihutasari mifupi ya injili. Mihutasari mingine mifupi ya injili ni pamoja na **Yohana 3:16; Matendo 10:36-43; 13:32-33; 16:30-31; Rom 3:21-26; 5:8; 10:8-13; 1 Kor 15:1-8; Efe 2:8-10; Tito 3:4-7**.

[5] Asili ya injili na kile ambacho Kristo ametimiza msalabani vimejadiliwa kwa kirefu katika Menn 2015-2020: 83-87 na Menn 2017: 20-23.

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

Katika **Math 12:32** (ona pia **Marko 3:29**) Yesu anasema kwamba ye yote atakayesema kinyume na Roho Mtakatifu hatasamehewa *"iwe katika ulimwengu huu, au katika ulimwengu ujao."* Vifungu hivyo huonyesha kwamba hakuna kipindi cha mapumziko au kipindi cha muda cha kusubiri kati ya *"zama hizi"* na *"zama zijazo."*[6]

Ujio wa Kristo wa kwanza ulikuja pamoja na "kuingia" kwa nguvu za zama zijazo katika zama hizi (**Ebr 6:4-5**). Hivyo, wakati ambapo zama zijazo ni zama za uumbaji mpya (**Rum 8:18-22; Ufu 21:1-4**), kwa mantiki fulani uumbaji mpya umeshaanza ndani ya Kristo kwa kupitia utendaji wa Roho Mtakatifu (**2 Kor 5:17; Gal 6:15**). Wakati **mst. 4** unazungumzia kuhusu Kristo "*kutuokoa sisi kutoka katika dunia hii mbovu iliyopo sasa,"* unadokeza mambo mawili: Kwanza, ijapokuwa waamini wanaishi katika dunia hii, hatupaswi kuwa "wa dunia hii" (ona **Yohana 17:14-16**). Badala yake, tunapaswa kuwa *"tumefananishwa na mfano wa Mwana wake [Yesu Kristo]"* (**Rum 8:29**). Paulo anaitenga **Wagalatia 5-6** kwa ajili ya kujadili jinsi maisha yale ya kufananishwa na Yesu Kristo yanavyopaswa kuwa. Pili, **mst. 4** unaonyesha kwamba mwishowe "tutaokolewa kutoka katika dunia hii mbovu" moja kwa moja wakati Kristo atakapokuja tena, katika wakati ambapo dunia yote itafanywa upya, tutapokea miili mipya ya utukufu kama wa kwake, na dhambi yote, huzuni, na kifo vitaondolewa milele. Mambo haya yote ni matokeo ya injili.

MASWALI YA KUJADILI

1. Aina mbili za "mitume" ni zipi katika Biblia na kazi zao ni zipi?

2. Watu wengi siku za leo hujiita "mitume." Ni kwa njia gani baadhi ya hawa "mitume" wa sasa wanatofautiana na wazo la kibiblia la utume?

3. Je "neema" ni nini?

4. Je "injili" ni nini?

B. Gal 1:6-9—Sababu ya kuandika: Ikiwa mtu awaye yote anawahubiri "injili" isipokuwa niliyowahubiri, na alaaniwe milele.

[6] Nastaajabu kwa kuwa mnamwacha upesi hivi yeye aliyewaita katika neema ya Kristo, na kugeukia injili ya namna nyingine. [7] Wala si nyingine; lakini wapo watu wawataabishao na kutaka kuigeuza injili ya Kristo. [8] Lakini ijapokuwa sisi au malaika wa mbunguni atawahubiri ninyi injili yoyote isipokuwa tuliyowahubiri, na alaaniwe. [9] Kama tulivyotangulia kusema, na sasa nasema tena, mtu awaye yote akiwahubiri ninyi injili yoyote isipokuwa hiyo mliyoipokea, na alaaniwe.

Katika nyaraka zake zote Paulo ispaokuwa huu, baada ya kusalimia tu hutoa sifa na shukrani kwa Mungu, au maombi, au amri. Hapa tu hakufanya hayo bali badala yake anashughulikia, kwa namna ya uzito mkubwa, swala la injili ile potofu ambayo ilikuwa imefundishwa Galatia. In **mst. 6** Paulo anazungumza kuhusu Wagalatia "kumuacha" Mungu kwa kufuata injili nyingine. Neno (Kiyunani = *metatithēmi*) linatumika kuhusiana na askari kuzunguuka au kuondoka au watu kubadilisha upande fulani kisiasa. Katika matumizi yake mengine katika Biblia, neno hilo linatumika kuhusiana na badiliko kubwa la kutoka mahali hadi mahali pengine tofauti kabisa (**Matendo 7:16; Ebr 11:5**), badiliko la asili ya ukuhani ambao umeletwa na Kristo (**Ebr 7:12**), na watu kuipotosha neema ya Mungu (**Yuda 4**). Hoja ya Paulo ni kwamba kutokuelewa—na kufundisha kwa makosa—kile ambacho ni injili, si tu ni kosa la kitheolojia bali husababisha kumuacha au kutoka kwa Mungu mwenyewe.

Paulo anawekea mkazo hili katika **mst. 7** anapotaja wale ambao "*wanataka <u>kugeuza</u> [potosha; chafua] injili ya Kristo."* Neno lile (Kiyunani = *metastrephō*) limetumika mara nyingine mbili tu katika AJ. Lina maanisha badiliko kubwa la kitu kutoka kilivyo na kuwa kinyume chake. Hivyo, **Matendo 2:20** inasema, *"Jua litageuka kuwa giza."* **Yak 4:9** inasema, *"Kucheka kwenu na kugeuzwe kuwa kuomboleza."* Hapa, Paulo anasema kwamba mafundisho yale ambayo Wagalatia walikuwa wameyapokea (ambayo, kimsingi, yalisema "unaweza kuokoka kwa imani lakini utakaa katika wokovu kwa sheria") ujumla wake ni kurudi nyuma kiinjili. Hugeuza injili (ambayo, kimsingi, inasema kwamba "unaokolewa kwa neema kwa njia ya imani na kuendelea kuwepo katika wokovu kwa neema kwa njia ya imani") kuwa sio injili kabisa. Sababu, kama ilivyotajwa hapo nyuma, ni kuwa injili inahusu kile ambacho alikifanya Kristo kwa ajili yetu, si kile tulichofanya sisi ili kupata

[6] Vizazi viwili vimejadiliwa kwa kirefu katika 2010-2017: 20-25.

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

upendeleo wa Mungu. Hata kama ingekuwa kwamba wokovu ungetegemea 1% ya kile tunachofanya sisi, hakuna ambaye angeokoka, kwa sababu viwango vya Mungu ni ukamilifu (**Math 5:48**), hawezi kukaa katika uwepo wa dhambi (**Hab 1:13; Rum 1:18**), lakini mioyo yetu ni midanganyifu (**Yer 17:9**) na haiwezi kurekebishwa na sisi. Sisi wenyewe sote tu wachafu, wenye dhambi, hatuwezi kumpendeza Mungu (**Rum 3:9-18; 7:5, 8-11, 14-24; Gal 5:17; Ebr 3:12-13**). Kwa hiyo, hatuwezi kufikia viwango vya Mungu na hatuwezi kujiokoa wenyewe, iwe kwa ukamili au sehemu.

Umuhimu usio na shaka unaonyeshwa katika **mst. 8-9** pale ambapo Paulo anasema mara mbili kwamba ikiwa mtu awaye yote—hata malaika kutoka mbinguni—angehubiri injili tofauti na ile ambayo Paulo aliifundisha, *"na alaaniwe."* Neno lililotumika kwa "alaaniwe" (Kiyunani = *anathema*) linamaanisha kulaaniwa au kutengwa na kuwekwa kwenye hukumu ya kiungu. Kwa maneno mengine, Paulo anasema, "Awaye yote akihubiri injili potofu, *na aende jehanum!*"[7]

MASWALI YA KUJADILI

1. Ni kwa nini kuielewa kwa usahihi na kuifundisha injili ya kweli ni muhimu sana?

2. Je tatizo la walimu wa uongo ni kubwa kwa kiasi gani ndani ya kanisa siku za leo? Tulikabili namna gani swala hili?

C. Gal 1:10-2:21—Huduma na ujumbe wa Paulo: Wayahudi na Mataifa sawasawa wanahesabiwa haki kwa imani katika Kristo peke yake, si kwa sheria.

Sehemu yote kuhusiana na maisha ya Paulo kama inavyoonekana katika **Gal 1:10-2:10** inadhihirisha kwamba maisha yake yote yalikuwa ni utetezi kwa ajili ya Kristo na injili:

- **1:10**: hakuna kutafuta maslahi binafsi = ombi la kutumia akili
- **1:11-12**: injili ilifunuliwa kiungu = ombi kwa Mungu na ufunuo maalumu
- **1:13-19, 21-22**: mtindo ulio tofauti kabisa = ombi kwa matokeo ya Kristo na injili katika maisha yake
- **1:20**: kiapo mbele za Mungu = ombi la uadilifu wa binafsi
- **1:23-24**: matunda ya Kimungu = ombi la matokeo ya Kristo na injili kwa wengine
- **2:1-10**: uthibitishaji kwa njia ya viongozi wanaotambulika = ombi kwa mamlaka

Utaratibu wa maisha ya Paulo kama Mkristo, kabla ya na mara baada ya kuandika Wagalatia, kama ilivyoonyeshwa katika Wagalatia na Matendo unaweza kulinganishwa na kufupishwa kama ifuatavyo:

Tukio	Wagalatia	Matendo
Kuokoka kwa Paulo	1:15-16a	9:1-19a
Kukaa Dameski	1:17	9:19b-22
Kutembelea Arabuni	1:17	-----
Kurudi Dameski	1:17	-----
Safari ya kwanza Yerusalemu	1:18-24	9:26-29
Anakwenda Shamu na anarudi nyumbani Tarso (katika Kilikia)	1:21	9:30
Safari ya pili (msaada kwa ajili ya njaa na mkutano wa viongozi)[8]	2:1-10	11:27-30; 12:25

[7] Paulo alitamani katika maeneo mengine mawili ya kwamba watu wangelaaniwa. Katika **1 Kor 16:22** alisema kwamba *"ikiwa mtu awaye yote hampendi Bwana na alaaniwe."* Hilo huonyesha kwamba wale walimu wa uongo waliokuwa wakiichafua injili katika Galatia ni sawasawa na wale ambao hawampendi Bwana. Katika **Rom 9:3** alitamani kwamba, yeye, mwenyewe alaaniwe ikiwa kwa njia hiyo angeweza kuwapata ndugu zake Wayahudi kwa Kristo. Jambo hilo huonyesha moyo wake na kwa kiwango gani alijisikia kwa ajili ya ndugu zake waliopotea.

[8] Wana zuoni kadhaa hushikilia kwamba mkutano huu wa Yerusalemu ulikuwa ndio lile Baraza la Yerusalemu la **Matendo 15**, si mkutano wa binafsi kati ya Paulo na viongozi wa kanisa Yerusalemu. Ikiwa ndivyo hivyo, basi Paulo aliandika Wagalatia baada ya Baraza la Yerusalemu, sio kabla. Hilo halionyesha kuwa sahihi, kwa hali yoyote, kwa sababu Baraza la Yerusalemu ulikuwa mkutano wa maana sana katika historia ya kanisa. Ulithibitisha nafasi ya Paulo. Bila shaka Paulo angeutaja ule mkutano katika Wagalatia kama angeandika Wagalatia baada ya lile Baraza. Kwa hiyo, kwa kutolitaja lile Baraza, ni ushahidi wenye nguvu kwamba aliandika Wagalatia kabla ya lile Baraza kufanyika. Ushahidi mwingine kutoka katika **Galatians 2** na **Matendo 15** unaonyesha kwamba safari ya pili ya Paulo kwenda Yerusalemu ilikuwa kabla ya safari inayoelezwa katika **Matendo 15**. Kwa mfano, **Gal 2:1** inasema kwamba Paulo alikuwa ameambatana na Barnaba na Tito

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

Safari ya Kwanza ya kimishenari	-----	13:1-14:28
Kuandika Wagalatia	-----	-----
Safari ya tatu (Baraza la Kanisa)	-----	15:1-35

- **1:10-12—**Paulo alivyoipokea injili.

[10] Maana, sasa je! Ni wanadamu ninaowashawishi, au Mungu? Au nataka kuwapendeza wanadamu? Kama ningekuwa hata sasa nawapendeza wanadamu, singekuwa mtumwa wa Kristo. [11] Kwa maana, ndugu zangu, injili hiyo niliyowahubiri, nawajulisha ya kuwa siyo ya namna ya kibinadamu. [12] Kwa kuwa sikuipokea kwa mwanadamu, wala sikufundishwa na mwanadamu bali kwa ufunuo wa Yesu Kristo.

Katika mistari hii, Paulo anatamka chanzo cha injli: *"siyo ya namna ya kibinadamu,"* lakini Paulo aliipokea moja kwa moja kwa njia ya *"ufunuo wa Yesu Kristo."* Kwa kurudia kwamba *"injili hiyo niliyowahubiri, nawajulusha ya kuwa siyo ya namna ya kibinadamu"* na *"Kwa kuwa sikuipokea kwa wanadamu wala sikufundishwa,"* Paulo anawekea mkazo utume wake wa kiungu ambao ulikuja moja kwa moja kutoka kwa Yesu Kristo. Anarudia kudokeza katika **mst. 15-16a**. Hiki *chanzo* cha kiungu cha injili kinakwenda pamoja na asili ya kiungu ya injili. Kila dini ambayo ipo hapa dunia kimsingi husema, "Ikiwa unamtaka Mungu au miungu akukubali na kukuchukuwa mbinguni, ni jukumu lako *wewe*—kutoa dhabihu za kutosha, na fanya matendo mema ya kutosha, na jinyime vitu mbalimbali." Zaidi ya hapo, kila dini iliyoko dunia ilianzishwa na mtu fulani ambaye kimsingi alisema, "Mimi siye Mungu, lakini nitakuambieni kile ambacho mnahitajika kufanya ili Mungu awakubali." Ukristo ni kinyume cha hayo yote. Katika Ukristo, Yesu alisema, "Mimi ni Mungu ambaye amekuja kuwatafuta." Ukristo peke yake unasema *hakuna* tunachotakiwa kufanya ili tuupate wokovu: hatuwezi kamwe kutoa dhabihu za kutosha, kufanya mambo mema ya kutosha, au kujinyima vitu vya kutosha. Badala yake, katika Ukristo, wokovu msingi wake ni kile alichofanya Kristo kwa ajili yetu100%. Sisi twaweza kuupokea wokovu tu kama zawadi ya neema yake.

- **1:13-14—**Maisha ya Paulo kabla ya kubadilika kiimani.

[13] Maana mmesikia habari za mwenendo wangu zamani katika dini ya Kiyahudi, kwamba naliliudhi kanisa la Mungu kupita kiasi, nikaliharibu. [14] Nami naliendelea katika dini ya Kiyahudi kuliko wengi walio hirimu zangu katika kabila yangu, nikajitahidi sana katika kuyashika mapokeo ya baba zangu.

Maisha ya Paulo katika Dini ya Kiyahudi yamekuwa ni ya kujifunza, mamlaka na nguvu. Katika **Filp 3:4-6** alisema, *"Mtu ye yote akijiona kuwa anayo sababu ya kuutumainia mwili, mimi zaidi. [5] Nilitahiriwa siku ya nane, ni mtu wa taifa la Israeli, wa kabila la Benjamini, Mwebrania wa Waebrania, kwa habari ya kuishika torati, ni Farisayo, [6]kwa habari ya juhudi, mwenye kuliudhi kanisa, kwa habari ya haki ipatikanayo kwa sheria sikuwa na hatia."* Katika **Matendo 22:3-5** aliongezea, *"[3] Mimi ni mtu wa Kiyahudi, nalizaliwa Tarso, mji wa Kilikia, ila nililelewa katika mji huu [Yerusalemu], miguuni pa Gamalieli[rabi aliyekuwa akiongoza wakati ule], nikafundishwa sheria ya baba zetu kwa usahihi, nikawa mtu wa jitihadi kwa Mungu kama ninyi nyote mlivyo leo hivi; [4] Nikawaudhi watu wa Njia hii hata kuwauwa, nikawafunga, nikawatia gerezani, wanaume kwa wanawake. [5] Kama kuhani mkuu naye anishuhudiavyo, na wazee wa baraza wote pia, ambao nalipokea barua kwao kuwapelekea ndugu wale, nikaenda Dameski, ili niwalete wale waliokuwa huko hata Yerusalemu, hali wamefungwaw, ili waadhibiwe."* Hata Paulo alikuwepo wakati mfia imani wa kwanza wa kanisa, Stephano alipokuwa akipigwa kwa mawe hadi kufa (**Matendo 7:58-8:1;** ona **Matendo 22:20**). Aliielezea ile hali yake alivyokuwa kabla ya kuongoka ya kuwa alikuwa *"mtukanaji, mwenye kuudhi watu, mwenye jeuri* (**1 Tim 1:13**). Mtazamo wake ulikuwa kama ule wa Mwislamu wa siku za leo anayepigana jihadi.

---

kwenda Yerusalemu, wakati ambapo **Matendo 15:2** inasema kwamba Paulo alikuwa ameambatana na Barnaba na "wengine kadhaa." Katika **Gal 2:2** Paulo anasema kwamba mkutano wake na viongozi wa Yerusalemu ulikuwa kwa "ufunuo" na ulikuwa "wa binafsi," wakati ambapo katika **Matendo 15:2** Paulo alitumwa na kanisa kwenda Yerusalemu, na lile Baraza la Yerusalemu lilikuwa la hadhara (**Matendo 15:12**). **Gal 2:9** inasema kwamba uongozi ambao Paulo alikutana nao kule Yerusalemu ni pmoja na Yohana, wakati ambapo katika **Matendo 15** Yohana hatajwi. Mwisho, Paulo alimkemea Petro katika **Gal 2:11-14**, wakati ambapo katika **Matendo 15:7-12** Petro na Paulo walikuwa wanaelewana. Kwa kuongezea, David Trobisch kwa kushawishi anaonyesha kwamba **Gal 2:1-10** na **Matendo 11:27-30** zinakubaliana (Trobisch 1999: 336-37). "Ufunuo" wa Paulo (**Gal 2:2**) pengine ulikuwa ukimzungumzia nabii Agabo ambaye alitabiri kuhusu njaa ijayo "kwa Roho" (**Matendo 11:28**).

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

- **1:15-16a—**Kubadilika kiimani kwa Paulo.

[15] Lakini Mungu, aliyenitenga tangu tumboni mwa mama yangu, akaniita kwa neema yake, [16] alipoona vema kumdhihirisha Mwanawe ndani yangu, ili niwahubiri Mataifa habari zake.

Kubadilika kiimani kwa Paulo kunaelezewa katika **Matendo 9:1-30** (ona pia **Matendo 22:1-16; 26:1-20**). Katika mistari hii miwili Paulo anaweka mkazo ya kuwa kuokoka kwake (wokovu)—na, kwa upana zaidi, kuokoka kwa ye yote—hutoka kwa Mungu: Mungu *humtenga* mtu kwa ajili yake yeye Mungu; Mungu *humuita* mtu kwa kupitia *neema* ya Mungu; na Mungu *hujifunua* yeye mwenyewe kwa mtu kwa ajili ya *furaha* na *kusudi* lake Mungu. Mistari hii inafunua mambo kadhaa muhimu kuhusu asili ya wokovu wa kweli:

1. Wokovu wa kweli unahusisha uingiliaji kati wa Mungu. Paulo amekuwa akiyaelezea maisha yake kabla ya kuokoka kama Myahudi katika **mst. 13-14**, lakini **mst. 15** unaanza na lile neno muhimu "Lakini." Tumedokeza jinsi Ukristo, tofauti na dini nyinginezo, msingi wake uko katika kile alichokifanya Mungu kwa ajili yetu kupitia Yesu Kristo, sio kile tunachokifanya kwa ajili ya Mungu. Katika shauri la Paulo, Mungu kwa namna ya kupendeza aliingilia kati na kuubadilisha kabisa uelekeo wote wa maisha ya Paulo. Hili limeonyeshwa katika kutofautiana kwa lugha kati ya **mst. 13-14** na **mst. 15**. Wakati Paulo anayajadili maisha yake ya kwanza, ya kutookoka kama Myahudi, anatumia maneno "Nami' na "yangu" kwa kurudiarudia. Hata hivyo, anapozungumzia kuhusu kuokoka kwake, mkazo uko katika maneno "Mungu" na "Mwana wake."

2. Wokovu wa kweli unahusisha mpango wa kimilele wa Mungu. Mistari hii pia inatoa sababu nyingine ni kwa nini tunajua kwamba wokovu msingi wake uko mikononi mwa Mungu, si kwetu: hili ni, fundisho la *uchaguzi* na *majaaliwa* ya Mungu. Katika **mst. 15** Paulo anasema kwamba Mungu *"aliyenitenga tangu tumboni mwa mama yangu."* Hili linakubaliana na mifano mingine ambapo imetamkwa kwamba mtu fulani aliitwa au kutengwa hata kabla ya kuzaliwa (ona **Isa 49:1** [Masihi]; **Yer 1:5** [Yeremia]; **Luka 1:15** [Yohana Mbatizaji]; **Rum 9:10-13** [Yakobo]). Hili pia linakubaliana na matamko mengine ya kiujumla ya kwamba wale waliookoka majina yao yalishaandikwa katika kitabu cha uzima *"tangu kuumbwa ulimwengu"*: **Math 25:34** (*"Kisha mfalme atawaambia wale walioko mkono wake wa kuume, 'Njoni, mliobarikiwa na Baba yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu."*); **Efe 1:4** (*"Kama vile alivyotuchagua katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ili tuwe watakatifu,watu wasio na hatia mbele zake katika pendo"*); **2 Tim 1:9** (Mungu *"ambaye alituokoa akatuita kwa mwito mtakatifu, si kwa kadiri ya matendo yetu sisi, bali kwa kadiri ya makusudi yake yeye na neema yake. Neema hiyo tulipewa katika Kristo Yesu tangu milele"*); **Ufu 13:8** (*"Na watu wote wakaao juu ya nchi watamsujudu, kila ambaye jina lake halimkuandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo, aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya dunia"*); **Ufu 17:8** (*"Na hao wakaao juu ya nchi, wasioandikwa majina yao katika kitabu cha uzima tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, watastaajabu wamwonapo yule mnyama"*). Wakati ambapo kuamini kwetu na kumpokea Kristo lazima kutokee kwa wakati muafaka, tukio lote la wokovu—ikiwa ni pamoja na kifo chake Kristo msalabani—ni *"kwa shauri la Mungu lililokusudiwa, na kwa kujua kwake tangu zamani"* (**Matendo 2:23**; ona pia **Matendo 4:27-28**).

3. Wokovu wa kweli huhusisha wito wa Mungu. Neno "wito" (Kiyunani = *kaleō*) linaweza kutumiwa kwa maana ya kiujumla ya "kukaribisha" (ona, mfano, **Math 22:3; Yohana 2:2**). Linaweza pia kutumika katika maana iliyo ya ki-amri, kimamlaka, yenye kuathiri. Hii ndiyo maana ambayo "wito" limetumika katika **mst. 15**: Wito wa Mungu ulitosha kusababisha mwitikio wa wokovu utokanao na imani ndani ya Paulo (ona pia **Rum 1:6; 8:28-30; 9:24; 1 Kor 1:9, 24, 26; 7:18, 21; Efe 4:1, 4; 2 Thes 2:14**). The *Westminster Confession of Faith* (1647) hueleza mashauri haya namna hii kwa kifupi:

> "Wale wote ambao Mungu amewajaalia kupata uzima, na hao tu, Aliamua katika wakati wake alioupanga na uliokubalika kwamba awaite, kwa Neno lake na Roho, kutoka katika hali ya dhambi na mauti, ambayo ndiyo waliyonayo kwa asili, kwenda kwenye neema na wokovu kwa Yesu Kristo; akiwatia nuru fahamu zao kiroho na kwa kuwaokoa waelewe mambo ya Mungu, akichukua moyo wao wa jiwe, na akiwapa moyo wa nyama; akifanya upya utashi wao, na kwa nguvu Zake kuu akiyakusudia yale yaliyo mema kwa ajili yao, na hatimaye kuwaleta kwa Yesu Kristo: ingawa bado, wakiwa wanakuja kwa uhuru wao, wakifanywa wawe na utashi kwa neema Yake." (*Westminster* 1647: ch. X.1)

Hili linakubaliana na kifungu kama hiki **Efe 2:8-9** ambacho husema tunaokolewa kwa neema ya Mungu kwa njia ya imani, lakini hata ile imani si ya kwetu sisi bali ni kipawa cha Mungu.

4. Wokovu wa kweli huhusisha neema ya Mungu. Paulo anaongezea kuwa Mungu alimwita *"kwa neema Yake."* Kama tulivyodokeza hapo awali, swala la neema ya Mungu (kinyume na matendo yetu) ndicho kinachotofautisha Ukristo na injili na dini nyingine zote duniani. Ni Ukristo peke yake unaosema *hatuna* kitu cha kufanya ili tuupate wokovu wetu. Badala yake, wokovu wetu una msingi katika kile ambacho Kristo amekifanya kwa ajili yetu 100%. Tunaweza tu kuupokea wokovu kama zawadi ya neema Yake.

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

5. Wokovu wa kweli huhusisha kuuona utukufu wa Kristo. Katika kumuita Paulo, Mungu *"alipoona vema kumdhihirisha Mwanawe ndani yangu."* Tafsiri nyingine hutafsiri hivi *"kwa mimi."* Vyovyote iwavyo, "uhalisia wa kushangaza wa Yesu Kristo—aliyesulibiwa, aliyefufuka, aliyepaa na anayetawala—ulidhihirishwa kwa Paulo" (Platt na Merida 2014: 34). Kimsingi wokovu na injili huhusika na kiini chake ni Mwana, Yesu Kristo (ona **Rum 1:1-4**). Kama Paulo alivyosema katika **2 Kor 4:6**, Mungu *"aliyeng'aa mioyoni mwetu, atupe nuru ya elimu ya utukufu wa Mungu katika uso wa Yesu Kristo."* Zaidi ya hapo, waaminio hawako peke yao tena (**Ebr 13:5**) na wao si mali yao wenyewe tena (ona **Matendo 20:28; 1 Kor 6:20; 7:23; Tito 2:14; 1 Pet 2:9; 2 Pet 2:1; Ufu 5:9**). Badala yake, kama Paulo anavyoiweka katika **Gal 2:20**, *"Wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu."*

6. Wokovu wa kweli huhusisha kuitwa kwa kusudi. Mungu anamdhihirisha Mwana Wake kwa Paulo kwa kusudi (m.y., ili aweza kumhubiri miongoni mwa Mataifa). Maisha ya Paulo yalibadishwa kikwelikweli na wokovu wake. Kutoka kuwa mtesaji wa Wakristo na kuwa anayeteswa (na hatimaye kukatwa kichwa) kwa sababu alikuwa Mkristo (ona **2 Kor 11: 23-33**). Hili linakubaliana na kifungu cha maneno kama **Efe 2:8-10** ambacho husema ya kuwa tumeokolewa na neema ya Mungu kwa njia ya imani kwa sababu, ambayo ni, "*tutende matendo mema, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza [m.y. kabla ya misingi ya dunia] ili tuenende nayo"* (ona pia **Yohana 15:16; Efe 1:11-12; Yak 1:18**). Hili litufanye tutambue ya kwamba sisi, kama Paulo, tumeitwa kwa kusudi *"tupate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyetuita tutoke gizani tukaingie katika nuru yake ya ajabu"* (**1 Pet 2:9**) na kuudhihirisha ubora wa Kristo kwa njia ya kuwa*"watu wasiolipa baya kwa baya, au laumu kwa laumu; bali wenye kubariki; kwa sababu hayo ndiyo mliyoitiwa ili mrithi baraka"* (**1 Pet 3:9**).

- **1:16b-24—**Maisha ya Paulo mara tu baada ya kubadilika kiimani na mkutano wake wa kwanza na uongozi wa Yerusalemu.

[16b] Mara sikufanya shauri na watu wenye mwili na damu; [17] wala sikupanda kwenda Yerusalemu kwa hao waliokuwa mitume kabla yangu; bali nalikwenda zangu Arabuni, kisha nikarudi tena Dameski. [18] Kisha, baada ya miaka mitatu, nalipanda kwenda Yerusalemu ili nionane na Kefa, nikakaa kwake siku kumi na tano. [19] Lakini sikumwona mtume mwingine, ila Yakobo, ndugu yake Bwana. [20] Na hayo ninayowaandikia, angalieni, mbele za Mumgu, sisemi uongo. [21] Baadaye nalikwenda pande za Shamu na Kilikia. [22] Lakini sikujulikana uso wangu na makanisa ya Uyahudi yaliyokuwa katika Kristo; [23] ila wamesikia tu ya kwamba huyo aliyetuudhi hapo kwanza, sasa anaihubiri imani ile aliyoiharibu zamani." [24] Wakamtukuza Mungu kwa ajili yangu.

Kutokana na **Matendo 9:19-20**, mara tu baada ya kuokoka kwake, Paulo alibaki Dameski (hapo alipokuwa amekusudia kwenda kuwatesa Wakristo wakati Kristo alipomtokea) *"akamhubiri Yesu katika masinagogi, kwamba 'yeye ni Mwana wa Mungu.'"* Zaidi ya hayo, alihojiana na Wayahudi na aliwashangaza *"akithibitisha ya kuwa huyu ndiye Kristo"* (**Matendo 9:22**). Hili huonyesha kwamba Paulo aliielewa injili vizuri sana kutoka katika ufunuo wa Yesu hadi kwake hata akaweza kutangaza na kuhojiana kwa ajili ya Kristo. Kutaja kwake katika **mst. 18-19** kuhusiana na kwenda Yerusalemu kukutana na Kefa (Petro) na Yakobo bila shaka inahusu **Matendo 9:26-29**. Katika **mst. 21**, kwenda kwake katika eneo la Kaisaria na Kilikia kunaonekana katika **Matendo 9:30** ambapo husema baadhi ya Wayahudi wa Kiyunani katika Yerusalemu walijaribu kumuua Paulo, kwa hiyo waamini *"wakamchukuwa mpaka Kaisaria, wakampeleka aende Tarso."* Tarso iko katika jimbo la Kilikia.

Maisha ya Paulo yanaonyesha jinsi ambavyo injili ya kweli inavyoathiri sio wewe tu bali pia na wale ambao unawashawishi. Katika swala la Paulo, kwa kuwa yeye alilitesa kanisa, mwanzoni waamini wengi walikuwa hawamwamini au hata walimwogopa (**Matendo 9:13-14, 26**). Hata hivyo, haikuchukuwa muda mrefu kwa tunda la Roho kuonekana ndani ya maisha ya Paulo, kiasi kwamba watu walisikia kuhusu Paulo na kuhusu badiliko lake *"Wakamtukuza Mungu kwa ajili yake"* (**Gal 1:24**). Maisha yetu sisi yanapashwa kufanana na haya. Tunapaswa kuwa watu wenye maadili ambao hatuihubiri injili kwa ajili ya kupata faida ya binafsi. Tunapaswa kuonyesha mabadiliko katika mtindo wa maisha yetu na tunapashwa kuzaa matunda yanayofanana na injili. Tunahitaji kujiuliza: "Je watu wanamtukuza Mungu kwa sababu *yangu*?"

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

- **2:1-10—** Mkutano wa pili wa Paulo na uongozi wa Yerusalemu.

    - **mst. 1-5:** ***[1] Kisha, baada ya miaka kumi na minane, nalipanda tena kwenda Yerusalemu pamoja na Barnaba, nikamchukua na Tito pamoja nami. [2] Nami nalikwenda kwa kuwa nalifunuliwa, nikawaeleze injili ile niihubiriyo katika Mataifa, lakini kwa faragha kwa hao wenye sifa, isiwe labda napiga mbio bure au nalipiga mbio bure. [3] Lakini Tito aliyekuwa pamoja nami naye ni Myunani, hakulazimishwa kutahiriwa. [4] Bali kwa ajili ya ndugu za uongo walioingizwa kwa siri; ambao waliingia kwa siri ili kuupeleleza uhuru wetu tulio nao katika Kristo Yesu, ili watutie utumwani; [5] ambao hata saa moja hatukujitia chini yao, ili kwamba kweli ya injili ikae nanyi.***

Kwa namna fulani haiko wazi kwamba ile miaka kumi na minne inayotajwa katika **mst. 1a** ilikuwa baada ya kuokoka kwake au baada ya safari yake ya kwanza kwenda Yerusalemu. Swala lililoko katika **mst. 1-5** kuhusu ikiwa Tito (Myunani, sio Myahudi) atahiriwe ni mfano mojawapo wa madai ya "ndugu wa uongo" (wale Wayahudishaji) ambayo ni kiini katika Wagalatia na walikuwa kiini cha ile sababu ambayo ilisababisha Baraza la Yerusalemu lilikaa katika **Matendo 15** (ona **Matendo 15:1**, *"Wakashuka watu waliotoka Uyahudi wakawafundisha wale ndugu ya kwamba, 'Msipotahiriwa kama desturi ya Musa hamwezi kuokoka'"*). Paulo alikataa Tito kutahiriwa (**mst. 3**). Alitambua kwamba akifanya hivyo italeta *"kuwatia utumwani"* (**mst. 4**). Hili lingekuwa "utumwa wa Sheria" ambao kwa huo Paulo ametumia sehemu kubwa ya waraka huu kuupinga (ona **Gal 2:4; 3:10, 23; 4:21-26; 5:3, 18;** ona pia **Rum 7:6**). Rich Lusk anaelezea, "Tohara, ni wazi, halikuwa ndilo tatizo pekee, lakini lilikuwa ndilo kubwa zaidi na alama ya kipekee ya Dini ya Kiyahudi. . . . Tohara ilikuwa jambo kubwa kwa sababu ilikuwa ndiyo alama yan kumuingiza mtu katika uanafunzi wa Musa. . . . Paulo hataki Wakristo wa Galatia kukubali kutahiriwa kwa sababu kwa kufanya hivyo watakuwa kimsingi wameikana kazi ya Kristo. Kwa kupitia kifo chake na kufufuka, Kristo aliifuta kabisa sheria, pamoja na vikwazo vyake vya kuufikia uwepo wa Mungu (fikiria kuhusu lile pazia ndani ya hekalu) na vikwazo vyake kati ya watu wa Mungu (fikiria kuhusu ule mfumo wa yale madaraja ya kuingia katika hekalu). Kwa kuendelea kufanya tohara kama ishara ya kuingia katika agano kutamaanisha kwamba kazi ya Kristo ilikuwa ina upungufu au kasoro. Kwa hiyo, tohara haikupaswa kufanywa. Yesu alikuwa ameshaufungua mlango wa agano kamili kwa Mataifa kama ilivyo, kwa mujibu wa ahadi za kale (Mwz. 12:1ff, n.k..). . . . Kwa Wayahudishaji, kuwa chini ya Torati = chini ya neema. Lakini kwa Paulo, wigo wa Torati hauko mpana kwa kiwango kile cha neema ya Mungu. Ndani ya Kristo, neema inapatikana pia kwa wale ambao *hawako* chini ya Torati." (Lusk 2003: n.p.)

Kwa upande mwingine, katika safari yake Paulo ya pili ya Kimisionari, alikuwa pamoja na Timotheo, mwana wa mama wa Kiyahudi na baba wa Kiyunani (**Matendo 16:1**). Katika tukio hili, *"Paulo akamtaka huyo afuatane naye'akamtwaa akamtahiri kwa ajili ya Wayahudi waliokuwako pande zile; kwa maana walijua ya kuwa babaye ni Myunani"* (**Matendo 16:3**). Paulo angeweza kuhukumiwa kwa kutokuwa na msimamo kwa sababu hakuruhusu Tito atahiriwe lakini akamtahiri Timotheo. "Lakini kutokana na mtazamo wa Paulo, matukio yote yalifanyika kwa kanuni za msingi. Alikataa kuruhusu Tito kutahiriwa katika muktadha wa Ukristo mahali ambapo kutahiriwa kungeashiria kwamba Tito (na Paulo, pia) walikubali kwamba mtu alihitaji kuwa Myahudi hasa ili amkubali Masihi wa Kiyahudi—na hilo lingehatarisha ule utoshelevu wa kipekee wa Kristo. Katika muktadha wa sinagogi la Kiyahudi, hata hivyo, mahali ambapo Paulo alikuwa akijaribu kuwaleta watu kwa Kristo kwa ushupavu na hakuna hata mmoja aliyekuwa akisoma yatokanayo na mtu kuwa Mkristo, kutahiriwa kwa Timotheo kulikuwa ni sehemu tu ya ule utashi wake wa 'kuwa vitu vyote kwa watu wote ili kwamba kwa njia zozote ziwezekanazo [a]weze kuwaokoa baadhi yao' (1 Kor 9:22)." (Carson and Moo 2005: 468n.31)

Swala hili ni muhimu sana kiasi kwamba katika **mst. 4** Paulo anawaita wale Wayahudishaji "ndugu za uongo," ambalo humaanisha kwamba fundisho lao limewaweka nje ya imani. Hilo limethibitishwa katika **mst. 4** ambapo anaongezea kwamba wali-"ingia kwa siri" (au "penyeza") ambalo ni neno "lililotumika kama wasaliti ambao hujifanya kwamba wao ni sehemu ya kundi ili waweze kupeleleza na kulidhoofisha" (Ngewa 2006: 1417). Swala lilikuwa *"kweli ya injili"* (**mst. 5**). Paulo alikuwa anasema kwamba uhuru unakuja kutoka katika njia ya kweli na misingi yake ni kweli. Ingawaje tohara au sheria ya Kiyahudi yaweza isiwe ndilo swala tunalolikabili siku za leo, sisi kama watu na makanisa tuna ile hali ya kuzusha sheria zetu wenyewe ambazo zinatutaka tufanye au tusifanye vitu fulani. Tunapofuata hizi sheria ambazo zimewekwa na wanadamu tunafikiri kwamba tunapata ile hali ya kukubaliwa na Mungu. Hiyo ni hali tu ya kufuata sheria sana. Kujiwekea sheria hulazimisha makosa mawili yaliyo kinyume cha injili ya kuwa tohara inatetewa na Wayahudishaji ilitaka: (1) kuongeza mahitaji kwa ajili ya wokovu na ni nani ndiye mshiriki sahihi wa agano la wana jamii ya Kristo zaidi ya kile ambacho Kristo alikifanya kwa ajili yetu; na (2) kugawanya mwili wa Kristo. Maneno ya Paulo yanapaswa kusimama kama onyo kali kwa wale wanaojiita Wakristo kujiepusha na hali hii ya kujiwekea sheria.

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

Kwa kuwa uhuru huja kutoka katika kweli na misingi yake ni kweli, vifungo vya sheria zilizowekwa na wanadamu humaanisha kwamba kanisa limetoka kutoka katika kweli na limetoka kutoka katika injili.

Swala la injili dhidi ya ushikiliaji mno wa sheria linaathiri tabia yetu vile vile. Paulo anazungumza kuhusu "*uhuru wetu tulio nao katika Kristo Yesu"* (**mst. 4**) dhidi ya "kifungo" ambacho hutokea tunapokuwa "chini ya sheria" (ona **Gal 2:4; 3:10, 23; 4:21-26; 5:3, 18;** ona pia **Rum 7:6**). Watu wengi hufikiri kwamba injili ya uhuru ndani ya Kristo huishia kwenye kutupa kibali cha kufanya chochote tutakacho. Hilo si sahihi. Uhuru wetu kama Wakristo si wa kibinafsi, yaani ule uhuru wa "fanya chochote utakacho" kile *"ndani ya Kristo Yesu."* Ni kitu kama ndoa yenye upendo: mtu anapoingia katika ndoa, hawezi kufanya chochote atakacho wakati wowote atakao na ye yote atamkaye. Na bado kwa hiari yetu tunauacha ule uhuru wa kibnafsi kwa ajili ya ule uhuru ulio mkubwa zaidi, unaoletwa na ndoa wa amani, ulinzi, na upendo. Kristo ni bwana arusi wetu (**Math 9:14-15; Marko 2:18-20; Luka 5:33-35; Yohana 2:9; 3:29; 2 Kor 11:2; Efe 5:25-27; Ufu 19:7; 21:2; 22:17**) na sisi ni bibi arusi wake na mke (**2 Kor 11:2; Efe 5:25-27; Ufu 19:7-8; 21:2, 9-10**). Kwa hiyo, kama Wakristo tuko chini ya ile *"sheria ya Kristo"* (**1 Kor 9:21; Gal 6:2**).[9] Mfano mmojawapo wa hili ni kutokutumia pesa zetu vibaya kwa ajili ya sisi wenyewe na anasa zetu bali badala yake *"kuwakumbuka maskini"* (**Gal 2:10**). Katika **Wagalatia 5-6** anajadili kwa ufasaha yale maadili ambayo tunapaswa kuyafuata kama bibi arusi wa Kristo.

Kuwa ndani ya Kristo Yesu ina maanisha kwamba sisi sasa tuna *moyo wake* (**Ezek 36:26**), *nia yake* (**1 Kor 2:16**), *Roho wake* (**Ezek 36:27; Yohana 14:16-20; 2 Kor 3:3**), na *sheria yake* imeandikwa katika mioyo yetu (**Yer 31:33; Rum 8:2; 1 Kor 9:21; Gal 6:2**). Tunapokuwa tunatii na kumfuata Bwana mwenendo wetu na yale tunayoyapa kipaumbele hubadilika. Kwa mantiki hii, kwa hiyo, ndani ya Kristo Yesu *tunaweza kufanya* chochote tutakacho—kwa namna Bwana anavyofanya kazi ndani yetu kutubadilisha kuwa katika sura ya Kristo (**Rum 8:29**), kwa kawaida tutaanza kufikiri, kusema na kufanya kama Kristo mwenyewe na hatutakuwa tukiendelea tena kuyafanya matakwa ya mwili (ona **Rum 8:1-14; Gal 5:17**), kwa sababu tunapokuwa ndani ya Kristo Yesu, *"ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema"* (**Filp 2:13**). Kwa naneno mengine, tunaanza sasa kufikiri, kusema, na kutenda kwa namna ya ile asili yetu halisi tuliyonayo—kwa namna Mungu alivyotuumba tuwe. Kwa upande mwingine, Wakristo wanapofanya visivyo hii *siyo* ishara ya uhuru wao katika Kristo Yesu bali ni ishara ya kwamba *wanakosa kumtii* Kristo.

- **mst. 6-10:** ***[6] Lakini wale wenye sifa ya kuwa wana cheo; (walivyokuwa vyovyote ni mamoja kwangu; Mungu hapokei uso wa mwanadamu); nasema, hao wenye sifa hawakuniongezea kitu; [7] bali, kinyume cha hayo, walipoona ya kuwa nimekabidhiwa injili ya wasiotahiriwa, kama vile Petro ya waliotahiriwa; (maana yeye aliyemwezesha Petro kuwa mtume wa waliotahiriwa ndiye aliyeniwezesha mimi kwenda kwa Mataifa); [9] tena walipokwisha kuijua ile neema niliyopewa ; Yakobo, na Kefa na Yohana, wenye sifa kuwa ni nguzo, walinipa mimi na Barnaba mkono wa kuume wa shirika; ili sisi tuende kwa Mataifa, na wao waende kwa watu wa tohara; [10] ila neno moja tu walitutakia, tuwakumbuke maskini; nami neno lilo hilo nalikuwa na bidii kulifanya.***

Katika **mst. 2** Paulo alisema alikwennda kwa Yakobo, Petro, na Yohana na *"nikawaeleze injili ile niihubiriyo katika Mataifa . . . isiwe labda napiga mbio bure au nalipiga mbio bure."* Ni wazi kabisa alitaka kujua ni kwa mtazamo gani wale viongozi wakuu wa kanisa wangeitambua ile injili ya neema aliyokuwa akiihubiri, hasa hasa kwa sababu iligeuza mtazamo wa kijadi wa Wayahudi na kujitenga. Jibu linapatikana katika **mst. 6-9**: Paulo alikubaliwa; Tito asiyetahiriwa alikubaliwa; na kukawa na jaribio la kutaka kuiboresha injili aliyohuibiri Paulo. Hakika, Petro, Yakobo, na Yohana wote walitambua kwamba Paulo alikuwa amepokea neema ile ile na alikuwa akiihubiri injili ile ile ambayo waliipokea na kuihubiri. Ingawaje wale ambao Paulo aliwalenga walikuwa Mataifa na walengwa wa Petro walikuwa Wayahudi, Petro hakuwa akihubiri kwamba baada ya kumpokea Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wao Wayahudi walitakiwa kujiweka chini ya sheria ya Kiyahudi. Zaidi ya hayo, kwa kuwapa Paulo na Barnaba "mkono wa kuume wa shirika," wale viongozi wa Yerusalemu walikuwa wamekubali kwamba utume wa Paulo ulikuwa katika daraja moja la mamlaka kama ule wa kwao. Ijulikane kwamba **mst. 6** ni matokeo ya **mst. 3**: ni kama lile kovu la nje la tohara katika mwili, silo linaloamua ile mipaka ya watu wa Mungu au kumpa mtu fulani "hadhi kubwa" mbele za Mungu, kiasi kwamba ile hadhi ya hali ya ndani isiyo ya mwili iwe haina maana mbele za Mungu. Mungu hana upendeleo kwa watu

[9] Yaliyo bayana kuhusu "sheria ya Kristo" yatajadiliwa kwa kirefu chini katika mjadala wa **Gal 6:1-5** ambapo kifungu cha maneno "sheria ya Kristo" kinatumika hasa.

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

mbalimbali tofauti (**Kumb 10:17; Matendo 10:34; Rum 2:11**). Badala yake, *"Hapana Myahudi wala Myunani. Hapana mtumwa wala huru. Hapana mtu mume wala mtu mke. Maana ninyi nyote mmekuwa mmoja katika Kristo"* (**Gal 3:28**; ona pia **Kol 3:11**).

Huu mkutano wa binafsi ulikuwa na maana kubwa sana kwa kanisa. Uliweka ukweli kwamba kuna injili moja tu, na kweli ya injili haibadiliki. Kunaweza kukawa na mitindo tofauti na mikazo tofauti katika kuwasilisha injili kwa aina tofauti za wapokeaji, na makubaliano fulani yanaweza kufanywa na watu kuhusiana na maswala sera (mfano, Paulo kumtahiri Timotheo katika **Matendo 16:3** na makubaliano yake na wale "ndugu walio dhaifu" katika **Rum 14:1-15:1** na **1 Kor 8:1-13**). Lakini kamwe haitawezekana kufanya mjadala kuhusiana na maswala ya kanuni na maswala ya kweli ya injili yenyewe.

Muktadha wa tamko katika **mst. 10** ku "kumbuka maskini" ni kwamba Paulo alikuwa akiwaendea Mataifa wakati ambapo Petro, Yakobo, na Yohana kimsingi walikuwa wakihudumu kwa Wayahudi. Mataifa ndio waliokuwa na sehemu kubwa ya pesa. Kumbuka matoleo yaliyochukuliwa kule Antiokia kwa ajili ya kuwasaidia waamini maskini wa Yudea (ona **Matendo 11:29-30**). Yakobo, Petro, na Yohana kimsingi walikuwa wakisema, "Unapokuwa katika safari zako huko katika Dola ya Rumi na kushughulika na Mataifa walio tajiri wenye nguvu, usiwasahau maskini wa Yudea."

AK na AJ kwa kurudia rudia huweka mkazo umuhimu wa kuwajali maskini (mfano, **Kut 22:22; 23:6, 11; Kumb 10:18; 14:28-29; 15:9; Zab 12:5; 74:21; 140:12; Mith 14:21, 31; 22:9; 28:27; 31:9; Isa 3:14-15; 58:6-7; 61:1; Yer 22:3; Ezek 16:49; Amosi 2:6-7; Zech 7:10; Math 19:21; Luka 4:18; 12:33; 14:13; 18:22; Matendo 10:4; Rum 12:20; Gal 2:10; 1 Tim 5:3; Yak 1:27; 2:2-6; 1 Yohana 3:17-18**). Kuwajali maskini na wahitaji ni moja ya mambo muhimu ya injili kijamii. Katika *Commentary on Galatians,* Martin Luther anajadili ule umuhimu wa kuwajali maskini: "Baada ya kuhubiri injili, ofisi na jukumu la mchungaji wa kweli na aliye mwaminifu, ni kuwa makini na maskini. . . . Kwa swala la dunia na shetani kulitesa kanisa, na kusababisha umaskini kwa watu wengi. . . . Kwa upande mwingine, dini ya uongo na kufuru inastawi na kuzidi katika utajiri na mafanikio. Kwa hiyo mchungaji wa kweli na aliye mwaminifu ni lazima awajali maskini: na hata Paulo anakiri kwamba alikuwa na kujali huku." (Luther 1979: 55)

- **2:11-21—**Kweli ya injili iko juu ya umuhimu wa watu binafsi na urithi wake mtu:

    - **2:11-14—**Paulo anauweka hadharani unafiki wake Petro kuhusiana na jinsi alivyowatandea waamini wa Mataifa.

    [11] Lakini Kefa alipokuja Antiokia, nalishindana naye uso kwa uso, kwa sababu alistahili hukumu. [12] Kwa maana kabla hawajaja watu kadha wa kadha waliotoka kwa Yakobo, alikuwa akila pamoja na watu wa mataifa; lakini walipokuja wao, akarudi nyuma akajitenga, huku akiwaogopa waliotahiriwa. [13] Na hao Wayahudi wengine wakajigeuza pamoja naye, hata na Barnaba pia akachukuliwa na unafiki wao. [14] Walakini, nilipoona ya kuwa njia yao haiendi sawasawa na ile kweli ya Injili, nalimwambia Kefa mbele ya wote, Ikiwa wewe uliye Myahudi wafuata desturi za Mataifa, wala si za Wayahudi, kwa nini unawashurutisha Mataifa kufuata desturi za Wayahudi?"

Mistari hii inatuonyesha kwamba swala la kanisa ni zaidi ya kuongeza mahitaji ya imani katika Kristo (kama vile kutahiriwa au kushika sheria ya Musa). Mistari hii inatuonyesha kwamba injili huathiri kila eneo la maisha yetu, ikiwa ni pamoja na hata yule tunayekula naye. Matukio ya **mst. 11-14** yalitokea baada ya mateso ya kanisa yaliyozuka Yerusalemu na kwingineko yatokanayo na mamlaka za Wayahudi (ona **Matendo 4:1-21; 5:17-40; 6:8-8:4; 9:1-2; 11:19; 12:1-5; 13:44-45; 14:1-2**). Kwa ufahamu huo, inawezekana kwamba nia ya Yakobo, watu aliowatuma, na Petro ilikuwa nia njema, m.y., huenda waliacha kula na Mataifa kwa kujaribu kuwaepusha Wakristo wa Kiyahudi kutokana na upinzani na mateso kutoka kwa Wayahudi wasiookoka ambao walikuwa na fikra kwamba Wayahudi na Mataifa walipaswa kuwa wametengana milele. Kwa kufanya hayo, Wakristo wa Kiyahudi wangeweza kusema kwa Wayahudi wasioamini na mamlaka za Kiyahudi, "Mnaona, bado tunaheshimu jadi zetu za Kiyahudi ijapokuwa tunamwamini Yesu kama Masihi wetu."

Hata hivyo, Paulo aliona kwamba, lisha ya hiyo nia yao, matendo na matokeo ya kile Petro na wengine walichokifanya kiliingia na kupenye katika moyo wa injili yenyewe. Katika **Matendo 10** Petro alionyeshwa ya kwamba Mungu hana upendeleo kati ya Wayahudi na Mataifa. Aliweza hata kushuhudia kuhusu hili katika **Matendo 11** kwa Wayahudi waliokuwa wamempinga alipokuwa amekula na Mataifa wasiotahiriwa. Wakati Petro alipokutana na Paulo Yerusalemu, alikubaliana na fundisho la Paulo (**Gal 2:1-10**). Sasa, hata hivyo, Petro anaikana injili ile ile aliyoihubiri kwa namna alivyokuwa akiishi. Makusudio ya Petro ya nje, hayakuenda

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

sambamba na yale ya ndani, imani za nafsi. Kwa hiyo, Paulo alimwita "mnafiki" wazi wazi. Kwa kuwa swala hili halikuwa la faragha kati ya Petro na baadhi ya watu Mataifa bali kanisa lote liliathirika na asili ya injili yenyewe ilikuwa katika tatizo, Paulo hakumwendea Petro faraghani (kama inavyoonyesha **Math 18:15-16**) bali wazi wazi alimkabili *hadharani* (ona **Efe 5:11; 1 Tim 5:20**).

Petro alifanya kwa namna ya kujitenga kipekee, ya msimamo wa kati ambao ulikuwa kinyume na injili. Ndio maana Paulo hakumkabili Petro kwa misingi ya kwamba Petro alikuwa akitenda kwa sababu za kikabila, au ubaguzi wa rangi, au chuki, au kwa namna ya kudhuru, ingawaje alitenda katika njia hizo zote. Badala yake, mashambulizi ya Paulo yalihusu kiini hasa cha jambo, yaani, ya kuwa Petro hakuwa "*sawasawa na ile kweli ya Injili"* (**mst. 14**). Tafsri ya Biblia iitwayo NENO hutafsiri hii hivi *"sawasawa na kweli ya injili."* Petro aliikana injili kwa kuwatenga Mataifa kutoka katika ushiriki mkamilifu na usawa katika maisha ya kanisa. Na pia aliwanyima Mataifa ile hali ya kuwakubali kabisa *katika maisha yake ya binafsi* (m.y., kuhusu nani alikula naye) kwa sababu tu ya ule ukweli kwamba walikuwa Mataifa. Matokeo yake, ingawaje alijua anachopaswa kufanya, Petro aliifanya injili kuwa ni kwa ajili ya "Wayahudi tu." Jambo hili ni kinyume kabisa na historia yote ya mabadiliko ya wokovu na kusudio lake ni kuliondoa Agano Jipya na kuliweka tena Agano la Kale. Rich Lusk anasema, "Kwa sababu zile sheria za Agano la Kale zilikuwa sheria za kifungo na kujitenga badala ya kuwa zenye kumfanya mtu kupata nafasi na ukaribu, sheria za ahadi badala ya kutimilika kwa hizo ahadi, kwa kuwaweka waliookoka wa Mataifa chini ya sheria hizi ingekuwa ni kwenda hatua kubwa nyuma, ni kama tu kwa Wayahudi kuwa chini yake ingekuwa ni kubaki katika kizazi cha kale. . . . Tofauti muhimu [kati ya Paulo na wale Wayahudishaji] ni kuwa Paulo alitambua kuhusu kufa, kufufuka na kuja tena kwa Kristo dhidi ya kujitoa kwa Wayahudishaji' katika kuifuata Torati. Paulo angeweza kusema, na wapinzani wake wa Kiyahudi wasingesema, ya kuwa kizazi cha nyakati za mwisho zilizoahidiwa kimekwisha fika katika historia, na kufungua malango ya baraka za agano, si tu kwa wana wa Ibrahimu wa kijenetiki, lakini hatimaye kwa wana wote wa kijenetiki wa Adamu. Tatizo la msingi la Wagalatia lilikuwa ni utaifa wa Kiyahudi au utofauti wa wao, ulio na mizizi katika uelewa usio sahihi wa ratiba ya historia ya ukombozi wa Mungu. Israeli aliigeuza Torati, ambayo ingekuwa ndiyo njia ya kufikia lengo la kuja kwa Kristo (cf. Rum. 10:4), na kuifanya yenyewe kuwa ndiyo lengo lenyewe, na hivyo kuifanya kuwa aina ya ibada ya sanamu (Gal. 4:8-9; cf. Rum. 2:22)." (Lusk 2003: n.p.)

Kifungu hiki, na swala hili ni muhimu sana kwa kanisa hivi leo. Kwetu sisi swala linaweza lisiwe kwamba ni nani tunaekula naye. Swala la aina hii linaweza kutokea wakati wowote kanisa au Mkristo mmoja apingapo uanachama wa mtu mwingine, nafasi ya uongozi, ushirika, au usawa kamili kwa sababu ya kabila, mbari, matatizo ya kijamii na kiuchumi, au sababu nyinginezo kama hizi. Hili lilikuwa tazizo kubwa si tu kule Galatia lakini pia katika kanisa la kwanza kule Yerusalemu (ona **Matendo 6:1; Yak 2:1-13**); linaendelea kuwa tatizo kubwa kwa kanisa duniani kote leo. Tatizo hili huonekana pia katika hali ile ya kukosa ushirikiano ambayo baadhi ya madhehebu wanayo dhidi ya madhehebu mengine. Bila shaka, sisi sote tunafikiri kwamba theolojia yetu iko sahihi na ile ya wale wasiokubaliana nasi si sahihi. Hata kama tuko sahihi katika theolojia yetu, hata hivyo, twaweza kuwa sahihi kwa misingi ile ile ambayo Petro alikuwa sahihi: imani yake ya ndani kuhusiana na umoja wa Wayahudi na Mataifa ndani ya Kristo ilikuwa sahihi, lakini kwa kuwa hakuidhihirisha ile imani yake ya ndani katika matendo chanya yaliyowazi kuhakikisha kwamba Mataifa walitendewa kwa usawa, Petro alikuwa mnafiki *"ambaye hakuwa mnyofu kuhusiana na kweli ya injili."* Kwa kufanya hivyo, aligeuza urithi wake wa Kiyahudi na utamaduni kuwa sanamu ya kuabudu. Jambo hili ni la kutazama kwa umakini mkubwa sana. Injili ni *kweli,* na kweli ni lazima iathiri namna tunavyoishi pamoja na namna tunavyoamini. Ikiwa makanisa (na watu binafsi) hawajihoji kwa makusudi na kuamua kubadili matendo yao ili wawe sambamba na nia ya injili, maamuzi ya Mungu siku ile ya hukumu yaweza kuwa kwamba hatukuwa waamini waaminifu au kanisa bali kwa hakika tulikuwa wanafiki na waabudu sanamu.

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

- **2:15-21—**Hata Wayahudi huhesabiwa haki kwa imani, si kwa sheria.

> ***15 "Sisi tulio Wayahudi kwa asili, wala si wakosaji wa Mataifa, 16 hali tukijua ya kuwa mwanadamu hahesabiwi haki kwa matendo ya sheria, bali kwa imani ya Kristo Yesu; Sisi tulimwamini Kristo Yesu ili tuhesabiwe haki kwa imani ya Kristo, wala si kwa matendo ya sheria; maana kwa matendo ya sheria hakuna mwenye mwili atakayehesabiwa haki. 17 Lakini ikiwa sisi wenyewe, kwa kutafuta kuhesabiwa haki katika Kristo, tulionekana kuwa wenye dhambi, je! Kristo amekuwa mtumishi wa dhambi? Hasha! 18 Maana nikiyajenga tena yale niliyoyabomoa, naonyesha ya kuwa mimi mwenyewe ni mkosaji. 19 Maana mimi kwa njia ya sheria naliifia sheria ili nimwishie Mungu. 20 Nimesulubiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu. 21 Siibatili neema ya Mungu; maana, ikiwa haki hupatikana kwa njia ya sheria, basi Kristo alikufa bure."***

Mistari hii inatoa sababu ni kwa nini Paulo alikuwa mkali kuhusiana na lile swala la kumkabili Petro. Mistari hii inatuhabarisha angalau mambo matatu. Kwanza, kurudi kwenye sheria ya Musa baada ya kumpokea Kristo kama Bwana na mwokozi humaanisha kusema kwamba Kristo ametuleta katika *dhambi* kwa sababu *tumeacha* kuitii Sheria ya Musa tulipokuja kwa Kristo. Hata hivyo, hilo haliwezekani kwa sababu Kristo hana dhambi: yeye mwenyewe hakufanya dhambi na wala hawezi kumfanya mwingine atende dhambi (ona **2 Kor 5:21; 1 Pet 2:21-24; Ebr 4:15**). Yeye aliitimiza Sheria kama ilivyopasa tu (ona **Math 5:17-20**) ili aweze kutukomboa kutoka katika laana ya Sheria (**Gal 3:13; 4:4-5**). Hivyo, ye yote anayerudi katika Sheria baada ya kuja kwa Kristo inamaanisha kwamba yeye haelewi kabisa kile ambacho Kristo amekitenda pale msalabani na haielewi injili.

Pili, kwa kuwa Kristo alichukuwa dhambi zangu msalabani, ina maana *"Nimesulibiwa pamoja na Kristo"* (**Gal 2:20**). Kwa hiyo, kupitia Kristo *"naliifia sheria"* (**Gal 2:19**). Matokeo yake, Sheria haina madai kwa wamwaminio Kristo (ona **Rum 7:1-6**). Hata hivyo, **Gal 2:18** inaonyesha kwamba *"nikiyajenga tena yale niliyoyabomoa, naonyesha ya kuwa mimi mwenyewe ni mkosaji."* Kwa maneno mengine, matokeo yaliyo kinyume ya kurudi kwenye Sheria baada ya kumpoke Kristo ni kwamba ninakuwa mkosaji au mwenye dhambi.

Tatu, kile ambasho Paulo anakisema hapa na katika Wagalatia kwa ujumla huonyesha wazi ile tofauti iliyopo kati ya Ukristo na dini nyinginezo duniani. Kwa kufanana katika Biblia "Sheria" na "matendo ya sheria" humaanisha ile sheria ambayo Israeli walipewa kupitia kwa Musa (m.y., sheria ya Musa). Hata hivyo, zile kanuni ambazo Paulo anazijadili hutumika katika dini zote. Sababu ni kwamba kila dini iwayo yote duniani huwataka watu wajikomboe wenyewe kwa kufuata sheria, taratibu, na kanuni mbali mbali zilizowekwa na wanadamu. Kwa maneno mengine, ingawaje hizo sheria ambazo wanadamu wanatakiwa kuzifuata si Sheria ya Musa, bado watatakiwa kutimiza "matendo ya sheria," m.y., watategemea juhudi zao wenyewe ili kupata wokovu (wakijitahidi kutii amri na sheria zote, wakifanya matendo mema kiasi cha kutosha, kutoa dhabihu za kutosha wakijinyima vitu vya kutosha). Hivyo, dini nyingine zote katika neno ispokuwa injili ya Kikristo ni dini za "wokovu wa binafsi" zenye misingi katika sheria na matendo, sio wokovu kwa neema peke yake kwa njia ya imani peke yake katika kile ambacho Kristo alikifanya kwa ajili yetu. Programu zote za aina hii za "wokovu wa binafsi" lazima zishindwe kwa sababu angalau tano:

- Kwanza, kwa sababu Mungu mwenyewe ni mtakatifu na mkamilifu, hicho ndicho kipimo ambacho kwacho Mungu anatupimia sisi (**Math 5:48**). Hata hivyo, "mtu anapotenda dhambi, haiwezekani kamwe kuwa mkamilifu" (Sproul 2002: 94; ona pia ibid.: 53).
- Pili, hata yale matendo yetu mema yana madoa ya dhambi na yanatokana na makusudi na nia mchanganyiko. Hakika, ikiwa tunafanya matendo mema ili kukwepa hukumu ya Mungu ya jehanum, hilo peke yake huyafanya matendo yetu mema kuwa *si* "mema." Sababu ni kwamba ikiwa lengo letu ni kukwepa jehanum kwa kufanya "matendo mema," basi hayo matendo kwa tafsiri, ni ya kibinafsi, na kiini chake ni ubinafsi, mfano, tunapowasaidia maskini, kimsingi tunajisaidia *wenyewe* kukwepa jehanum. Hivyo, hakuna kiwango chochote cha matendo, kwa kuwa hayo yenyewe yana madoa ya dhambi, yanaweza kulipia adhabu ya dhambi zetu.
- Tatu, hakuna aliyefanya matendo mema "vya kutosha" au kutoa dhabihu za kutosha kumridhisha Mungu. Timothy Keller anasema, "Viwango vya kiroho na uadilifu vya dini zote viko juu sana, na Mafarisayo [m.y., wote wanaojaribu kujiokoa wenyewe kwa kufanya matendo mema na kutii sheria za dini] wanajua wazi ndani yao ya kuwa hawaishi kwa kuvifuata viwango hivyo. Hawaombi vya kutosha kama wanavyopaswa. Hawawapendi jirani zao na kuwatumikia vya kutosha kama wanavyopaswa. Mawazo yao ya ndani si masafi kama yanavopaswa kuwa." (Keller 2008: 178)

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

- Nne, hakuna kiwango chochote cha matendo mema kinachoweza kuibadili asili ya dhambi na tabia za dhambi za moyo. Sheria, amri, na kanuni huwaambia watu tu kile wanachopaswa kufanya, lakini haziibadili mioyo ya watu au kuwapa watu uwezo au shauku ya kufanya kile wanachopaswa kufanya. Kufanya matendo mema hakuwabadili watu waovu, watendao dhambi kuwa wenye haki, wasio na dhambi katika mioyo yao; wanabaki kuwa watu wenye dhambi. Ikiwa Mungu atawaruhusu watu wenye dhambi kuingia mbinguni na katika nchi mpya ambamo watu wataishi milele (**Ufunuo 21-22**), mbingu na nchi mpya zitaendelea kuwa na uovu milele. Mungu hatoweza kuwepo pale kwa kuwa "dhambi haiwezi kumkaribia Mungu, na Mungu hawezi kuivumilia dhambi" (Stott 1986: 106). Kwa hakika, ikiwepo hulka ya mwanadamu ya uovu na mwelekeo wa dhambi, mbinguni kutageuka kuwa jehanum.
- Tano, mwisho wa yote dhambi inapingana na Mungu kwa sababu sheria ya Mungu inatoka kwake na taswira ya asili yake takatifu; kwa hiyo, kutenda dhambi kwa kuihalifu sheria yake ni kumkosea yeye binafsi. Kuwatenda wengine dhambi ni kumtenda Mungu kwa sababu watu wameumbwa kwa mfano wa Mungu (**Mwz 1:26-27; 9:6; Yak 3:9-10**). Dhambi huleta kutokumheshimu na kuinajisi sura ya Mungu na kwa njia hiyo kudhihirisha kile ambacho mtenda dhambi hufikiri hasa kuhusu Mungu mwenyewe. Hali hii ni sawa na ile ya mtu anapofanya uhalifu dhidi ya mtu mwingine; yule mhalifu amemkosea si yule mtu tu bali kimsingi anavunja sheria ya nchi. Kwa hiyo, ni serikali ndiyo inayomhukumu mvunja sheria, na sio yule mtu aliyetendewa uhalifu. Vivyo hivyo na dhambi ni kama kutupa jiwe ndani ya dibwi la maji; lile jiwe kutengeneza maduara kutoka pale lilipoangukia hadi kwenye maji yote yanayozunguka. Kwa namna iyo hiyo dhambi humharibu na kumbadilisha mwenye dhambi moja kwa moja, watu wengine, na dunia kwa namna ambayo huenda isijulikane kwa mtenda dhambi. Kwa hiyo, "matendo mema" au mambo mengine tunayojaribu kufanya kulipia kwa ajili ya dhambi yetu ili kuupata wokovu, kwa asili yake hasa, ni ya *kitambo tu na yasiyo makamilifu*. Hayambadilishi mtenda dhambi kuwa mtu mtakatifu na hayawezi kuondoa matokeo ya ile dhambi ambayo yameiharibu nafsi ya mtenda dhambi *moja kwa moja* na kuwaathiri watu wengine na dunia.

  Mungu hana ukomo: ana utakatifu usio na ukomo; ana upendo usio na ukomo; ana wema usio na ukomo. Kwa hiyo, wajibu wetu kwake hauna ukomo (**Kumb 6:5; Math 22:37; Marko 12:30; Luka 10:27**), na dhambi yetu dhidi yake hutufikisha katika uovu usio na ukomo. Kwa kifupi, hakuna kitu kijulikanacho kama kosa lenye ukomo dhidi ya Mungu asiye na ukomo. Kwa hiyo, hakuna matendo yetu yo yote ya kitambo, yenye ukomo, na yasiyo na ukamilifu yanaweza kulipa kwa ajili ya dhambi zetu zisizo na ukomo. Kama John Stott anavyihitimisha, "Kama tutaweza kusamehewa kwa namna ye yote ile, ni lazima tulipie kile tunachodaiwa [ona Anslem 1903: I:11]. Bado hatuna uwezo wa kufanya hili, iwe kwa ajili, yetu au kwa ajili ya watu wengine. Utii wetu wa sasa na matendo mema haviwezi kufanya utoshelevu kwa ajili ya dhambi zetu, kwa kuwa haya yanatakiwa kutoka kwetu hata hivyo. Kwa hiyo hatuwezi kujiokoa wenyewe." (Stott 1986: 119)

Kwa upande mwingine, **Rum 5:6** anasema, *"Kristo alikufa kwa ajili ya waovu."* Ndiyo maana **mst. 17** unasema, *"Kwa kutafuta kuhesabiwa haki katika Kristo, tulionekana kuwa wenye dhambi."* Swala ni kwamba kuwa mwenye haki na kuwa mwenye dhambi si swala la "ama/au." Badala yake, kwa mujibu wa Ukristo sisi tu wenye haki na watenda dhambi *kwa wakati huo huo*. Martin Luther alielewa kwamba kiini cha injili ni kwamba ndani ya Kristo, tuna *"simul justus et peccator,"* ambayo kwa Kilatini humaanisha "kwa wakati mmoja wasio na hatia [wenye haki kiroho] na watenda dhambi." R. C. Sproul huielezea hali hii: "Alikuwa akisema kutoka katika mtazamo mmoja, katika maana moja, hatuna hatia. Katika maana nyingine, katika mtazamo tofauti, tu watenda dhambi; na namna anavyoitafsiri hiyo ni rahisi. Ndani yetu na kwa sisi wenyewe, chini ya uchambuzi wa uchunguzi makini wa Mungu, bado sisi tuna dhambi; bado tu watenda dhambi. Lakini, kwa kushutumiwa na kwa imani katika Yesu Kristo, ambaye utakatifu wake sasa umehamishwa katika akaunti yetu, hivyo na sisi tunatambulika hatuna hatia au wenye haki. Hiki ndicho kiini hasa cha injili." (Sproul 2019: n.p.) Sproul anatoa ufafanuzi: "Ikiwa ningetakiwa kuutegemea utakatifu wangu ili niingie mbinguni, ningekata tamaa kabisa na kupoteza tumaini kabisa la uwezekano wa kukombolewa. Lakini wakati tunapoona ile haki ambayo ni yetu kwa imani ndiyo haki iliyo kamilifu ya Kristo, hapo tunaona jinsi gani habari njema za injili ni za utukufu. Habari njema ni hizi kwa lugha rahisi, naweza kupatanishwa na Mungu, naweza kuhesabiwa haki na Mungu si kwa mujibu wa yale niliyotenda, lakini kwa mujibu wa yale yaliyoyafanywa na Kristo kwa ajili yangu.

Lakini katika kiini cha injili kuna shutuma mbili. Dhambi yangu imewekwa juu ya Yesu. Haki yake imewekwa juu yangu. Na katika huu muamala wa pande mbili tunaona kwamba Mungu, ambaye hafanyi majadiliano na dhambi, ambaye haufanyii mwafaka uadilifu wake kwa wokovu wetu, lakini badala yake huadhibu dhambi kikamilifu na hasa baada ya kumshutumu Yesu, anabaki na haki yake, na kwa hiyo ana haki na mwenye kuhesabia haki. . . . Kwa hiyo dhambi zangu zinaenda kwa Yesu, Haki yake inakuja kwangu mbele za macho ya Mungu." (Ibid.)

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

Jambo hili lina maana kubwa sana kwa Wakristo. Ndio maana Paulo alimkabili Petro awe "*mnyofu kuhusiana na kweli ya injili.*" Kuna maana kadhaa muhimu za jambo hili:

Kwanza, ni injili tu ambayo inatilia maanani swala la Sheria. Washika sheria *hufikiri* kwamba wao wako makini kuhusiana na sheria kwa wao wenyewe kujiweka ama chini ya ile Sheria ya Musa au chini ya sheria na kanuni ambazo zimewekwa na wanadamu. Hata hivyo, kiukweli *hawaitilii* maanani sheria kabisa. Sababu ni kwamba wao huitii sheria kwa sehemu tu na, hata hivyo, si kwa kuendelea wakati wote.[10] Kwa mfano, Yesu alisema kwamba sheria yote imefupishwa katika amri mbili: "MPENDE BWANA MUNGU WAKO KWA MOYO WAKO WOTE, NA KWA ROHO YAKO YOTE NA KWA AKILI ZAKO ZOTE" na "MPENDE JIRANI YAKO KAMA NAFSI YAKO" (**Math 22:37-39**; ona pia **Marko 12:29-31; Luka 10:25-28; Gal 5:14**). Ukweli ni kwamba hakuna anayetii amri hizi au mojawapo ya hizi amri wakati wote au hata katika sehemu kubwa ya muda wake. Je ni kweli sisi tunampenda Mungu kwa moyo wetu *wote,* nafsi yetu *yote,* akili zetu *zote,* wakati wote? Na kumpenda jirani yetu kama tunavyojipenda wenyewe ingemaanisha kwamba tungetumia muda ule ule, fikra, juhudi, na pesa katika kutafuta mafanikio ya wengine kama vile tufanyavyo tunapotafuta mafanikio yetu wenyewe. Hakuna mtu ye yote anayefanya hivyo.

Hakuna hata mmoja, hii ina maana, ispokuwa Yesu. Yeye peke yake alimpenda Mungu Baba kwa moyo wake wote, nafsi yake yote, na akili zake zote, na yeye peke yake alimpenda jirani yake kama alivyojipenda mwenyewe. Kufanya hivyo kulimgharimu maisha yake msalabani. Lakini kwa sababu yeye peke yake alizitii amri zote, yeye peke yake alistahili kuchukuwa dhambi zetu juu yake na kuweka haki yake juu yetu. Kwa sababu haki ya Yesu imewekwa juu yangu, Mungu ananiona mimi kuwa ni mwenye haki! Hii humaanisha sihitajiki—au—"kufanya matendo" ili kupata haki, kwa kuwa Yesu amefanya kazi yote kwa ajili yangu. Kwa misingi ya kitheolojia, hii humaanisha kwamba ikiwa nitajiweka mwenyewe chini ya Sheria ya Musa au chini ya sheria zozote zile ile niweze kuwa na haki mbele za Mungu au kuupata upendeleo wa Mungu, hapo nitakuwa *ninakataa* kile ambacho Yesu alikifanya kwa ajili yangu. Ingawaje tunatakiwa *"tuutimize wokovu [wetu] wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka"* (**Filp 2:12**), tunafanya hivyo kwa misingi mipya kabisa: tunamfuata na kumtii Mungu, si *kutendea kazi* upendelea wake lakini kwa shukrani na furaha itokanayo na kule *kuupokea* upendeleo wake tayari! Na tunafuata uongozi wa Mungu na kumtii hali tukikumbuka kwamba, sasa, *"ndiye Mungu atendaye kazi ndani [yetu] kutaka kwetu na kutenda kwetu kwa kulitimiza kusudi lake jema"* (**Filp 2:13**). Sisi hatuko peke yetu tena. Hilo ndilo linaloufanya Ukristo kuwa tofauti na dini nyinginezo zote duniani.

Pili, tukiuchukuwa ukweli huu ndani yetu zaidi, ni lazima utaathiri uhusiano wetu na watu wengine. Ikiwa tutaelewa hasa kwamba sisi tu watenda dhambi, basi hatuwezi kumdharau mwingine awaye yote tena. Hatuwezi kujiona sisi wenyewe kuwa tu "bora" au "wenye haki" zaidi au "watakatifu" zaidi ya wengine—kwa sababu tunatambua kuwa haki yetu si ya kwetu wenyewe bali ni ya Kristo wakati ambapo dhambi yetu ni ya kwetu. Hivyo, injili haiwagawanyi watu bali inawaunganisha. Kama N. T. Wright anavyotoa wazo, "Hili dokezo la kuhesabiwa haki kwa imani, katika muktadha huu, ni . . . kukazia kwamba wale wote ambao wanaishiriki imani hii ya Kikristo ni washirika wa familia moja ya Mungu ndani ya Kristo *na hivyo wao ni wa meza hiyo hiyo*." (Wright 2000: 234) Hicho ndicho ambacho Petro hakukielewa katika **Gal 2:11-14**.

Injili ina matokeo mengine muhimu kwa ajili ya maisha yetu. Tunapotambua kwamba Kristo amechukuwa dhambi yetu juu yake na adhabu ile ambayo tungeistahili, hilo linatupa ujasiri kumjia Mungu *"kwa damu ya Yesu"* (**Ebr 10:19**). Pia inatupa ujasiri wa kuikabili dhambi, uovu, na unafiki ulioko duniani, kama vile Paulo yeye mwenyewe alivyofanya. Kwa namna iyo hiyo, mabaya yanapotupata, na tunapopata mateso, tunatambua kwamba, kama watenda dhambi, hatustahili chochote kilicho kizuri kamwe, hivyo hatumkasirikii Mungu; pia tunatambua kwamba, katika mateso, tunafuata nyayo za Yesu ambaye alikuwa *"mtu wa huzuni nyingi ajuaye sikitiko"* (**Isa 53:3**). Kwa upande mwingine, tunaweza pia kutambua kwamba, kwa sababu Yesu alichukuwa dhambi yetu, anayatumia meteso yetu na huzuni zetu ili kutupatia mema katika maisha yetu na, kupitia sisi, katika maisha ya wengine, kama vile Mungu alivyoleta mema mengi kwa wanadamu kwa kupitia mateso ya Yesu. Kwa kifupi, ni injili peke ya inayotoa picha ya kweli ya watu. Zaidi ya hayo, ni injili peke yake hutupa sisi ile nguvu inayotubadilisha tunayoihitaji ili tuwe kama Yesu, kwa sababu tumewekwa huru kutoka katika sheria ili tuishi kwa ajili ya Mungu (**mst. 19**) na hatuko peke yetu tena, lakini Kristo anaishi ndani yetu (**mst. 20**). Kwa hiyo, tunapomkaribia Kristo na kukumbuka sisi ni nani (wenye haki na watenda dhambi

[10] Si katika Wagalatia wala mahali pengine popote Paulo anawatambulisha wapinzani wake kama watu ambao ni watii kwa sheria. Ingawaje katika **Gal 3:10** anazungumza kwa habari ya wale ambao *"ni wa matendo wa Sheria,"* kile kifungu cha maneno "haikumaanisha kitu kama 'wale walikuwa ni watu ambao waliitimiza sheria'" (Silva 2007: 799). Kwa kweli, katika **Gal 6:13** anasema wao *"wenyewe waliotahiriwa hawaishiki Sheria."* Moisés Silva anahitimisha, "Ni wazi kwamba Paulo, kama angalibanwa, angekubali kwamba wapinzani wake Wayahudi walitii amri nyingi bayana, lakini hiyo ni habari nyingine kutoka katika swali ya kuwa kama wangeweza kwa usahihi *kuwekwa katika fungu* la watu ambao wanaitii sheria" (Ibid.).

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

kwa wakati mmoja) hatupaswi kuendelea kujivuna (tunapofikiri hatuna tatizo) au katika hali ya kukata tamaa na kukasirika au kusongwa na mfadhaiko (mambo yasipotuendea vema au mabaya yanapotupata na tunateseka).

MASWALI YA KUJADILI

1. Maisha ya Paulo yalionyeshaje uhalisia wa kuokoka kwake?

2. Je, maisha yetu yanapaswa kuonyesha uhalisia wa kuokoka kwetu? Kama ndivyo, ni kwa nini iwe hivyo na ni kwa njia gani maisha yetu yanapaswa kuonyesha uhalisia wa wakovu wetu?

3. Je Mungu ana nafasi gani katika wokovu wa mtu?

4. "Ushikaji mno wa sheria" ni nini"?

5. Je makanisa yetu ya siku za leo yana sheria za kushika, jadi zinazofanana na zile ambazo wale Wayahudishaji waliowataka Wagalatia kuzitimiza? Kama ndivyo, ni matendo gani ya kisheria ambayo makanisa yetu siku za leo hutaka yafanywe na tuikabili kwa namna gani hali hiyo ya ushikaji wa sheria?

6. Ni kwa nini tunaweza kusema kwamba Wakristo wana uhuru ndani ya Kristo Yesu na wanaweza kufanya watakacho, na bado haimaanisha kwamba wana kibali cha kufanya dhambi?

7. Ni kwa nini kuwajali maskini ni muhimu sana? Ni mambo gani bayana tunapaswa kufanya mtu mmoja mmoja na kama kanisa kuwajali maskini?

8. Je, ni kwa njia zipi Wakristo wa siku za leo hawatendi "sawa sawa na kweli ya injili" (kama vile alivyofanya Petro alipoacha kula na Mataifa)? Ni kwa namna gani sisi watu binafsi na makanisa tunaweza kutatua shida hii?

9. Ukristo unatofautianaje na dini nyingine zote duniani?

10. Ni sababu zipi ambazo zinaonyesha kwamba haiwezekani kwa mtu ye yote kuweza kuupata wokovu kwa matendo yake kwa njia ya kuitii sheria au kufanya matendo mema?

11. Je, inamaanisha nini "kuwa mwenye haki na mwenye dhambi kwa wakati mmoja," na hii husababisha nini?

D. <u>Gal 3:1-4:31—Utofautishaji imani/sheria:</u> Hili ni la msingi na huturudisha nyuma tangu wakati wa Ibrahimu.

Sura hizi mbili ni miongoni mwa sura zilizo muhimu sana katika Biblia yote. Zina umuhimu mkubwa kwa sababu zinatupa muhtasari wa mpango wa Mungu wa wokovu. Kwa kufanya hivyo, sura hizi mbili hutuambia uhusiano uliopo kati ya agano la Ibrahimu na Sheria ya Musa, zinajadili makusudi ya Sheria, na zinajadili Israeli na kanisa kwa kuhusiana na Agano la Kale na Jipya.

- **<u>3:1-5—</u>**<u>Swali kuu: Je unakamilishwa kwa mwili (sheria), au kwa Roho (imani)?</u>

  [1]Enyi Wagalatia msio na akili, ni nani aliyewaloga, ninyi ambao Yesu Kristo aliwekwa mbele ya macho yenu ya kuwa amesulubiwa? [2]Nataka kujifunza neno hili moja kwenu. Je! Mlipokea Roho kwa matendo ya sheri, au kwa kusikia kunakotokana na imani? [3]Je! Mmekuwa wajinga namna hii? Baada ya kuanza katika Roho, mnataka kukamilishwa katika mwili? [4]Mmepatikana na mateso makubwa namna hii bure? Ikiwa ni bure kweli. [5]Basi, yeye awapaye Roho na kufanya miujiza kati yenu, je! Afanya hayo kwa matendo ya sheria, au kwa kusikia kutokanako na imani?

Katika mistari hii Paulo anafanya tena kile alichokifanya katika **sura ya 1** na **2**—anatofautisha Ukristo na kila dini nyingineyo yote duniani. Ndio maana **mst. 2** na **5** hutofautisha yale machaguo mawili ya pekee: Roho na imani dhidi ya *"matendo ya sheria."* Dini za wanadamu misingi yake ni "*matendo ya sheria,"* m.y., kujaribu kufuata amri fulani kadhaa. Katika **mst. 3** Paulo analinganisha *"matendo ya Sheria"* na *"mwili."* Kwa upande mwingine, Ukristo una misingi katika *"kusikia kwa imani,"* m.y., kuamini injili na kukitegemea kile alichokifanya Kristo kwa ajili yetu. Katika mistari hii mitano yote Paulo anawekea mkazo kwa Roho Mtakatifu.

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

Roho ndiye anayeufanya Ukristo uwe tofauti ukilinganishwa na dini nyinginezo. Roho ni Mungu (**Matendo 5:3-4; 2 Kor 3:17**). Ikiwa mtu hanaye Roho, mtu huyo si Mkristo (**Rum 8:1-17; 2 Kor 3:5-6**). Roho alimiminwa, kuanzia siku ya Pentekoste, baada ya Yesu kuwa ameitimiza sheria kupitia maisha yake makamilifu ya utii, kifo chake cha kujitoa dhabihu, kufufuka kwake, na kupaa kwake kurudi kwa Baba. Kwa maneno mengine, katika maisha yake, kifo, kufufuka, na kupaa, Kristo alifanya *kila kitu* kilichokuwa kinahitajika ili kutupatanisha sisi na Mungu. *Hakuna* ambacho kilibakia kwa ajili ya sisi kukifanya wenyewe. Kwa hiyo, Roho anaweza tu "kupokelewa" (**mst. 2**), si kwa kutenda kazi kwa matendo yetu yasiyokamilika. Roho *hupokelewa* wakati mtu anapomwamini Yesu. Kisha Roho *hukaa* ndani ya mwamini katika maisha yote ya mwamini. Hili humaanisha kwamba Sheria ya Musa na sheria walizojiwekea watu hazina uwezo kutusafisha au *"kutukamilisha"* (**mst. 3**), m.y., kubaki katika wokovu na kuishi maisha ya uaminifu, kama ilivyo kwa kuhesabiwa kwetu haki au *"kumpokea yule Roho"* (**mst. 2**), m.y., kuokoka kwetu hasa. Hili pia linaonekana katika **mst. 5** ambao unasema kwamba Mungu *"awapaye Roho na kufanya miujiza kati yenu."* "Awapaye" na "kutenda" yote yako katika wakati uliopo, wakati tendi. Hivyo, **mst. 5** unazungumza kuhusu kazi inayoendelea ya Roho katika maisha ya waamini. Kwa maneno mengine, tunampokea Roho na kuja kwa Kristo kwa imani na tunaendelea kudumu kwa uaminifu kupitia Roho kwa imani. Kwa kusema kwamba watu huja kwa Kristo kwa imani lakini baada ya hapo wanaendelea kudumu kwa matendo au wanaendelea kudumu kwa sheria ni kuikana ile injili yenyewe.

Watu wengine wanaweza kufikiri kwamba mkazo wa Paulo juu ya kuhesabiwa haki na kutakaswa kwa imani peke yake, nje ya kufanya matendo ya sheria, hutofautiana na kile asemacho Yakobo katika **Yak 2:24** ya kwamba *"mwanadamu huhesabiwa kuwa ana haki kwa matendo yake; si kwa imani peke yake."* Hata hivyo, Paulo na Yakobo hawatofautiani bali hukamilishana. Hili liko hivyo kwa sababu kadhaa:

- Paulo na Yakobo "wanazungumzia kuhusu mambo tofauti: Paulo kuhusiana na kutamkwa kwetu kuwa wenye haki, na Yakobo kuhusiana na ushahidi wa haki yetu. . . . Wote Paulo na Yakobo wanazungumzia haki ya mtenda dhambi mbele za Mungu, lakini fokasi ya Paulo iko katika upokeaji wa mwanzo wa hadhi hiyo na Yakobo kuhusu ile njia ambayo hiyo hadhi inathibitishwa mbele za Mungu katika hukumu." (Carson and Moo 2005: 633) "Tofauti iliyopo kati ya Paulo na Yakobo ipo katika mtiririko wa utendaji na badiliko: Paulo anapinga kule kufaa kwa matendo yoyote kabla ya kuokoka, bali Yakobo anasihi ule umuhimu wa matendo baadaya ya kuokoka" (Moo 1985: 102). Burdick analiweka hilo kwa namna hii: "Yakobo alipambana na imani iliyokuwa juujuu ambayo haikuwa na matokeo yanayoonekana katika maisha ya mtu anayekiri kuwa yeye ni mwamini. Paulo, kwa upande mwingine, alikuwa akipambana na ile hali ya ushikaji sana sheria—ile imani kwamba mtu anaweza kupata haki ya wokovu mbele za Mungu kwa matendo yake mema." (Burdick 1981: 185)
- Kwa sababu Yakobo na Paulo walikuwa wakifokasi katika maswala tofauti au walipambana na mawazo tofauti potofu kuhusiana na kweli, imani ya Kikristo, wanatumia wazo la "imani peke yake" (m.y., imani bila ya matendo) katika maana tofauti, ingawaje wote wanakubaliana juu ya ile imani ya kweli iokoayo ni ipi: Yakobo anaielezea "imani peke yake" kama ambayo si ile ya kweli, imani iokoayo; Paulo anatumia lile wazo la "imani peke yake" kama kuielezea imani iokoayo ya kweli: "'imani peke yake' ya Yakobo ni ile ambayo iko mbali na imani halisi ya Kikristo: 'imani peke yake' hii ni maneno matupu kuhusiana na matendo (mst. 15-16) au maarifa yaliyo kichwani tu bila ya maarifa ya moyoni (mst. 19). Hii siyo imani ya Kikristo. Na kuhusiana na hili Paulo hangekuwa na mabishano; yeye pia alikazia kwamba ni imani 'itendayo kazi kwa upendo' [**Gal 5:6**] ndiyo ambayo ina maana." (Moo 1989: 1157) "Ile aina ya imani ambayo Yakobo anasema kwamba 'imekufa' (hiyo ni kibali cha kiakili tu, 2:14-17) sio ile ambayo Paulo angeitambua kuwa ni imani halisi (yaani 'imani itendayo kazi kwa upendo', Gal. 5:6)" (Marshall, Travis, and Paul 2002: 255).
- "Namna ambavyo Paulo analichukulia swala la 'imani na matendo' huhusiana na swali ikiwa Wakristo wa Mataifa ni lazima wafanya 'matendo ya sheria' – hasa hasa kutahiriwa, sabato na sheria za chakula. Hoja ya Yakobo haiwahusu Mataifa wala hayo 'matendo ya sheria' katika mtazamo wake kabisa. . . . Kwa kweli wao hawako katika mabishano kati ya wao kwa wao bali na wapinzani tofauti – Paulo akipingana na wale ambao wanaolazimisha 'matendo ya sheria' kwa Mataifa, Yokobo akipingana na watu ambao wamekuwa walegevu katika maisha yao ya Kikristo" (Marshall, Travis, and Paul 2002: 255)." (Marshall, Travis, and Paul 2002: 255)

Carson na Moo wanatilia mkazo umuhimu wa kusikiliza mitazamo yote miwili wa Paulo na Yakobo: "Unapokuwa unakabiliwa na ushikaji wa sheria sana, ambao una nia ya kuweka misingi ya wokovu katika matendo ya watu, Paulo anahitaji kusikilizwa—kwa kuwa alikuwa na nguvu sana wakati wa Matengenezo. Lakini unapokabiliwa na falsafa ya unyenyekevu, yenye mwenendo ambao huondoa umuhimu wa matendo kwa Wakristo, Yakobo inabidi asikilizwe—kwa kuwa alikuwa na nguvu vile vile wakati wa kina Wesleys." (Carson

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

and Moo 2005: 633)

- **3:6-9—**Ni wale tu walio wa imani (wawe Wayahudi au Mataifa) ndio watoto wa kweli wa Ibrahimu.

> ***6 Kama vile Ibrahimu ALIVYOMWAMINI MUNGUAKAHESABIWA HAKI. 7 Fahamuni basi, ya kuwa wale walio wa imani, hao ndio wana wa Ibrahimu. 8 Na andiko, kwa vile lilivyoona tangu zamani, kwamba Mungu atawahesabia haki Mataifa kwa imani, lilimhubiri Ibrahimu habari njema zamani, kusema, "KATIKA WEWE MATAIFA YOTE WATABARIKIWA." 9 Basi hao walio wa imani hubarikiwa pamoja na Ibrahimu aliyekuwa mwenye imani.***

Katika **mst. 1-5** Paulo alishasema si tu umuhimu wa imani bali pia upekee wake (kinyume na "matendo ya sheria") ikiwa ni kwa ajili ya kuhesabiwa haki na kwa kutakaswa. Sasa, akianza na Ibrahimu, anaendelea kujadili uhusiano uliopo kati ya imani na sheria, akiweka msingi wa hoja yake katika mkondo mkubwa wa historia ya ukombozi. Huu ndio unakuwa mtazamo unaotawala katika sehemu yote iliyobaki ya **sura 3** hadi mwisho wa **sura 4**. Huu mtazamo wa ukombozi-kihistoria unahusisha uhusiano kati ya Agano la Ibrahimu na Sheria ya Musa, makusudi ya Sheria, na Israeli na kanisa ikihusianishwa na Agano la Kale na Jipya. Huu mtazamo wa ukombozi-kihistoria ni muhimu kwa sababu "kosa la Wagalatia lilikuwa, katika ngazi ya msingi, kihistoria-kitheolojia kimwenendo. Ulielekezwa visivyo kuhusiana na nafasi ya agano la Sinai [la Musa] kafika mpango wa wokovu, walitumaini lihusishwe kwa watu wa Mungu (uzao wa Ibrahimu) kwa njia isiyo sahihi (matendo ya sheria)." (Silva 2007: 793)

Katika **mst. 6** Paulo anaanza kwa kunukuu **Mwz 15:6**. Katika **Mwanzo 15**, Mungu alikuwa amemwahidi Ibrahimu uzao kama nyota za angani ingawaje Ibrahimu alikuwa hana mtoto, mzee wa miaka zaidi ya 80, na mkewe alivuka ule umri wa kuweza kuchukuwa mimba na kuzaa watoto. Hata hivyo Ibrahimu *"alivyomwamini Mungu, akahesabiwa haki."* Imani ya Ibrahimu ilidhihirishwa katika muktadha wa Agano la Ibrahimu. Agano lile lilikuwa limetolewa hapo awali na Mungu kwa Ibrahimu katika **Mwz 12:1-3**. Na baadaye likatamkwa tena katika **Mwz 13:14-17; 15:1-21; 17:1-21; 22:15-18** na likathibitishwa kwa mwana wa Ibrahimu Isaka (**Mwz 26:1-5, 24**) na kwa mwana mdogo wa Isaka Yakobo (**Mwz 28:3-4, 13-15; 35:11-12**). Agano la Ibrahimu linaonekana katika AK lote na kukutana na utimilifu wake katika Kristo. Kwa hiyo, linaweza kuchukuliwa kama ndio uti wa mgongo wa kitheoloji na mpango makini wa Biblia yote. Agano la Ibrahimu na tamko kwa Ibrahimu *"alivyomwamini Mungu, akahesabiwa haki"* ndio ufunguo wa mjadala wa Paulo katika **Wagalatia 3-4**. Agano la Ibrahimu lilikuwa na ahadi tatu kuu: ahadi ambazo zilihusiana na ardhi, mbegu (baraka za uzao), na baraka za dunia yote (m.y, ahadi zilizohusiana na baraka za watu wengine kuhusiana na mbegu ya Ibrahimu).[11]

Wakati ambapo **mst. 6** huzungumzia ile "mbegu" ya baraka ya agano, **mst. 8** unanukuu **Mwz 12:3** kuhusiana na ahadi za agano kubariki mataifa yote kupitia mbegu ya Ibrahimu. **Mstari 8** pia inasema kwamba Mungu *"lilimhubiri Ibrahimu habari njema zamani."* Yesu alitaja hili katika **Yohana 8:56** alipowaambia wale Wayahudi, *"Ibrahimu, baba yenu, alishangilia kwa vile atakavyoiona siku yangu; naye akaiona, akafurahi."* Kwa sababu Agano la Ibrahimu hatimaye lilielekezwa kubariki dunia yote, matumizi ya Paulo kwa ajili yetu yanapatikana katika **mst. 7** (*"hao walio wa imani ambao ni wana wa Ibrahimu"*) na **mst. 9** (*"hao walio wa imani hubarikiwa pamoja na Ibrahimu aliyekuwa mwenye imani"*). Kwa maneno mengine, kama ambavyo Paulo anasema hapa na kurudia kusema tena na tena katika sura yote ya **Sura 3** na **4**, Mbegu ya kweli ya Ibrahimu ni ya kiroho, na sio ya kimwili; watoto wake wa kweli ni wale ambao wana imani, kama vile Ibrahimu alivyokuwa na imani. Kama vile Mungu alivyomwahidi Ibrahimu ya kuwa uzao wake watakuwa wengi kama nyota za mbinguni (**Mwz 15:5**), hilo limetimia kwa njia ya kanisa la Kristo (m.y., mbegu ya kiroho ya kweli ya Ibrahimu), ambayo ni pamoja na watu *"wa kila taifa, na kabila, na jamaa, na lugha"* duniani (**Ufu 5:9; 7:9**). **Mstari 7** na **9** inabainisha kwamba, katika AK na AJ, Mungu wakati wote amekuwa na mpango mmoja wa wokovu kwa neema kwa njia ya imani. Kutajwa kwa Ibrahimu kuwa aliisikia "injili" na ukweli kwamba wana wa kweli wa Ibrahimu ni *"wale walio wa imani"* huonyesha hilo. Tofauti pekee kati ya Ibrahimu na sisi ni kwamba Ibrahimu *alitarajia* kwa imani ile kazi ya Kristo kwa niaba yake, wakati ambapo sisi twatakiwa kuangalia *kule nyuma* kwa imani kwenye ile kazi ya Kristo kwa niaba yetu.

[11] Agano la Ibrahimu na kutimia kwake katika Kristo limejadiliwa kwa kirefu katika Menn 2009-2018: 14-15, 30-34 na Menn n.d.: Gen 15:1-18-"Unabii Mkuu katika Biblia."

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

- **3:10-14—**Hakuna anayehesabiwa haki kwa sheria ispokuwa yuko chini ya laana.

[10] Kwa maana wale wote walio wa matendo ya sheria, wako chini ya laana; maana imeandikwa, AMELAANIWA KILA MTU ASIYEDUMU KATIKA YOTE YALIYOANDIKWA KATIKA KITABU CHA TORATI AYAFANYE." [11] Ni Dhahiri ya kwamba hakuna mtu ahesabiwaye haki mbele za Mungu katika sheria; kwa sababu "MWENYE HAKI ATAISHI KWA IMANI." [12] Na torati haikuja kwa imani, bali "AYATENDAYE HAYO ATAISHI KATIKA HAYO." [13] Kristo alitukomboa katika laana ya torati, kwa kuwa alifanywa laana kwa ajili yetu; maana imeandikwa, "AMELAANIWA KILA MTU AANGIKWAYE JUU YA MTI;" [14] ili kwamba baraka ya Ibrahimu iwafikie Mataifa katika Yesu Kristo, tupate kupokea ahadi ya Roho kwa njia ya imani.

Neno "Kwa maana," ambalo huanza aya hii, huonyesha kwamba **mst. 10-14** ina uhusiana na **mst. 6-9**. Hata hivyo, "Kuna badiliko linaloonekana kutoka mstari wa 9 hadi wa 10. Paulo anatoka kwenye lile dokezo kwamba wana wa Ibrahimu ndio wana wa imani peke yake, hadi kuweka wazi kwamba sheria huleta laana, na ya kwamba wale wanaotafuta kuhesabiwa haki kwa utii wao kwa sheria, kwa hakika watajikuta wako chini ya laana ya sheria! Hebu ona ule utofauti ambao Paulo anaufanya hapa kati ya 'yule mtu wa imani' (katika mstari wa 7-9) na 'wote ambao huitegemea sheria,' katika mstari wa 10. Ni uchaguzi wa kati ya kimoja au kingine. Ama unahesabiwa haki kwa neema peke yake kwa njia ya imani ndani ya Kristo peke yake, vinginevyo uko chini ya laana ya sheria." (Riddlebarger 2003: n.p.)

Kumbuka kwamba walikuwa ni watu waliokuwa wakidai kuwa wao ni Wakristo—wale Wayahudishaji—ambao waliwataka Wakrisro wengine wajiweke wao wenyewe chini ya Sheria ya Musa baada ya kumpokea Kristo. John Piper anatoa maoni, "Sababu inayofanya kitabu cha Wagalatia kuwa na ujumbe mkali wa jinsi hii wenye kubadili maisha ni kwamba unatamka laana kutoka kwa Mungu sio kwa wasiomwamini Mungu au kukubali uwepo wa habari za kwamba Mungu yuko bali kwa wale wanaodai kuwa wao ni Wakristo ambao wanajaribu kumtumikia Mungu kwa njia ambayo huishusha thamani neema yake na kurutubisha kiburi chao" (Piper 1983a: n.p.). Uzima na mauti hugawanyika kati ya Baraka za kiungu na laana za kiungu "sio kati ya watu wa kanisa na watu wasio wa kanisa, wala sio kati ya wale wamwitao Yesu 'Bwana' na wale wasiofanya hivyo. Ni kati ya wale, kwa upande mmoja wamesulibiwa pamoja na Kristo na sasa wakiwa maskini wanaendelea kuishi kwa kumtegemea Kristo aishiye, na wale, kwa upande mwingine, ambao kamwe hawajawahi kufa katika nafsi zao na ambao matendo yao ya kidini, ingawaje 'ni ya kimaadili' na ya ukali, ni bidii ya kibinafsi ya kujifanyia matengeno." (Ibid.) Kwa hiyo, kila wanaodai kuwa wao ni Wakristo ni lazima mara kwa mara wajichunguze wenyewe kwa uaminifu ili kuona kama kweli tunamtukuza na kumheshimu na kumtegemea Kristo ndani yetu au tunajiinua sisi wenyewe tu (ona **2 Kor 13:5**).

Hii mistari mitano inaanza na laana lakini kisha inaendelee kusema dawa pekee ya ile laana—ni uwepo wa Yesu Kristo na ile kazi yake na zile baraka anazokuja nazo. Hapa kuna mambo matatu yanayoendelea katika mazingira haya ambayo yalishatajwa hapo awali. Jambo la kwanza ni swala la kushika sana sheria. Katika muktadha bayana ambao unahusu swala la Paulo kuwaandikia Wagalatia, kushika sana sheria ndilo lililokuwa dai la Wayahudishaji ya kuwa mtu anaweza kuokoka kwa imani ndani ya Yesu lakini ni lazima aitimize sheria ya Musa ili adumu katika wokovu. Hilo ni tatizo kwa makanisa mengi hivi leo, hata kama tohara sio lile jambo bayana ambalo linatatiza. Jambo la pili, kushika sana sheria ni matumizi bayana ya swala la kiujumla, ambalo ni, ule ukweli kwamba kuna aina mbili tu ya dini duniani: dini zilizofanywa na wanadamu ambazo misingi yake iko katika kigezo kwamba wokovu wa mtu (upendeleo wa Mungu) unapatikana kwa juhudi za mtu katika kufanya matendo mema au kufuata sheria na amri zilizowekwa na watu (ambazo sio lazima ziwe ni Sheria ya Musa), m.y., dini ya "matendo," dhidi ya Ukristo, ambao misingi yake ni katika kile ambacho Kristo amekifanya kwa ajili yetu, m.y., dini ya "neema." Mambo haya yote yalishajadiliwa hapo awali kuhusiana na **Gal 2:1-5, 15-21**, na **3:1-5**. Yanahusiana na swala la tatu—swala la upekee wa Wayahudi—ambalo lilijadiliwa awali kuhusiana na **Gal 2:11-14**. Kushika sana sheria au aina yoyote ya dini ambayo misingi yake ni matendo moja kwa moja hupindua Agano Jipya na kuwaweka watu tena katika Agano la Kale. Zaidi ya hayo hili lina maana katika tabia zetu: ni injili peke yake ambayo iko kamili; lakini kushika sana sheria kwa aina yoyote (iwe ni wale Wayahudishaji wa Galatia au dini za leo za kushika sheria za wanadamu), kwa asili yake kabisa huwatenga wale ambao hawakidhi vigezo halisi vya ushikaji wa sheria au wale ambao si wanachama wa mbari au kabila halisi.

Tatizo ambalo lipo kwa dini yoyote ile ambayo vigezo vyake ni matendo (ikiwa vinahusiana na wokovu au utakaso) linawekwa wazi na nukuu ya Paulo katika **mst. 10** kutoka **Kumb 27:26** ya kuwa yeyote asiyeshika na kutenda *"yote yaliyoandikwa katika kitabu cha torati"* amelaaniwa. Yakobo anaonyesha jambo lilo hilo katika **Yak 2:10** ambapo alisema, *"Maana mtu awaye yote atakayeishika sheria yote, ila akajikwaa katika neno*

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

moja, amekosa juu ya yote." Ukweli ni kwamba hakuna ye yote kamwe ambaye amewahi au anaweza kwa ukamilifu kuitii sheria; kwa hiyo, kila mtu yuko chini ya ile laana.[12] Katika **mst. 11** Paulo ananukuu **Hab 2:4** (*"Mwenye haki ataishi kwa imani yake"*). Kim Riddlebarger anadokeza kwamba Habakuki anasema, "Ni kwa kupitia imani pekee mtu anapokea haki na ataishi" (Riddlebarger 2003: n.p.). Kwa kuwa hilo ni kweli, ni "dhahiri" (wazi; iliyonyooka; isiyo shaka) kwamba hakuna mtu ye yote ambaye anaweza kuhesabiwa haki kwa kuitii Sheria.[13]

Paulo anawekea mkazo jambo hili katika **mst. 12** kwa kunukuu **Wal 18:5** (*"mtu akizitumia [sheria za Mungu na hukumu] ataishi kwa hizo"*) ili kuweka dokezo kwamba *"Torati si ya imani."* Inaweza kuonekana kwamba **Wal 18:5** inadai kwamba mtu anaweza kuokoka kwa kutenda matendo ya Sheria (kwa kuwa **Hab 2:4** na **Wal 18:5** hutumia neno "kuishi"). Hata hivyo, Paulo anauweka mstari huu katika kupingana na **Hab 2:4**. Sababu ni kwamba Paulo anaitazama imani dhidi ya matendo na ile sheria katika muktadha wa historia ya ukombozi. Alitangulia kulisema jambo hili hapo nyuma katika sura hii kwa kumtaja Ibrahimu, na ataendelea kusema kwa upana juu ya hili katika sehemu iliyobaki ya sura. Wakati Paulo anasema *"ile Sheria si ya imani,"* anasema ya kuwa Agano la Musa lote (ikiwa pamoja na Sheria ambayo ilikuwa sehemu ya lile agano) "ni vya kipindi tofauti cha ukombozi kikilinganishwa na injili" (Silva 2007: 804; ona pia Garlington 1997: 101). Paulo ataendelea kudokeza kwamba Sheria ya Musa ilikuja miaka 430 baada ya Agano la Ibrahimu na haikuweza kila mwaka kutekeleza lile agano ambalo lilikuwa na misingi katika *imani* ya Ibrahimu (**Gal 3:17**); hivyo, katika mantiki moja, Sheria ilikuja *baada* ya kanuni ya imani.[14] Kwa upande mwingine, **Gal 3:23-25** inasema kwamba ile Sheria kabla ya kuja kwa Kristo na ilikusudiwa *kutuongoza* sisi kwenye imani ndani ya Kristo; hivyo, kwa maana nyingine, ile Sheria ilikuja *kabla* ya ule wakati wa imani. Kwa namna yoyote, ile Sheria iko mbali na haifanani na imani na, kwa hiyo, *"ile Sheria si ya imani."*

Jambo lililo muhimu zaidi kuliko lile la *mpangilio wa muda* wa Agano la Musa na ile Sheria na kuhusiana na imani na ule ukweli kwamba Agano la Musa na ile Sheria vilikuwa na kusudi tofauti kabisa mbali na injili. Katika **mst. 10** ile nukuu kutoka **Kumb 27:26** imedokeza kwamba "matendo" na "Sheria" inahusiana na "kufanya," ikitofautiana na "imani" ambayo inahusiana na "kusikia" (**Gal 3:2, 5**) na "kuamini" (**Gal 3:6**). Todd Bordow anaeleza kwa muhtasari, "Ile kanuni ya sheria ya Musa na kanuni ya Injili hupingana zenyewe. Ile njia ambayo ingetumika ambayo kwayo taipolojia na baraka za kitambo za agano la Musa zingekuja ni kwa kupitia matendo ya sheria. Zile thawabu za utii zilikuwa ni baraka za taipolojia za nchi ya Kaanani. Zile laana zingekuwa ni hukumu juu ya watu kwa njia ya kuchukuliwa mateka nje ya ile nchi. Lakini kisha Kristo alikuja. Ni kile ambacho lile Agano la Musa lilidokeza kilikuwa kimekuja. Kile ambacho kilikuwa utimilifu wa ile ahadi ya Ibrahimu kilikuwa kimekuja. Sasa ile kanuni ya injili inapingana na ile ya Sheria ya Musa. Sasa tuko chini ya neema. Hili ndilo dokezo la Paulo katika Wagalatia 3. Ustahili ambao unatupatia baraka za agano hili si utii wetu, bali utii wa Kristo. Faida zote za agano hili huja kwetu kwa njia ya imani. Tunapokea faida za agano hili si kwa njia ya matendo yetu, bali kwa njia ya imani. Na Mungu anaendelea kutuhudumia zile faida za agano hili kwa njia ya imani. Hivyo zile baraka zote ambazo Kristo ametushindia, ikiwa ni pamoja na utakaso, hutujia kwa

---

[12] John Piper anaweka dokezo muhimu kwamba, katika muktadha wa Wagalatia, "Ile laana katika mstari 10 si kwa sababu *unashindwa* kufanya matendo ya sheria. Ni kwa sababu *unayafanya*. Ule ushauri wa Wayahudishaji kuongezea 'matendo ya sheria' katika imani unaleta matokeo yaliyo kinyume kabisa na yale yaliyotarajiwa—unaleta laana, sio baraka. Ni wakati ule ambapo Petro alianza *kufuata* sheria za kula ndipo Paulo alisema alikuwa nje ya utaratibu wa injili na kuivunja sheria. Ni wakati ule ambapo wale Wayahudishaji walipotaka *kufuata* amri ya kumtahiri Tito katika 2:3 ndipo Paulo aliposema kwamba kweli ya injili ilikuwa iko hatarini. Tatizo walilokuwa nalo Wayahudishaji si kushindwa kwao kufuata yale maelekezo yaliyoanishwa katika sheria; tatizo lilikuwa kwamba walilikosa somo kubwa la sheria, ambalo ni, kwamba bila ya moyo mpya (Kumb. 30:6, 7) na bila kuwezeshwa na Mungu (Kumb. 4:30, 31; 5:29; 29:4) na bila ya imani (Kut. 14:31; Hesb. 14:11; 20:21; Kumb. 1:32) juhudi zote za kutii sheria zitakuwa tu ni mahangaiko ya kimwili katika kushika sana sheria." (Piper 1983a: n.p.)

[13] Paulo hapo awali alisha dokeza katika **Gal 2:16** (ona pia **Rom 3:20**). Silva anaongezea kwamba dondoo ya Paulo ya hapo awali ya **Mwz 15:6** (*"Ibrahimu akamwamini Bwana , naye akamhesabia jambo hilo kuwa haki"*) na ile dondoo hapa kutoka **Hab 2:4** (*"Mwenye haki ataishi kwa imani yake"*) kwa kweli inaweza kuwa inashughulika na wazo moja—ile asili ya kweli, imani iokoayo: "Nabii [Habakuki] alikuwa akiwashawishi watu wa Yuda kufuata nyayo za Ibrahimu, ambaye imani yake haikuwa tukio la mara moja tu, bali maisha yake yote alikuwa na utii ulioambatana na uvumilivu (ona hasa Mwz. 22, ambayo ndio msingi wa Yakobo 2:21-24). Imani inahusisha kusubiri kutendeka kwa jambo na hivyo wakati wote iko katika hatari ya kutikiswa; kwa hiyo, uimara na uthabiti ni muhimu." (Silva 2007: 802)

[14] Ile "imani" inayozungumziwa hapa si tu kanuni ya kiujumla au hata "imani kwa Mungu kiujumla," bali ni imani katika Yesu Kristo, kuiamini injili. **Gal 3:8** inaonyesha hili inaposema kwamba Mungu *"alimhubiri Ibrahimu habari njema zamani"* (ona pia **Yohana 8:56**, *"Ibrahimu, baba yenu, alishangilia kwa vile atakavyoiona siku nyangu; naye akaiona akafurahi"*).

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

njia ya imani." (Bordow 2018: n.p.)[15]

Rum 10:4 inatuambia kwamba *"Kwa maana Kristo ni mwisho wa sheria, ili kila aaminiye ahesabiwe haki."* Neno la Kiyunani kwa neno "mwisho" ni *telos,* ambalo humaanisha kikomo, ukamilishaji, au lengo. Zodhiates anaelezea maana ya *telos* katika **Rum 10:4**: "Kristo ni mwisho wa Sheria, ili kila aaminine ahesabiwe haki. Hii humaanisha kwamba Sheria kama wajibu unaodaiwa imefikia mwisho wake kwa sababu Yesu ameshatimiza madai yake na kuwapa haki yake wale wanaoamini. Kristo amewaweka huru waaminio mbali na uonevu wake. Yale matarajio ya haki hutujia sisi si kutoka nje yetu kwa kuwekewa madai, bali kutoka ndani yetu kwa njia ya Roho ambaye anaandika ile Sheria mioyoni mwetu." (Zodhiates 1993: *telos,* 1376-77) Kwa kuwa huyu (Kristo; injili) ndio mwisho wa mambo ya nyakati hizi kuhusiana na ile Sheria, hiki ndicho kile ambacho sheria yote ya Musa ilikuwa imetangulia kukilenga hapo awali. Garlington anahitimisha kwa kuelezea ni kwa nini nukuu ya Paulo ya **Kumb 27:26** katika **Gal 3:10** hudhihirisha namna vile ambavyo kuja kwa Kristo duniani hubadilisha uhusiano wa historia ya ukombozi wa ile Sheria, baraka za Mungu, na laana za Mungu: "Ni wajibu wa kinyume unaotokana na mazingira yanayohusu habari za theolojia ya nyakati za mwisho ambayo hufungua njia ya kuelewa lile tatizo ambalo liliainishwa mwanzoni mwa insha hii, ambalo ni, ambapo Gal. 3.10a hutamka laana juu ya ye yote ambaye atajaribu kuishi kwa Torati, kifungu cha Biblia ambacho kwacho Paulo anasihi, Kumb. 27.26, unatamka ambacho ni kinyume: laana haiwapati wale wanaoitimiza Sheria, bali wale wanaoshindwa kuitimiza (Gal. 3.10b). . . . Hii ndio kusema, katika ile hali yao ya kuishika sheria, wale wapinzani hawakuishika, kwa sababu hawajai 'tetea' kwa kufuatana na mpango wa theolojia ya nyakati za mwisho, ambayo ni, kuielekeza Israeli kwa Yesu wa Nazareti ambaye ndiye aliyeondoa vizuizi vya utengano kati ya mataifa. Hivyo 'udanganyifu' wao ni pamoja na kuendelea kuishika Torati kwamba *ipso facto* ilikuwa ya kuzuiliwa kiuzalendo. Kuieleza tena kwa njia nyingine, ni kwa sababu wapinzani wanabaki na utambulisho wao kama Wayahudi wa kundi la Musa ya kuwa wameshindwa 'kutimiza ile sheria'." (Garlington 1997: 120)

Kwa kutaka kuendelea kuwa na ile hali ya upekee kama Wayahudi kwa misingi ya ile Sheria ya Musa, Wayahudishaji walikuwa wakifanya yaliyo kinyume na ile kazi ya sheria ya theolojia ya nyakati za mwisho ambayo ilikuwa imekusudiwa kutoa baraka na laana kwa kutegemeana na msimamo wa mtu kuhusiana na uhusiano wake na Yesu Kristo. Wale Wajahudishaji' (au washika sheria wowote) hujaribu kuijaliza neema ya Mungu kwa njia ya imani kwa kuiongezea masharti ya sheria kwa kile ambacho Kristo pekee amekifanya ni kinyume na injili na ni kinyume na kusudi la sheria yenyewe (ambalo lilikuwa ni kudhihirisha ule utegemezi wetu kwa Kristo peke yake usiopinga). Kwa hiyo, hata kama mtu angekuwa na uwezo wa kuyafuata *kikamilifu* matakwa ya sheria zozote zile za ziada, yeye huyo bado atakuwa yuko chini ya laana ya Mungu kwa sababu yeye atakuwa akitenda kinyume na Mungu, kinyume na Kristo, na kinyume na kusudi la sheria kwa kujaribu kuupata wokovu wake kwa njia ya matendo yake. Hivyo, kutokana na msimamo wa kitheolojia na wa nia, kuongezea "matendo ya sheria" yoyote kwa kile ambacho Kristo pekee amekifanya humuweka mtu kuwa chini ya laana. Bila shaka, kwa kutokana na msimamo wa kiutendaji ule ukweli kwamba hakuna ye yote (ispokuwa Kristo) amesha wahi au ataweza kuitii sheria yote kikamilifu hilo pia humuweka chini ya laana yule ambaye anajaribu kufanya hivyo. Chaguo *pekee* ambalo linaweza kuleta uzima ni neema ya Mungu tu kwa njia ya imani yetu peke yake ndani ya kile alichokifanya Kristo peke yake.

Mstari 13-14 unatupa ufumbuzi dhidi ya ile hali ya upungufu wa ile sheria na laana ambazo inazileta: Kristo na kile alichokifanya msalabani. In **mst. 13** Paulo anatoa nukuu kutoka **Kumb 21:23** (*"amelaaniwa kila mtu aangikwaye juu ya mti"*). Neno la Kiyunani lililotafsiriwa kama "mti uliohai" ni *xulon* ambalo humaanisha hasa "mti uliokatwa." Katika muktadha huu inazungumza kuhusu msalaba na kwa njia iyo hiyo ndivyo imetumika katika **Matendo 5:30; 10:39; 13:29**; na **1 Pet 2:24**, yote pia husema kuhusu Yesu kuangikwa msalabani. Kwa kuzileta hizi dondoo mbili kutoka katika Kumbukumbu la Torati pamoja katika kifungu hiki (m.y., **Kumb 27:26** katika **mst. 10** na **Kumb 21:23** katika **mst. 13**), Paulo anasema kwamba *Yesu aliichukuwa laana kutoka kwa Mungu kwa ajili yetu* msalabani. Hii ina maana kwamba Kristo alitukomboa kutoka katika laana ya sheria kwa njia ya yeye mwenyewe kulipia ile adhabu kwa ajili ya dhambi zetu ambayo vinginevyo sisi

[15] Ni muhimu kutambua kwamba ile Sheria ya Musa haikusamehe dhambi wala kutoa uzima wa milele. Agano Jipya litakuwa ni agano la milele ambalo kwa hilo Mungu ataiandika sheria yake ndani ya mioyo ya watu Wake, watu Wake wamjua Bwana kwa hakika, na atawasamehe dhambi zao na hatazikumbuka tena kamwe (**Yer 31:34**; ona pia **Yer 32:38-40; 50:4-5; Ezek 11:14-20; 36:24-32; 37:15-28**). Agano Jipya ambalo Yesu aliliasisi kwa damu yake (**Luka 22:20**; ona pia **1 Kor 11:25**) hutoa uzima wa milele (**Rum 6:22**). Ule "upya" wa Agano Jipya "haupaswi kudharauliwa; unahusisha viwango tofauti vya mawazo mapya ambavyo huakisi kiini cha kutokuendelea kwa mambo ya zamani (cf. Yer. 31:32): kuondolewa kwa dhambi kabisa (Yer. 31:34; Ezek. 36: 29, 33); badiliko la ndani la moyo (Yer. 31:33; Ezek. 36:26); uhusiano wa karibu sana na Mungu (Yer. 31:34a; Ezek. 36:27)" (Williamson 2007: 180). Ile asili ya taipolojia ya nyanja tofauti za Agano la Kale na kutimilika kwake ndani ya Kristo na kanisa vinajadiliwa kwa kirefu katika Menn 2009-2018: 26-93.

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

wenyewe tungeilipia (ingawaje tusingeweza kamwe). Kwa ajili ya jambo hilo, Mungu kamwe haziweki dhambi zetu juu yetu (kwa kuwa Kristo alizichukuwa juu yake na ile adhabu ambayo ilizistahili). "Ni kwa sababu kufanyika kwa Kristo kuwa laana *kwa ajili* yetu, na hivyo kuiondoa ile laana *kutoka* kwetu, ya kwamba tunaweza kuhesabiwa haki kwa imani na kuwa watoto wa Ibrahimu" (Riddlebarger 2003: n.p.). Ile sababu iliyomfanya afanye hayo imetajwa katika **mst. 14**, ambayo ni, kwamba ndani ya Kristo tuzipate zile baraka za Ibrahimu, hasa ile ahadi ya Roho Mtakatifu.[16] Kwa maneno mengine, Kristo alifanyika kuwa laana kwa ajili yetu ili sisi tuzipokee zile baraka ambazo Ibrahimu aliahidiwa, kwa sababu tunapokuwa tumeunganishwa na Kristo kwa njia ya imani tu watoto halisi wa Ibrahimu.

Kwa upande mwingine, kuukataa ule utoshelevu kamili wa Kristo na kile alichokitimiza pale msalabani—kushika kwamba kitu kingine chochote badala ya au pamoja na imani juu ya kile ambacho Kristo amekifanya ni lazima kwa ajili ya wokovu wa mtu (kama wale Wayahudishaji walivyokuwa wakifanya)—ni kujiweka mwenyewe chini ya laana. Garlington anaeleza ni kwa nini: "Kumb. 21.23 na 27.26 inakubaliana na laana ya [Paulo] ya Gal. 1.8-9, ambayo inaweza kutafsiriwa, 'Amelaaniwa mtu ye yote yule ambaye kimsingi si mwaminifu kwa injili'. Kuna, mtu anaweza kusema, si tu 'ile laana ya sheria', lakini pia 'ile laana ya injili', ni laana ambayo imetamkwa dhidi ya wale ambao watairudia sheria. Kwa hiyo kwa kejeli, ile laana ya injili ni laana ya sheria itokanayo na theolojia ya nyakati za mwisho inayoamriwa juu ya wale ambao huitaka hiyo badala ya Kristo anayehubiriwa na Paulo." (Garlington 1997: 119)

Kuna nyanja mbili muhimu za kiutendaji kuhusiana na hili:

- Kwanza, katika **mst. 14** Paulo anataja tena kwamba Mungu alishaahidi kuwabariki Mataifa (au "mataifa") kupitia Ibrahimu (ona **Gal 3:8**; ona pia **Mwz 12:3; 17:4-6; 18:18; 22:18; Matendo 3:25**). Baada ya kuzungumza kuhusu zile baraka za Ibrahimu ambazo zingekuja kwa Mataifa, kisha Paulo anasema *"ili kwamba baraka ya Ibrahimu iwafikie Mataifa katika Yesu Kristo."* Ingawaje yeye mwenyewe Paulo alikuwa Myahudi, alikuwa akijiweka kuwa yu sawa na Mataifa—hata alijiita yeye mwenyewe Mmataifa. Jambo hilo huonyesha ile nguvu kubwa ya kiutendaji ya kuleta usawa iliyomo ndani ya injili. Kama ambavyo Paulo anasema baadaye, *"Hapana Myahudi wala Myunani. Hapana mtumwa wala huru. Hapana mtu mume wala mtu mke. Maana ninyi nyote mmekuwa mmoja katika Kristo Yesu"* (**Gal 3:28**; ona pia **Kol 3:11**). Hili hutufikisha kuona kuwa ni kwa nini wale Wayahudishaji na Petro walikuwa wamekosea sana katika **Gal 2:11-14**. Upekee wao wa Kiyahudi ulikuwa kinyume na injili moja kwa moja. Hili ni sawa pia na upekee wa kanisa lolote lile na ule upekee miongoni mwa Wakristo (mfano, upekee kwa misingi ya mbari, kabila, hali ya kiuchumi, au kwa mambo mengine yanayofanana na hayo).
- Pili, kile ambacho hutuweka sisi chini ya baraka za Mungu au chini ya laana ya Mungu si sana kile unachofanya ukilinganisha ile nia ya moyoni ambayo kwayo unafanya. Kutahiriwa kwaweza kuwa 'tendo la sheria' [**Gal 2:1-5**] au tendo ambalo kwalo upendo hutiririka kutoka katika imani [**Matendo 16:3**]. Kujitiisha mwenyewe katika sheria za chakula yaweza kuwa 'tendo la sheria' [**1 Kor 8:7**] au tendo huru la upendo ambalo hutokana na imani [**Rum 14:21; 1 Kor 8:13**]. Kufundisha darasa la Shule ya Jumapili, kuhubiri, harakati za kupinga utoaji wa mimba, maandamano ya kupinga matumizi ya nyuklia, kujihusisha na ugawaji wa chakula jijini, ajira yako—hivi vyote vyaweza kuwa 'matendo ya sheria' ambayo tunayafanya kwa nguvu zetu, ili kuuvuta upendeleo wa Mungu kwetu, au yanaweza kufanywa kwa unyenyekevu kwa kuzitegemea nguvu za Mungu ambazo Yeye hutupatia bure ili katika kila kitu aweze kutukuzwa. Uamuzi wa laana au baraka hutegemea vile *namna* unavyotii [au, mtu anaweza kusema, *kwa nini* unatii] na ni nani anapata sifa." (Piper 1983a: n.p.)

- **<u>3:15-24—</u>**<u>Makusudi ya sheria.</u>

Katika vifungu vidogo vitatu vifuatavyo Paulo anaendelea kujadili umuhimu wa lile Agano na Ibrahimu na ile Sheria ya Musa katika mchakato wa historia yao ya ukombozi. Ni muhimu kutambua kwamba mapatano ya Mungu na Ibrahimu na Musa yalikuwa na misingi katika kanuni mbili tofauti. Kwa Ibrahimu Mungu alitoa *ahadi*; kwa Musa Mungu alitoa *sheria*. *Ahadi* ni Mungu kusema, "Nita…"; *sheria* inasema, "uta…" na "huta…" *Ahadi* ni ya *kuaminiwa*; *sheria* ni ya *kuitii*. Zaidi ya hayo, wakati lile Agano na Ibrahimu lilipokuwa

[16] Ahadi ya kwanza ya Ibrahimu haikumtaja Roho Mtakatifu. Hata hivyo, "Paulo anapata kujua kuhusu utimilifu wa ahadi ile kama ilivyoanzishwa juu ya vyote kukirimiwa kwa Roho kwa wale walio na imani. Imedhihirika kwamba katika mawazo ya Paulo zile baraka za kuhesabiwa haki zina uhusiano ulio karibu sawa na (kwa hakika hutokea kwa wakati mmoja) kumpokea Roho. Kwa hiyo baraka zote za ahadi, msamaha wa dhambi, kupewa haki na 'ile hali ya kusimama bila hatia' mbele za Mungu, na zawadi ya kipawa cha Roho Mtakatifu, huja kwetu kwa njia ya kutenda na kufa kwa Yesu Kristo tu na hupokelewa kwa njia ya imani ***tu***." (Riddlebarger 2003: n.p.)

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

limeidhinishwa Mungu mwenyewe alikuwa dhiye mdhamini kwamba lile agano litatimizwa (ona **Mwz 15:7-18**; Menn n.d.: Mwz 15:1-18-"Unabii ulio Mkuu katika Biblia"). Kwa upande mwingine, Waisraeli waliapa kwamba *wao* wangeitimiza Sheria ya Musa (**Kut 24:3**). Mantiki ya Paulo ni kwamba Ukristo ni dini ya Ibrahimu. Kama tutakavyoona, ile sheria hutumikia kusudi, lakini ile ahadi na ile sheria haipaswi kutokueleweka au kuchanganywa.

- **3:15-18—**Sheria haiwezi kuweka agano na Ibrahimu kila mwaka.

  [15] Ndugu zangu, nanena kwa jinsi ya kibinadamu. Lijapokuwa ni agano la mwanadamu, hata hivyo likiisha kuthibitika, hakuna mtu alibatilishaye, wala kuliongeza neno. [16] Basi ahadi zilinenwa kwa Ibrahimu na kwa mzao wake. Hasemi, "kwa wazao," kana kwamba ni wengi bali kana kwamba ni mmoja, "Kwa mzao wako," yaani Kristo. [17] Nisemalo ni hili; agano lililothibitishwa kwanza na Mungu, torati iliyotokea miaka mia nne na thelathini baadaye hailitangui, hata kuibatilisha ile ahadi. [18] Kwa maana urithi ukiwa kwa sheria, hauwi tena kwa ahadi; lakini Mungu alimkirimia Ibrahimu kwa njia ya ahadi.

Neno "agano" ni neno la Kiyunani *diathēkē,* ambalo ni neno lile lile lililotumika sawa na "wosia" au "hati ya wasia." Wakati ambapo Paulo anaanza sehemu hii kwa kusema kwamba anazungumza kwa misingi ya mahusiano ya kibinadamu, wosia wa mtu ndicho kile ambacho wasomaji wake wanakitazama katika fahamu zao. Umuhimu wa hili ni kwamba hakuna mwingine awezaye kuubadilisha wosia wa mtu ispokuwa yule aliyeuandika na "chini ya baadhi ya mifumo ya kisheria ya kale, hata yule aliyeuandika wosia hawezi kuufuta wosia halali au kuongezea kiambatisho cha kufafanua zaidi au kutangua sehemu fulani" (Mikolaski 1970: 1098). Jambo hili ni muhimu kwa njia tatu zinazohusiana:

- Kwanza, kwa kuwa wosia wa mwanadamu haukuweza kuwekwa pembeni au kubadilishwa, je si zaidi sana agano la Mungu lazima libaki pasipo kubadilishwa.
- Pili, katika **mst. 16**, ingawaje neno "mbegu" (kama vile neno "kondoo") huweza kumaanisha kundi au mmoja, Paulo anabainisha kwamba lile agano la Ibrahimu halikuwa kwa mbegu ya mwilini(uzao) ya Ibrahimu lakini inatimilika katika mbegu moja maalum, ambayo ni, Kristo. Paulo anadokeza ya kwamba, hata kama Waisraeli wangekuwa na uwezo wa kuitimiza sheria (ambayo hawakuweza), wao wasingekuwa utimilifu wa lile agano. Badala yake, "lile Agano la Ibrahimu lingetimizwa na mtu ambaye ni mkombozi, si kwa njia ya mkusanyiko wa sheria zinazofuatwa na wengi" (McClelland 1989: 1013).
- Tatu, **mst. 17-18** inadokeza kwamba ahadi na sheria ni vitu vya makundi mawili tofauti; vina makusudi na kazi ambazo hutofautiana. Ule "wosia ["hati ya wasia ya Mungu" au agano na ahadi kwa Ibrahimu] ni vya Ibrahimu na uzao wake. Huja kwa njia ya zawadi na huwakalia wale ambao huchukuwa nafasi katika hilo kwa haki ya urithi. Mwenye kuandika wosia humuonyesha mrithi wake na hupanga kwamba katika muda uliokwisha kupangwa atapokea ahadi iliyobainishwa (Gal. 4:2)." (Zodhiates 1993: *diathēkē,* 427). Kwa kuwa urithi hutegemea ahadi na imani, sheria iliyotolewa baadaye kwa mtu mwingine [Musa na taifa la Israel] haiwezi kubatilisha agano ambalo lilitolewa na kuthibitishwa hapo awali na ahadi na haki za urithi zilizotolewa na agano na ahadi.

- **3:19-22—**Sheria huifunua hali yetu ya dhambi.

  [19] Torati ni nini basi? Iliingizwa kwa sababu ya makosa, hata aje huyo mzao aliyepewa ile ahadi; iliamriwa kwa utumishi wa malaika kwa mkono wa mjumbe. [20] Basi aliye mjumbe si mjumbe wa mmoja; bali Mungu ni mmoja. [21] Basi je! torati haipatani na ahadi za Mungu? Hasha! Kwa kuwa, kama ingelitolewa sheria iwezayo kuhuisha, yakini haki ingepatikana kwa sheria. [22] Lakini andiko limeyafunga yote chini ya nguvu ya dhambi, makusudi hao waaminio wapewe ile ahadi kwa imani ya Yesu Kristo.

Kwa kuwa Paulo ametuambia hivi punde kile ambacho sheria haiwezi kukifanya, sasa anafafanua lile kusudi la ile sheria ni nini. Katika **mst. 19** anasema kwamba sheria *"iliingizwa kwa sababu ya makosa."* Riddlebarger anafafanua, "Paulo hatupi sisi *sababu* kwamba ni kwa nini Mungu alitoa ile Sheria, 'kwa sababu ya makosa,' badala yake, Paulo anaweka wazi kwetu yale matokeo ya Mungu kutoa ile sheria kwetu, ikimaanisha kwamba 'ili kufanya makosa yawe yanatambulika kisheria.' Hili linamaanisha kwamba ile sheria haikuletwa kwetu ili kurekebisha hali yetu ya dhambi. Badala yake ile sheria ililetwa kwetu ili kuionyesha wazi hali yetu ya dhambi." (Riddlebarger 1998a: 4-5) Hili linaonyeshwa na Paulo kwa kutumia neno "iliingizwa."

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

Kwa maneno mengine, watu walikuwa tayari ni watenda dhambi hata babla ya sheria "kuingizwa," lakini ile sheria ilionyesha kwamba dhambi zetu zilikuwa hasa ni "makosa," m.y., uasi dhidi ya mapenzi matakatifu ya mamlaka ya Mungu mwenyewe.

Kisha Paulo anaonyesha hali ya kutojitosheleza ya ile Sheria ya Musa ikilinganishwa na ahadi iliyotolewa kwa Ibrahimu. Anafanya hivyo kwa njia tatu:

- Kwanza, anadokeza kwamba ile sheria ilikuwa ya muda tu. Ile Sheria ya Musa ingetenda kazi tu *"hata aje huyo mzao aliyepewa ile ahadi."* Ile "mbegu," bila shaka, alikuwa Kristo. Hili humaanisha kwamba wale ambao hujaribu kuwaweka Wakristo tena chini ya Sheria ya Musa kimsingi hawaelewi historia ya wokovu na mpango wa Mungu wa ukombozi. Ile hali ya muda ya ile Sheria ya Musa ni sehemu muhimu ya taswira ya historia ya ukombozi ambayo Paulo alianza kukazia katika **sura 2** na mwanzo wa **sura 3**.
- Pili, kutajwa kwa "mjumbe" katika **mst. 19-20** ni wazi humaanisha Musa (ona **Kut 20:19; 32:10-14; Kumb 5:5**). Swala hapa linaonekana ni kwamba "ile sheria ilitolewa kwa watu kwa njia isiyo ya moja kwa moja, bali kwa kupitia mjumbe wa katikati, badala ya kutoka kwa Mungu, tofauti na ile ahadi aliyopewa Ibrahimu. Hivyo, kwa mantiki hii, Paulo anaweza kusema kwamba ile sheria iko chini ikilinganishwa na ile ahadi." (Riddlebarger 1998a: 5) Zaidi ya hapo, "huyu mpatanishi anawakilisha wale watu kama walio na wajibu wa kuitetea ile Sheria. Hasimami kwa niaba ya Mungu (ambaye ni 'mmoja') bali kwa niaba ya wale watu (ambao ni 'wengi', mst. 20). Kwa sababu yeye ni mpatanishi wa agano kwa niaba ya wale wengi ('mbegu') agano hili haliko katika mstari mmoja na ile ahadi ambayo Ibrahimu alipewa kwa niaba ya yule mmoja ('mbegu'). Hivyo ile Sheria ni ya muda tu, ilianzishwa mpaka hapo ile mbegu moja itakapokuja (mst. 19b)." (Belleville 1986: 55-56)
- Tatu, ile sheria *haikuweza "kutia uzima"* (ona pia **2 Kor 3:6**); kama ile sheria ingaliweza kutia uzima, *"basi kwa hakika haki ingehesabiwa kwa njia ya sheria."* Hii ni dondoo muhimu, kwa Wayahudishaji wa nyakati za Paulo na kwa aina yoyote ya washika sheria sana wa leo. Ile Sheria ya Musa au sheria yoyote ile ya wanadamu, amri, au kanuni kazi yake ni kuwaambia watu kile wanachopaswa kufanya au kutofanya tu. Hata hivyo, sheria haiwapi watu uwezo wa kuitii ile sheria. Sheria haifanyi chochote kubadili zile tamaa mbaya za moyo ambazo kwazo dhambi hutokea (ona **Math 15:16-19; Marko 7:14-23**). Hakika, kama Paulo anavyodokeza katika **Rum 5:20** na **Rum 7:5, 8, 11** ya kuwa sheria kwa kweli huchochea hamu ya kutenda dhambi na hivyo huongezea makosa! Kwa hiyo, sheria haiwezi wala haiokoi watu.

Katika **mst. 21-22** Paulo anamalizia hiki kifungu kidogo ambacho alikianza katika **mst. 19**. Katika **mst. 21** anadokeza kwamba ile sheria haipingani na ahadi za Mungu. Badala yake, kama ilivyoonyeshwa katika **mst. 17-18**, Paulo anasema katika **mst. 21-22** ya kwamba lile kusudi na kazi ya ile sheria haikuwa kinyume bali ni tofauti na lile kusudi na kazi ya ile ahadi. Sheria ya Mungu, kama ilivyoandikwa katika maandiko, iliyafunua mapenzi yake. Kwa hivyo inaonyesha kwamba "waume kwa wake wote ni watoto wa Adamu, ambao mara kwa mara na kwa kuendelea, ikiwa kimawazo, maneno na matendo, kwa kukusudia, kwa uasi, na kwa mfululizo, hutenda kinyume na mapenzi ya Mungu aliyoyafunua, na kwa njia hiyo kufanywa mateka wa kifungo cha dhambi. Ile sheria hutufanya sisi sote 'wafungwa' wa dhambi." (Riddlebarger 1998a: 6; ona **Rum 3:9-20**) Kwa kuwa sisi sote tu watenda dhambi ambao hatuwezi kuikimbia hali yetu ya dhambi, sisi sote kwa haki kabisa tuko chini ya hukumu ya Mungu.

Ile hali ya tatizo la kibinadamu kuwa la kidunia (utumwa wetu na kifungo cha dhambi) huendana na ahadi ya ukombozi kuwa ni ya kidunia pia: *"makusudi hao waaminio wapewe ile ahadi kwa imani ya Yesu Kristo."* Kwa maneno mengine, kwa kuwa watu wote wako katika kifungo cha dhambi, kusudi moja la ile sheria ni kutufanya sisi kuona ile hali yetu ya dhambi na kushindwa kwetu kujiokoa. Tunapoona ya kuwa "hatuwezi kwenda mbinguni kwa misingi ya chochote kilichomo ndani yetu au kwa sababu ya chochote ambacho tumekifanya" (Riddlebarger 1998a: 8), hapo sasa kusudi la pili la ile sheria huja katika uwanja: ile sheria inatuonyesha kwamba, ili tuweze kufika mbinguni, tunahitaji kuangalia nje yetu—tunamhitaji mwokozi. Kwa kifupi, kufuatana na **mst. 22**, ile sheria hapo hutuelekeza kwenye utatuzi wa tatizo letu, ambayo ni, *"ile ahadi ya imani ndani Yesu Kristo."* Kushindwa kwetu kuitekeleza sheria na kushindwa kwa ile sheria yenyewe kutupa uzima hufanya ile ahadi ya imani ndani ya Yesu Kristo iwe si tu ya kutamanika bali pia ya lazima kabisa! Hii hali ya makusudi mawili ya ile sheria (m.y., kudhihirisha kifungo chetu cha dhambi na kule kutuelekeza kwenye njia yetu ya kuponea kwa njia ya imani katika Kristo) itufanye sisi "kuuhisi" ule uzito wa dhambi zetu na kutokuweza kwetu zaidi sana lakini, kwa wakati huo huo, tumuone Kristo na tumaini letu la wokovu kuwa tamu zaidi. Kuna maana ya kimatendo ya jambo hili katika mahusiano yetu na wengine, "ni pale tu ghadhabu ya Mungu na kisasi vinapokuwa vinaning'inia kwa uhalisia ulio mkali juu ya kichwa cha adui wa mtu ndipo kitu fulani kuhusu maana ya kuwapenda na kuwasamehe kinaweza kugusa mioyo yetu" (Bonhoeffer 1997: 157).

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

- **3:23-24—**Sheria ilikuwa mwangalizi aliyetuongoza kwa Kristo.

[23] Lakini kabla ya kuja ile imani tulikuwa tumewekwa chini ya sheria, tumefungwa mpaka ije ile imani itakayofunuliwa. [24] Hivyo torati imekuwa kiongozi kutuleta kwa Kristo, ili tuhesabiwe haki kwa imani.

Mistari hii miwili huweka mkazo juu ya kile ambacho kilishasemwa katika **mst. 19-22**, ambacho ni, ya kwamba ile sheria ilituweka sisi chini ya uangalizi na ilikuwa ya muda mpaka alipokuja Kristo (**mst. 23-24**). Tambua kwamba **mst. 23-24** kwa kurudia hutofautisha "ile sheria" na "imani." Paulo ameonyesha huu utofauti mara kwa mara katika **sura 3** yote. Kwa kuendelea kuonyesha kwamba "ile sheria" na "imani" hupingana zenyewe, anatuonyesha kwa wale Wayahudishaji (au dini nyingine ambayo ina misingi katika kutenda sheria) ni kinyume na ile asili hasa ya Ukristo wenyewe, ambao kwa huo wokovu na uhusiano wa mtu na Mungu hauna misingi katika ile sheria au matendo ya mtu lakini una misingi katika ile ahadi ya Mungu na hupokelewa kwa neema ya Mungu kwa njia ya imani peke yake.

Mistari hii huongezea maelezo muhimu kuhusiana na asili ya ile sheria, ambayo ni ya kwamba ile sheria ilikuwa "kiongozi" chetu (au "mwalimu wa shule" au "msimamizi" au alikuwa "mwangalizi" wetu). Lile neno "kiongozi" ("mwalimu wa shule"; "msimamizi"; "mwangalizi") kwa Kiyunani ni neno *paidagōgos.* Huyu *paidagōgos* "alikuwa mtumwa wa nyumbani, ambaye alikuwa na kazi ya kuangalia shughuli za watoto katika familia kuanzia wakati wa uchanga hadi kubalehe. . . Yeye pia aliwajibika kufundisha tabia njema na maadili mema. Hili jukumu la usimamizi ilihusisha kukemea na adhabu kwa makosa ya kitabia. . . . Mtoto alikuwa chini ya usimamizi wa *paidagōgos* wake katika masaa yake yote ya mchana. Hata hivyo, wakati atakapofika umri wa ukomavu aliachiliwa kutoka kwa *paidagōgoi* wake; hawakuendelea tena 'kumtawala'." (Belleville 1986: 59-60; ona pia Danker 2000: *paidagōgos,* 748).

Kutajwa kwa ile sheria kama *paidagōgos* mara nyingine hutilia mkazo ile taswira ya kihistoria-kiukombozi. Kama ilivyo kwa *paidagōgos* kule katika jamii ya Kigiriki-Kirumi, "Ile Sheria [ilituweka] sisi katika uangalizi ulioidhinishwa. Inazuia[med] katika uhuru wetu na kusimamia kila Nyanja ya maisha yetu. . . . Sisi [tulikuwa] 'chini ya' mamlaka yake. Ulikuwa ni usimamizi wa lazima kwa sababu sisi [tulikuwa] tumefungwa chini ya usimamizi wa madhara yanayoendelea ya dhambi." (Belleville 1986: 60) Kuwa *"chini ya paidagōgos"* (**Gal 3:25**) ni jambo linalokubaliana na kuwa sawa na kuwa *"chini ya sheria"* (**Rum 6:14-15; 1 Kor 9:20; Gal 3:23; 4:4-5, 21; 5:18**), *"chini ya mawakili na watunzaji"* (**Gal 4:1-2**), *"tukitumikishwa na kawaida za kwanza za dunia"* (**Gal 4:3**), na *"chini ya laana"* (**Gal 3:10**), kwa sababu sisi tulikuwa *"chini ya dhambi"* (**Gal 3:22**).

Hiyo ndiyo ilikuwa hali ya watu (hasa hasa, Israeli ya AK) kabla ya kuja kwa Yesu duniani. Israeli ilikuwa ni mtoto mdogo katika mpango wa Mungu wa wokovu na, kwa sababu ya hulka yake ya dhambi, lilihitaji usimamizi na uadibishwaji wa ile sheria na kuwaandaa kwa kuja kwa Masihi na mkombozi, Yesu Kristo. Katika maana ya kiujumla zaidi, hiyo ndiyo hali ya wanadamu wote ambao hawajafanywa upya ambao hutafuta kutegemea sheria zilizowekwa na wanadamu, amri, kanuni na matendo yao wenyewe ili kupata kibali cha Mungu. Kwa hiyo Paulo anageuza kipindi kipya-mabadiliko ya asili ya kuja kwa Kristo duniani katika sehemu ifuatayo.

- **3:25-4:7—**Ndani ya Kristo sisi si watumwa tena au watoto walio chini ya mwangalizi, lakini tumekombolewa, tumeasiliwa, wana na warithi wa Baba.

[25] Lakini iwapo imani imekuja, hatupo tena chini ya kiongozi. [26] Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa Mungu kwa njia ya imani katika Kristo Yesu. [27] Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo. [28] Hapana Myahudi wala Myunani. Hapana mtumwa wala huru. Hapana mtu mume wala mtu mke. Maana ninyi nyote mmekuwa mmoja katika Kristo. [29] Na kama ninyi ni wa Kristo, basi, mmekuwa uzao wa Ibrahimu, na warithi sawasawa na ahadi.
4 [1]Lakini nasema ya kuwa mrithi, wakati wote awapo mtoto, hana tofauti na mtumwa, angawa ni bwana wa yote; [2] bali yu chini ya mawakili na watunzaji, hata wakati uliokwaisha kuamriwa na baba. [3] Kadhalika na sisi, tulipokuwa watoto, tulikuwa tukitumikishwa na kawaida za kwanza za dunia. [4] Hata ulipowadia utimilifu wa wakati, Mungu alimtuma Mwanawe ambaye alizaliwa na mwanamke, amezaliwa chini ya sheria, [5] kusudi awakomboe hao waliokuwa chini ya sheria, ili sisi tupate kupokea hali ya kuwa wana. [6] Na kwa kuwa ninyi mmekuwa wana, Mungu alimtuma Roho wa Mwanawe mioyoni mwetu, aliaye, "Aba, yaani, Baba." [7] Kama ni hivyo, wewe si mtumwa tena bali u mwana; na kama u mwana, basi, u mrithi kwa Mungu.

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

Katika sehemu hii, Paulo anatangaza matokeo ya kuja kwa Kristo duniani yakihusianishwa na uhusiano wetu na sheria. Ndipo anaendelea kuelezea matokeo ya kuja kwa Kristo yakihusianishwa na uhusiano wetu na Mungu na watu wengine.

Mstari 25 unatoa tamko la maana sana, *"Lakini iwapo imani imekuja, hatupo tena chini ya kiongozi."* Kwa maneno mengine, "zile zama za walio wengi sasa zimekuja. Zile zama za sheria kama *paidagōgos* wakati wake umepita." (Belleville 1986: 60) Imani ina uwezo wa kufanya kile ambacho sheria kamwe haikuweza kufanya. Sababu ni kwamba Yule *msababishaji* wa imani yetu—Yesu Kristo—aliweza kufanya kwa ajili yetu kile ambacho hatukuweza kamwe kufanya kwa ajili yetu wenyewe. Yeye *"amezaliwa chini ya sheria"* (**Gal 4:4**), lakini yeye peke yake hakuwahi kutenda dhambi na kikamilifu aliitimiza ile sheria. Ndiyo maana kusudi kuu la ile sheria lilikuwa ni *"kutuleta kwa Kristo"* (**Gal 3:24**). Sisi hatuko tena *chini* ya sheria kwa sababu *hatuihitaji* ile sheria kutufuatilia kama msimamizi wetu. Ile sheria imetimilizwa na Bwana wetu wa kweli, mpya, ambaye kwake tumeunganishwa kwa imani (m.y., sasa sisi *"tumemvaa Kristo,"* **Gal 3:27**; *"ndani ya Kristo Yesu,"* **Gal 3:28**; *"ni wa Kristo,"* **Gal 3:29**). Kile alichokifanya Kristo ni kweli kuu ya kihistoria. Kwa hiyo, ile programu yote ya Wayahudishaji—kuwashawishi Wakristo, kwa matokeo, kuwaweka tena chini ya Sheria ya Musa kwa njia ya kutahiriwa na kufuata jadi nyinginezo za Kiyahudi zilizotakiwa na ile Sheria—si kwamba ni ujinga tu, kwa sababu zama zile ambazo jadi hizo zilitakiwa sasa zimepita, lakini pia hugeuza ile historia yote ya mpango wa wokovu na kusudi hasa la ile Sheria yenyewe!

Wakati ambapo **Gal 3:25** inatuonyesha sisi kwamba kuhesabiwa haki kwa njia ya imani ndani ya Kristo humaanisha kwamba sisi hatuko tena *"chini ya sheria"* bali tuko *"ndani ya Kristo,"* **Gal 3:26—4:7** inatupa matokeo manne yatokanayo na kuwa ndani ya Kristo maana yake kwa ajili yetu tukiwa na mahusiano na Mungu na watu wengine.

- <u>Kwanza, ndani ya Kristo sisi sote ni *"wana wa Mungu"* (**3:26-27; 4:5-7**).</u>[17] Katika muktadha huu, Paulo anatumia neno "sisi" **Gal 3:25** na "ninyi" katika **Gal 3:26-27** kimsingi anazungumzia Wayahudi na Mataifa. Riddlebarger anatoa mawazo, "Ni Yesu Kristo ambaye anawaunganisha Wayahudi na Mataifa kuwa mwili mmoja kwa njia ya imani peke yake. Lakini ni Wayahudishaji ambao badala yake hutafuta kuwagawa Wayahudi na Mataifa. Swala hili hutoa maelezo, kwa sehemu, kwa nini juhudi za wale Wayahudishaji za kutenganisha kile ambacho Mungu alikiunganisha pamoja katika mwili mmoja, zilionekana na yule mtume kuwa cha uharibifu mkubwa." (Riddlebarger 1998b: 1-2)

  Wito wa Paulo kwa wote walio ndani ya Kristo kuwa ni *"wana wa Mungu"* una matumizi sawa kwa wanawake kama ilivyo kwa wanaume; hakika, ina maana kipekee kwa wanawake. Sababu ni kwamba katika AK Israeli, ni wana peke yake ndio walipewa urithi wa mali za baba yao; mabinti wangeweza kurithi ikiwa tu baba alikufa bila kuwa na wana wowote (**Hes 27:1-11; Josh 17:3-6**). Sasa, ndani ya Kristo, wanawake wana hadhi sawa na wanaume kama *"watoto wa Mungu"* na wao ni *"warithi pamoja wa neema ya uzima"* (**1 Pet 3:7**). Katika **2 Kor 6:18** Paulo anatumia Agano la Daudi kwa kanisa. Katika mstari huu ananukuu **2 Sam 7:14**, mahali ambapo Mungu alitoa ahadi kwa kuhusiana na mwana wa Daudi Sulemani (*"Mimi nitakuwa baba yake, naye atakuwa mwanangu"*). Hata hivyo, Paulo anabadilisha maneno ya ile ahadi kuwa *"Nitakuwa Baba kwenu, nanyi mtakuwa kwangu wanangu wa <u>kiume na wa kike</u>."* Anafanya hivyo kuwekea mkazo ule usawa ambao watu wote—waume na wake—sasa wanao kama "wana" wa Mungu ndani ya Kristo.

  Gal 4:5 huelezea umuhimu mwingine wa swala hili wakati inapozungumzia kuhusu Yesu kutukomboa sisi *"ili sisi tupate kupokea hali ya kuwa wana."* Kuasili huzungumza kuhusiana na sisi kuingizwa katika familia ya Mungu. Hivyo, kuasili huenda mbele zaidi ya kuhesabiwa haki (wokovu). Kuhesabiwa haki kunahusiana na badiliko letu la hadhi ya "kisheria" mbele za Mungu, m.y., sisi ambao tulikuwa tumehukumiwa kama wenye dhambi sasa tunakuwa "hatuna hatia" kwa sababu Kristo alichukuwa hatia yetu na kulipa gharama kwa ajili ya dhambi yetu yeye mwenyewe. Kuasili nako kuna mlengo wa kisheria, m.y., sisi sasa tu wana familia wa familia mpya kisheria. Lakini kuasili huenda mbele zaidi ya hapo. Wakati ambapo kuhesabiwa haki hushughulika na Mungu katika nafasi yake kama hakimu, kuasili hushughulika na Mungu katika nafasi yake kama Baba. Lile wazo la familia, upendo, ukaribu, na upendano haya yote yanatupa maana nyingine ya dhana ya kuasili. Kama wana walioasiliwa na Mungu, "sisi ambao kwa asili tulikuwa wana wa ghadhabu na chini ya laana ya Mungu, si wa ahadi yake ya baraka, sasa tunaweza

[17] Paulo anautaja ubatizo katika **Gal 3:27** kwa sababu "ni katika ubatizo ndipo penye ishara ya kuingia katika kanisa la Kristo kwa kuwa ubatizo ni ishara inayoonekana na muhuri wa uhalisia wa kiroho usioonekana, ambao ni kufanywa upya na msamaha wa dhambi. . . . kwa hiyo, kwa njia ya imani kwa ile ahadi aliyoitoa Mungu kwa watu wake, ule ubatizo mmoja unapaswa kutambuliwa kuwa wa kuwafanya upya kana kwamba dhambi zao zimesamehewa." (Riddlebarger 1998b: 2) Au, kuisema kwa namna nyingine, imani *hutupatia* muunganiko wetu na Kristo; ubatizo *unauonyesha*.

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

kumsogelea Mungu katika ushirika wa karibu sana" (Ibid.: 7).

Ile dhana ya kuasili ndicho kiini cha Ukristo wenyewe. Hii ndiyo sababu nyingine ambayo iliufanya mjadala wa Paulo katika Wagalatia yote uwe wa fokasi ya kiukombozi-kihistoria. Hivyo, kuasili ndilo lengo la kule kutangulia kuchuguliwa (**Efe 1:5**). Ule utimilifu wa kazi ya Mungu ya ukombozi ndani ya Kristo unaonekana katika kuasili (**Gal 4:4-5**). Kiwango cha upendo wa Mungu (katika kuwabadili watumwa kuwa wana) kinaonekana katika kuasili (**Gal 4:6-7; 1 Yohana 3:1**). Ile huduma ya Roho Mtakatifu inadhihirisha kwa njia ya kuasili (**Rum 8:15**). Na kile kilele cha utimilifu wa mpango wa Mungu kwa ajili yetu hujadiliwa kwa namna ya kuasiliwa (**Rum 8:23**).

Kuna maana ya kimatendo kuhusiana na hili. Kutafakari kuhusiana na umuhimu kuwa kiini kwa kuasili—na hasa kwa Mungu kutuasili *sisi* katika familia yake—kutufanye sisi kuwa na shukrani sana, wenye kujitoa, na Wakristo waaminifu. Zaidi ya hapo, uaminifu wetu usiwe tu kwa shukrani zetu kwa kile ambacho Mungu ametufanyia, lakini tuyaishi maisha yetu ya uaminifu kwa ajili ya Baba yetu na kwa ajili ya faida ya familia yetu mpya tuliyoasiliwa.

- Pili, ndani ya Kristo sisi sote tu wamoja (**3:28**). Ile asili yenye nguvu ya Ukristo, ambayo inapasua theolojia yote ya Wayahudishaji, inasemwa katika **mst. 28**: *"Hapana Myahudi wa Myunani. Hapana mtumwa wala huru. Hapana mtu mume wala mtu mke. Maana ninyi nyote mmekuwa mmoja katika Kristo Yesu"* (ona pia **Kol 3:11**). Paulo anatamka kwa uwazi kabisa ya kuwa hakuna mipaka ya rangi, mbari kikabila, jinsi au kijamii-kiuchumi katika ufalme wa Kristo au vikwazo au matengano ndani ya ufalme wa Kristo. Katika Agano la Kale, Israeli walikuwa "watu waliochaguliwa" na Mungu" (**Kumb 7:6**). Chini ya Agano la Kale, Wayahudi na Mataifa walikuwa wamegawanyika. Ndani ya lile Hekalu la jengo ulikuwepo ukuta halisi unaotenganisha Wayahudi mbali na Mataifa. Pia kulikuwako na sehemu zinazowatenga wanawake na wanaume, makuhani na watu wa kawaida. Katika jipya, hekalu la kweli la kanisa, mgawanyiko kati ya Wayahudi na Mataifa umeondolewa. Kwa pamoja kama *"mtu mmoja mpya"* kanisa lina *"kua hata liwe hekalu takatifu katika Bwana"* (**Efe 2:11-22;** ona pia **Rum 3:22; Gal 2:11-14**). Ndani ya Kristo wote wako sawa, bila kujali jinsia, mazingira ya kuzaliwa, hali ya kiuchumi, lugha, au sifa nyinginezo za kimwili (**1 Kor 12:13; Gal 3:28; Kol 3:11; Ufu 5:9; 7:9**).

Hili liko sambamba na ukweli kwamba hakuna mipaka ya kijografia ndani ya ufalme wa Kristo. Kitabu cha Ufunuo kinadokeza kwamba Kristo amewanunua kwa damu yake wanaume na wanawake kutoka katika *"kila kabila na lugha na jamaa na taifa"* (**Ufu 5:9; 7:9**). Katika **Yohana 4:21, 23** Yesu alisema, *"saa inakuja ambayo hamtamwabudu Baba katika mlima huu, wala kule Yerusalemu.. . . . Lakini saa inakuja, nayo sasa ipo, ambayo waabuduo halisi watamwabudu Baba katika roho na kweli."* Yesu pia alisema, *"Kwa kuwa walipo wawili watatu wamekusanyika kwa jina langu, mimi nipo papo hapo katikati yao"* (**Math 18:20**). Ndani ya Kristo, watu hawana ulazima wa kwenda katika jengo (Hekalu au Hema ya kukutania) ili waweze kuwa karibu na Mungu; badala yake, Mungu amekuja kwa watu wake. Matokeo yake, sasa ndani ya Kristo kanisa *ndilo* Hekalu la Mungu (**1 Kor 3:9, 16-17; 2 Kor 6:16-7:1; Efe 2:21; 1 Pet 2:5; Ufu 3:12**; ona pia **Ufu 13:6** mahali ambapo kanisa linaitwa "Hekalu la Mungu").

Kanisa linapaswa kuwa ufalme wa duniani kote wenye usawa. Ndani ya Kristo tumeunganishwa na watu wote wa Mungu, wa zamani, sasa, na wa wakati ujao. Sisi tu sehemu ya familia kubwa na ufalme ambao haujui mipaka ya kijografia au kijamii. Hivi ndivyo ilivyo kwa kuwa kila mtu—bila kujali kundi la mbari, kabila, jinsi lugha au tofauti nyingineyo—yuko katika "mtumbwi huo huo": sisi sote tu wenye dhambi, tusioweza kujiokoa kwa chochote kile chetu au kwa chochote tunachofanya. Sisi sote kikamilifu kabisa tunaitegemea ile neema na rehema ya Yesu Kristo. Sisi sote lazima tukitegemee moja kwa moja kile alichokifanya kwa ajili yetu. Kwa hiyo, hatuwezi "kumdharau" au kumbagua mwingine ye yote aliye ndani ya Kristo. Jambo hilo, bila shaka, ilikuwa ndiyo sababu iliyomfanya Paulo amkabili Petro ana kwa ana katika **Gal 2:11-14**. Kama tulivyoona tulivyokijadili kifungu, swala hili huenda moja kwa moja kwenye kiini cha injili. Chakusikitisha, swala hili linaendelea kuwa tatizo kubwa kwa kanisa duniani kote hivi leo.

- Tatu, ndani ya Kristo sisi sote tu mbegu ya Ibrahimu (**3:29**). Mungu alikuwa amemwahidi Ibrahimu uzao au wazaliwa ("mbegu") *"kama mavumbi ya nchi"* (**Mwz 13:16**), au *"kama nyota za mbinguni, na kama mchanga wa ulioko pwani"* (**Mwz 22:17**; ona pia **Mwz 15:5**). Kile ambacho Paulo amekifanya katika **Wagalatia 3** yote ni kujaadili kwamba katika lile Agano la Ibrahimu, hatimaye ile "mbegu" ya kweli ya Ibrahimu ni ya rohoni (kutoka katika imani), sio katika mwili (kutoka katika uzao wa mwilini). Anadokeza jambo hilo hilo katika **Rum 4:11-18** mahali anaposema kwamba ile ahadi ya ibrahimu ilitolewa *"si kwa sheria bali kwa haki aliyohesabiwa kwa imani."* Anasema tena katika **Rum 9:6-8** anaposema kwamba *"maana hawawi wote Waisraeli walio wa uzao wa Israeli,"* na *"si watoto wa mwili walio watoto wa Mungu, bali watoto wa ile ahadi wanahesabiwa kuwa wazao ['mbegu']."* Ndiyo maana Paulo alishakuwa

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

na mtazamo wa kiukombozi-kihistoria: amekuwa akitilia mkazo kwamba lile Agano na Ibrahimu—ambalo lilitokea kwa makisio mwaka 1400 KK—lilikwenda mbali zaidi ya Ibrahimu, Isaka, na Israeli. Siku zote lilikuwa linae Yesu Kristo katika nia yake na sisi ambao tumeunganishwa na Kristo kwa imani—*"kutoka kila kabila na lugha na jamaa na taifa"* duniani (**Ufu 5:9; 7:9**). Ndio maana lile Agano la Ibrahimu linaweza kutazamwa kama uti wa mgongo wa kitheolojia wa Biblia yote.

- Nne, ndani ya Kristo sisi sote tu warithi kutokana na ile ahadi (**3:29; 4:7**). Kwa kuwa Kristo ndiye mbegu halisi ya Ibrahimu (**Gal 3:16**), wale wote walio ndani ya Kristo wao pia ni mbegu halisi ya Ibrahimu na warithi wa zile Baraka za ahadi ya Ibrahimu (**Gal 3:29**; ona pia **Gal 3:18**). Kama alivyofanya katika **Gal 3:24-25** kuhusiana na yule *paidagōgos,* katika **Gal 4:1-7** Paulo anajadili ile hadhi yetu kama "warithi" katika mtazamo wa jadi za Kiyunani-Kirumi. Chini ya sheria ya kirumi, aliye mtoto, "ingawaje kinadharia ndiye mmiliki wa kisheria wa urithi, alizuiwa katika kile kipindi cha utoto wake asisimamie ule urithi. . . . Wakati yule mtoto yuko 'chini ya watunzaji na mawakili' yeye, kama mtumwa, hana uwezo wa kujitambulisha na kuonyesha uwezo wake." (Belleville 1986: 62-63) Katika **Gal 4:3** kule kutajwa kwa *"kawaida za kwanza za dunia"* hudokeza "ile hali ya kuweka kanuni na vidhibiti ambavyo huchukuwa nafasi ya jitihada za binafsi lakini, kama vile ile Sheria, hazina uwezo wa kutia uzima (cf. 3.21)." (Ibid.: 68) Au, kama Riddlebarger anavyoiweka, "zile 'kanuni za msingi' za dunia . . . ni wazo kwamba tunaweza kutangazwa kuwa wenye haki mbele za Mungu kwa misingi ya matendo yetu au thawabu tuzipatazo kwa njia ya kuitii sheria" (Riddlebarger 1998b: 5). Mataifa huziinua hizi amri, kanuni, za nje na mawazo kwa "miungu" hata kama wao "si miungu" (ona **Gal 4:8**), kama vile Wayahudi wanavyoiinua ile Sheria ya Musa kuwa Mungu.

Sasa hali iko tofauti kabisa. Tumeona kuwa ile sheria haikuweza kabisa kutia uzima na ilikuwa ni kiongozi wa muda tu mpaka alipokuja Kristo. Tunampokea Kristo—na yeye hutupatia haki ndani yetu—kwa imani. Lakini Kristo alijua kwamba hata imani peke yake haitupi sisi nguvu ya kubadilika ambayo tunaihitaji ili tuweza kuishi maisha matakatifu. Kwa hiyo, aliwaambia wanafunzi kungoja ili wapokee ile *"nguvu akiisha kuwajilia juu yao Roho Mtakatifu"* (**Matendo 1:8**). Roho Mtakatifu alipokuwa akimiminwa siku ile ya Pentekoste, "ukombozi wetu kutoka katika utumwa" kwa hakika ukakamilika. Ile Sheria ya AK ilikuwa ya nje, imeandikwa kwenye vipande vya mawe. Sasa, kama **Gal 4:6** inavyosema, *"Mungu alimtuma Roho wa Mwanawe mioyoni mwetu."* Roho Mtakatifu anaishi ndani yetu (**Ezek 36:26-27; Yohana 14:16-17**), sheria ya Kristo imeandikwa mioyoni mwetu (**Yer 31:33; Ebr 8:10**), na sisi wenyewe tu *"barua ya Kristo . . . iliyoandikwa si kwa wino, bali kwa Roho wa Mungu aliye hai; si katika vibao vya mawe, ila katika vibao ambavyo ni mioyo ya nyama"* (**2 Kor 3:3**). Kwa hiyo, "Kama zile kanuni za kawaida za dunia, [pamoja] na kuja kwa imani ndani ya Kristo, kazi ya ile sheria kama mlezi na mlinzi inakoma na Roho Mtakatifu anakuwa ndiye kanuni iongozayo ya ndani." (Belleville 1986: 70)

Kristo ameleta badiliko kubwa sana kiukombozi-kihistoria duniani: watu wamewekwa huru mbali na utumwa wa dhambi, ile sheria, na kwa vile vitu vya asili vya dunia vinavyotawala; ndani ya Kristo watu si watoto tena, bali watu wazima; na waume kwa wake wa kila kabila na lugha na taifa wameasiliwa na kuungana wakiwa washiriki sawa ndani ya familia moja kubwa na ufalme kama wana na warithi wa Mungu. Na bado Kristo amefanya hata zaidi ya hayo. **Gal 4:6** inasema kwamba Mungu amemtuma Roho ndani ya mioyo yetu, *"aliaye, Aba, yaani, Baba.'"* Lile neno la Kiaramaiki "Abba" ni neno linaloonyesha upendo wa ukaribu, wa kibinafsi. Richard Bauckham anasema, "Ule utambulisho wa namna ya kipekee huonyesha kwamba "lile kanisa la kale lilijua kwamba katika namna hii ya utambulisho kwa Mungu lilikuwa na marupurupu ya kipekee ambayo wanawiwa na Yesu. Kwa mujibu wa hayo ni uhusiano wake Yesu na Mungu kama Abba ambao aliwashirikisha wanafunzi wake: uwana wao ulitokana na uwana wa kwake." (Bauckham 1978: 249) Matokeo yake, *"Tuna ujasiri wa kupaingia patakatifu kwa damu ya Yesu"* (**Ebr 10:19**). Hakuna dini nyingine au mtazamo wa kidunia ambao watu wanakuwa na ukaribu wa kibinafsi na Mungu mkuu kama ule ambao Yesu anatupa sisi. Kwa sababu ya kwamba Yesu ni nani na kile alichokifanya, sasa hakuna vikwazo kati ya sisi na watu wengine au kati ya sisi na Mungu mwenyewe. Kwa kuyajua hayo, kujaribu kuweka "vikwazo" kama vile matakwa ya ile sheria au yale "ya kawaida za kwanza za dunia" si tu kwenda mwelekeo usio sahihi bali pia unakufuru dhidi ya nafsi na kazi ya Kristo.

- **4:8-20—**Akiwasihi Wagalatia.

Paulo ndio amemaliza ile sehemu ambayo ndicho kiini cha kitabu hiki ambayo imeangalia upeo wote wa historia ya ukombozi. Ameonyesha ya kuwa ndani ya Kristo sisi si watumwa au watoto ambao tumefungwa chini ya Sheria ya Musa au "mambo ya kawaida ya dunia" lakini tunakombolewa, tunaasiliwa, tu wana na warithi wa Baba. Hata hivyo, anashughulika na watu (wale Wayahudishaji) ambao walitaka kuwashawishi

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

Wakristo warudi nyuma. Kwa hiyo, yeye sasa anatoa nasaha mbili kwa Wagalatia ili kuwasaidia kuliona kosa la kile wanachoagizwa kufanya. Ikiwa tunaelewa lile swala la msingi—ya kuwa injili iko kinyume kabisa na dini nyingine za duniani—tutaona kwamba nasaha za Paulo zina mantiki kwetu sisi leo kama ambavyo zilikuwa kwa wale Wagalatia, hata kama zile changamoto bayana za injili siku za leo zaweza kuwa ni tofauti zikilinganishwa na kile ambacho wale Wayahudishaji walikuwa wakikisema kwamba Wagalatia walipaswa kufanya.

- **4:8-11—**Ombi kwa mujibu wa hadhi yao katika Kristo.

  [8] Lakini wakati ule, kwa kuwa hamkumjua Mungu, mliwatumikia wao ambao kwa asili si miungu. [9] Bali sasa mkiisha kumjua Mungu, au zaidi kujulikana na Mungu, kwa nini kuyarejea tena mafundisho ya kwanza yaliyo manyonge, yenye upungufu, ambayo mnataka kuyatumikia tena? [10] Mnashika siku, na miezi, na nyakati, na miaka. [11] Nachelea, isiwe labda nimejitaabisha bure kwa ajili yenu.

Kabla ya kumjia Kristo, Wagalatia walikuwa wapagani. Kama ilivyokuwa *"hawakumjua Mungu"* (**Gal 4:8**). Paulo anadokeza vivyo hivyo katika **Efe 2:12** anaposema, *"kwamba zamani zile mlikuwa hamna Kristo, mmefarakana na jamii ya Israeli, wageni wasio na maagano ya ahadi ile. Mlikuwa hamna tumaini, hamna Mungu duniani."* Kama ilivyokuwa, wale Wagalatia walikuwa kama mtu mwingine ye yote wa duniani asiye Mkristo: *"kwa sababu, walipomjua Mungu hawakumtukuza kama ndiye Mungu wala kumshukuru; bali walipotea katika uzushi wao, na mioyo yao yenye ujinga ikatiwa giza. . . . Kwa maana waliibadili kweli ya Mungu kuwa uongo, wakakisujudia kiumbe na kukiabudu badala ya Muumba anayehimidiwa milele."* (**Rum 1:21, 25**) Walifuata mila za dini za kipagani na kuzisherehekea "sikumaalumu au takatifu" za kipagani. Wakati ambapo yale matendo bayana ya kidini ya wale Wagalatia yanaweza kuwa tofauti mbali na yale matendo ya kidini ya wasio Wakrisro wa siku za leo, hakuna tofauti *katika namna* ya kuisujudia miungu ya kipagani ya siku za kale dhidi ya kufunga katika mwezi wa Ramadhani au kujaribu kuupata upendeleo wa Mungu kwa kuwa "mtu mwema au kufanya matendo mema." Matendo yote ya namna hii hayana faida kiroho.

Katika **Gal 4:3** Paulo alishasema kwamba *"tulipokuwa watoto, tulikuwa tukitumikishwa na kawaida za kwanza za dunia."* Sasa katika **mst. 8** anadokeza kwamba zile *"kawaida za kwanza"* ambazo zilitutumikisha *"kwa asili si miungu."* Katika **mst. 9** anaendelea kusema kwamba zile *"kawaida za kwanza"* ambazo zilitutumikisha ni *"yaliyo manyonge, yenye upungufu."* Riddlebarger anadokeza, "Ule ushahidi kwamba "zile kanuni za msingi za dunia" ilikuwa ikimaanisha matendo-haki, ni ukweli kwamba pale tu ambapo wale Wagalatia wangerudi kwenye zile "kanuni za msingi," moja kwa moja, hali ya kushika sana sheria, imeinua kichwa chake kibaya. Jambo hili linaonekana wazi kwa ule ukweli kwamba hawa walimu wa uongo walikuwa wakiwataka wale waongofu wao washike siku za sherehe na sheria za vyakula pamoja na kukubaliana na tohara kama njia ya kupata au pengine kuendelea kuwa na hali ya kuhesabiwa haki mbele za Mungu." (Riddlebarger 1998c: 3)

Wale Wagalatia walikuwa wameachana na mila zao za kipagani kwa ajili ya Ukristo. Hata hivyo, wale Wayahudishaji walitaka kuleta kaida na jadi za dini ya Kiyahudi ndani ya kanisa. Hoja ya Paulo katika **mst. 9-10** ni kwamba kushika kaida za Kiyahudi kama vile kutahiriwa, sheria za vyakula, na zile *"siku, na miezi, na nyakati na miaka"* maalumu ya Wayahudishaji *viko katika daraja moja* kama kuabudu sanamu za kipagani au kujaribu kuifurahisha miungu ya milimani, kwenye mito, na kwenye miti. Kama alivyosema katika **Kol 2:16-17**, *"Basi, mtu asiwahukumu ninyi katika vyakula au vinywaji, au kwa sababu ya sikukuu au mwandamo wa mwezi, au sabato—mambo hayo ni kivuli cha mambo yajayo; bali mwili ni wa Kristo"* (ona pia **Marko 7:14-23; Matendo 10:9-16; Rum 14:1-17; 1 Kor 8:1-9:4; 10:23-30; 1 Tim 4:3-5; Ebr 9:9-10**). Kwa kiwango kikubwa, *uhuru* wetu ndani ya Kristo ni *uhuru wetu kutoka* katika vifungo vya kushika sheria vya namna hiyo (mambo ambayo yapo katika dini nyingine zote).

Kiini cha hoja ya Paulo na rai yake ni kwamba *"sasa mkiisha kumjua Mungu, au zaidi kujulikana na Mungu, kwa nini kurejea tena [kwenye taratibu na vitu ambavyo haviwezi kuwapeni uzima bali huwatumikisha tu]?"* Jambo hili *siku zote* ni changamoto kwa Wakristo. Wakati Wakristo wengi wanaposikia neno "kurudi nyuma," wanafikiria kuanguka katika dhambi fulani mahsusi. Kule kurudi nyuma ambako Paulo anakujadili hapa ni kwa umuhimu sana kuliko Wakristo kutenda dhambi fulani. Ni "kurudi nyuma kitheolojia au kiroho." Hilo swala linahusu kurudi katika aina fulani ya mfumo wa "matendo ya haki," m.y., mtazamo au matendo ya kidini ambayo kwayo tunafikiri tunaweza kutendea kazi au kuutunza upendeleo wa Mungu kwa kufanya matendo fulani ya kijadi badala ya au zaidi ya kukitegeme kikamilifu kile ambacho Kristo amekifanya kwa ajili yetu. Twahitajika kuelewa kwamba aina hii ya fikra ndio ile "namna ya kushindwa" ya watu wote, pamoja na Wakristo. Ndio maana siku zote hii ni hatari ambayo tunapaswa tuifahamu.

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

Katika kushughulika na hili, tunahitaji kukumbuka kile David Powlison anachokiita lile "swali lililo la msingi kuliko yote ambalo Mungu wakati wote anauuliza moyo wa kila mtu," ambalo ni, "Je kuna mtu fulani au kitu fulani mbali na Yesu aliye Kristo ambacho kimechukuwa nafasi ya kutegemea kwako, kukushughulisha, kuamini, utumishi, hofu na furaha? Ni suala linaloegemea katika kile kisababisho cha haraka cha tabia, mawazo, na hisia za mtu. Katika mawazo ya ki-Biblia, suala kisababisho ni suala la ubwana. Nani au nini 'kinatawala' tabia yako, Bwana au kilicho badala yake?" (Powlison 1995: 35) Kwa maneno mengine, sisi tunahitajika tuendelee kujiuliza, "Ni nani aliye Bwana wangu wa kweli *kiutendaji*?" "Ni *kwa nini* ninafanya kile ninachokifanya?" na "Je wokovu wangu unategemea nini *kiukweli na kiutendaji*?"

Tatizo tulilonalo sisi sote hatimaye ni la kitheolojia. Fokasi ya mtazamo wetu inazungukia kwetu sisi wenyewe. Hilo bila kujizuia inatupelekea sisi kujiangalia wenyewe na kile tunachofanya kama msingi wa kupata na kuendelea kuwa na upendeleo wa Mungu, badala ya kufokasi kwa Kristo. Hapa tena, swala linakwenda kwenye kiini cha injili: "Injili inasema, 'Mungu anakukubali wewe kama vile alivyo Kristo. Mungu ana upendo "usio na masharti" kwa ajili yako.' Kristo anaichukuwa laana ambayo ulipaswa kuchukuwa wewe. Kristo anampendeza Baba kikamilifu na anakupa wewe ule wema wake mkamilifu. Kristo anatawala kwa nguvu, akikufanya wewe mtoto wa Baba na anakuja karibu na wewe na kuanza kubadilisha kile ambacho hakikubaliki kwa Mungu kuhusu wewe. Mungu hanikubali mimi 'kama nilivyo.' Ananikubali mimi 'kama nilivyo ndani ya Yesu Kristo.' Kile kiini cha mvutano ni tofauti. Injili ya kweli hairuhusu upendo wa Mungu kunyonywa na hekaheka za tamaa ya nafsi kutaka kukubaliwa na kustahili katika na ndani yake. Badala yake, inawafanya watu wasijione wao kuwa ni kiini—kile ambacho Biblia hukiita "kumcha Bwana' na "imani"—kuangalia nje ya wao." (Ibid.: 49)

Hiyo ndiyo asili ya ombi la Paulo katika **mst. 8-11**. Tumekuja kumjua Mungu kwa njia ya Yesu Kristo; sisi si watumwa tena au watoto waliofungwa na Sheria au Musa au "mambo ya kawaida ya dunia" lakini tumekombolewa, tumeasiliwa, watoto wakomavu na warithi wa Baba. Kwa mujibu wa hayo, twawezaje tena kurudi katika mtazamo na matendo ambayo hutufunga sisi kama watoto na watumwa? Kufanya hivyo kimsingi kunakana kile ambacho Kristo amekifanya na ile nafasi yetu tuliyonayo ndani ya Kristo. Swala hilo hutukabili sisi sote, kama watu binafsi na kama makanisa.

- **4:12-20—**Ombi kwa mujibu wa mahusiano binafsi.

> ***[12] Nduguzangu, nawasihi, iweni kama mimi, maana mimi ni kama ninyi. Hamkunidhulumu kwa lo lote. [13] Lakini mwajua ya kuwa naliwahubiri Injili mara ya kwanza kwa sababu ya udhaifu wa mwili; [14] na jaribu lililowapata katika mwili wangu hamkulidharau wala kulikataa, bali mlinipokea kama malaika wa Mungu, kama Kristo Yesu. [15] Ku wapi, basi, kule kujiita heri? Maana nawashuhudu kwamba, kama ingaliwezekana, mngaling'oa macho yenu, mkanipa mimi. [16] Je! nimekuwa adui wenu kwa sababu nawaambia yaliyo kweli? [17] Hao wana shauku nanyi, lakini si kwa njia nzuri, bali wanataka kuwafungia nje, ili kwamba ninyi mwaonee wao shauku. [18] Navyo ni vizuri kuonewa shauku katika neno jema siku zote, wala si wakati nikiwapo mimi pamoja nanyi tu. [19] Vitoto vyangu, ambao kwamba nawaonea utungu tena mpaka Kristo aumbike ndani yenu; [20] laiti ningekuwapo pamoja nanyi sasa, na kuigeuza sauti yangu! Maana naona shaka kwa ajili yenu.***

Paulo sasa anawasihi Wagalatia kwa misingi ya mahusiano yake na wao. Paulo anazungumzia udhaifu wake wa mwili katika **mst. 13**. Katika **mst. 15** anasema ya kwamba wale Wagalatia *"wangaling'oa macho yao, wakampa yeye."* Jambo hilo huonyesha kwamba udhaifu wake wa mwili lilikuwa tatizo ambalo lilihusu macho yake (ambalo linaweza kuwa *"mwiba katika mwili"* wa Paulo ambao unatajwa katika **2 Kor 12:7-10**). Licha ya matatizo ya kimwili ya Paulo, ambayo yalikuwa "alama" kwa wale Wagalatia (**mst. 14**), wali- *"mpokea kama malaika wa Mungu, kama Kristo Yesu."* Hivyo, Paulo alikuwa na uhusiano wa karibu na Wagalatia ambao aliwasihi. Bado anawaita wao kwa kusema *"vitoto vyangu"* (**mst. 19**).

Hata hivyo, huu uhusiano wao wa karibu uliathiriwa vikali na wale Wayahudishaji (**mst. 16**). "Kinyume na vile ambavyo waliipokea injili kutoka kwa Paulo alipowahubiria kwa mara ya kwanza, Wagalatia walikoseshwa amani na ile kweli, kwa kuwa ile kweli ingewalazimisha kukubali kuwa walikuwa wamekosea na kama wangeikubali injili ya Paulo wangelazimika kuwaondoa wale Wayahudishaji miongoni mwao. Kwa kuwa Paulo alikuwa akiwakabili wao na kweli hii, inavyoonekana, baadhi yao ni wale ambao walikuwa na uhusiano wa karibu sana na Paulo, sasa walimwona kama adui." (Riddlebarger 1998c: 5) Hapa kuna somo kwa ajili yetu katika hili. Hatuwezi kiurahisi "kuijadili" injili ndani ya mtu. Badala yake tunapaswa kujaribu kujenga uhusiano wa karibu na watu ili kuwezesha ushuhuda wetu kwao. Hata hivyo, ni lazima tukumbuke kwamba jambo lililo

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

muhimu sio ule uhusiano bali ile kweli ya injili. Ni lazima wakati wote "tuseme kweli kwa upendo" (**Efe 4:15**) hata kama uhusiano wetu wa karibu utaathiriwa na ile kweli.

Kifungu hiki kidogo kinatupa dondoo nyingine. Katika **mst. 12** Paulo anasihi wale Wagalatia *"iweni kama mimi, maana mimi ni kama ninyi."* Hili liko sambamba na namna alivyowachukulia watu alivyosema katika **1 Kor 9:20-22** (*"Nalikuwa kama Myahudi kwa Wayahudi, ili niwapate Wayahudi . . . kwa wale wasio na sheria, nalikuwa kama sina sheria . . . kwa wanyonge nalikuwa mnyonge, ili niwapate wanyonge. Nimekuwa hali zote kwa watu wote, ili kwa njia zote nipate kuwaokoa watu"*). Aliifafanua kanuni hii katika **1 Kor 8:13**, *"Kwa hiyo chakula kikimkwaza ndugu yangu, hakika sitakula nyama hata milele, nisije nikamkwaza ndugu yangu."* Dokezo la kuwa kama wengine ni ili tuweze kujenga uhusiano na wao. Tunapojenga uhusiano na watu huruma yetu, upendo na mafundisho yapaswa viwalete kwa Kristo.

Kuwa *"kama mimi nilivyo"* inamaanisha kwamba maisha yetu yanapaswa kumuakisi Kristo kiukweli. Sisi sote tunapaswa kusema pamoja na Paulo *"mnifuate mimi, kama mimi ninavyonfuata Kristo"* (**1 Kor 11:**1; ona pia **1 Kor 4:16; Filp 3:17**). Ndio maana Paulo aliwaambia wale Wagalatia katika **mst. 19**, *"ambao kwamba nawaonea utungu tena mpaka Kristo aumbike ndani yenu."* Hatimaye, hilo ndilo lengo la maisha yetu, ya kwamba sisi *"tufananishwe na mfano"* wake Yesu Kristo (**Rum 8:29**). Ku-"fananishwa na mfano wa Kristo" inamaanisha kwamba tunafikiri kama Kristo alivyofikiri na kutenda kama alivyotenda; vile anavyovithamanisha vinakuwa ndivyo na sisi tunavyovithamanisha na anavyovipa kipaumbele vinakuwa kipaumbele na kwetu sisi. Swala hili linahusisha kila nyanja ya maisha yetu. Ili hili liweze kutokea, Kristo lazima awe fokasi iliyomuhimu kuliko zote katika maisha yetu. Tunatakiwa kuwa watu wa Neno, ili kwamba tujue vile ambavyo Mungu anavithamanisha, anavyovipa kipaumbele, na mapenzi kwa undani na kwa ukaribu sana. Huu ni mchakato wa utakaso. Ni mchakato ambao unaendelea maisha yetu yote. Lakini matokeo yatakuwa kwamba watu watakapotuona, na kuzungumza, na kuwa na maingiliano na sisi, watakuwa wamemwona na kuzungumza na kuwa na maingiliano na Kristo akitenda kwa kupitia sisi. Hakuna wito ulio mkuu zaidi katika maisha kuliko huu.

- **4:21-31—** Muhtasari: Utofautishaji wa sheria/ahadi yote uko kwa muhtasari kwa njia ya mfano ndani ya Hajiri (Ishmaili) na Sara (Isaka); kwa kushangaza, Israeli ni Ishmaili na Wakristo ni Isaka!

  [21] Niambieni, ninyi mnaotaka kuwa chini ya sheria, je! hamwisikii sheria? [22] Kwa maana imeandikwa ya kuwa, Ibrahimu alikuwa na wana wawili mmoja kwa mjakazi, na mmoja kwa mwungwana. [23] Lakini yule wa mjakazi alizaliwa kwa mwili, yule wa mwungwana kwa ahadi. [24] Mambo haya husemwa kwa mfano; kwa maana hawa ndio kama maagano mawili, moja kutoka mlima Sinai, lizaalo kwa utumwa, ambalo ni Hajiri. [25] Maana Hajiri ni kama mlima Sinai ulioko Arabuni, umelingana na Yerusalemu wa sasa; kwa kuwa anatumikia pamoja na watoto. [26] Bali Yerusalemu wa juu ni mwungwana, naye ndiye mama yetu sisi. [27] Kwa maana imeandikwa,
  "FURAHI, WEWE ULIYE TASA, USIYEZAA;
  PAZA SAUTI, ULIE, WEWE USIYE NA UTUNGU;
  MAANA WATOTO WAKE ALIYEACHWA PEKEE NI WENGI
  KULIKO WA HUYO ALIYE NA MUME."
  [28] Basi, ndugu zangu kama Isaka sisi tu watoto wa ahadi. [29] Lakini kama vile siku zile yule aliyezaliwa kwa mwili alivyomwudhi yule aliyezaliwa kwa Roho, ndivyo ilivyo na sasa. [30] Lakini lasemaje andiko? "MFUKUZE MJAKAZI NA MWANAWE, KWA MAANA MWANA WA MJAKAZI HATARITHI KABISA PAMOJA NA MWANA WA MWUNGWANA."
  [31] Ndiposa, ndugu zangu, sisi si watoto wa mjakazi, bali tu watoto wa huyo aliye mwungwana.

  Paulo anahitimisha mjadala wote kuhusiana na ile sheria na ile ahadi kwa kurudi tena kwa Ibrahimu na kuipitia historia ya ukombozi. Sasa, hata hivyo, anaiangalia ile sheria na ile ahadi ki-taipolojia.

  Katika **mst. 21-23** anaanza kwa kutambua kuwa Ibrahimu alikuwa na wana wawili: Ishmaili kwa Hajiri (mwanamke mtumwa) na Isaka kwa Sara (mwanamke aliye huru). Anaongezea kwamba Ishmaili alizaliwa kwa mwili (ona **Mwz 16:1-15**), lakini Isaka alizaliwa kwa ahadi ya Mungu na kinyume kabisa na uwezo wa mwili (ona **Mwz 17:15-19; 18:1, 10-14; 21:1-3**). Katika **mst. 24-28** Kisha Paulo anaitoa hoja yake kiistiari au kitaipolojia. Anasema kwamba Hajiri na Sara wanawakilisha maagano mawili. Hajiri anafananishwa kwa dhahiri kabisa na Agano la Musa (lile agano la sheria) kutoka Mlima Sinai; anahusiana na mambo ya mwilini, Yerusalemu ya duniani, na watoto wake wako utumwani (**mst. 24-25**). Kwa kuzingatia hoja za Paulo za awali katika **sura 3** na sehemu ya kwanza ya **sura 4**, wale watoto walio katika utumwa watakuwa ni wale Wayahudishaji ambao bado wamefungwa na sheria. Lile agano ambalo Sara analiwakilisha halitajwi bayana

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

(wala Sara mwenyewe hatajwi), lakini ni wazi yuko katika hilo agano la neema ya Mungu na ahadi yake ambayo misingi yake ni imani (ona **Gal 3:17**). Paulo anatofautisha bayana ile *"Yerusalemu ya sasa"* na utumwa wake wa sheria na *"ile Yerusalemu ya juu [ambayo] iko huru"* na anaongezea kwamba *"yeye ndiye mama yetu"* (**mst. 26**). Katika **mst. 28** anahitimisha huo ulinganishaji kwa kusema, *"Basi ndugu zangu [m.y., wale Wakristo Mataifa wa Galatia], kama Isaka, mu watoto wa ahadi"* (ona pia **mst. 31**). Kwa kuzingatia hoja ambazo Paulo ametoa katika **sura 3-4** zote, agano la pili linalowakilishwa na mwanamke aliye huru litakuwa ni lile Agano la Ibrahimu. Hata hivyo, hoja ya Paulo ni kwamba lile Agano la Ibrahimu linapata kutimizwa kwake ndani ya Kristo; hivyo, kutimilika kwa kweli kwa ahadi kwa Ibrahimu ni lile Agano Jipya, ambalo lilitabiriwa na Yeremia (**Yer 31:31-34**) na kuanzishwa na Yesu (**Luka 22:20**).

Utofautishaji wa Paulo wa *"ile Yerusalemu ya sasa [ya kimwili]"* (**mst. 25**) dhidi ya *"ile Yerusalemu ya juu"* (**mst. 26**) huonyesha kwamba lile Agano jipya ndilo ambalo Paulo analolimaanisha. Manabii walishatabiri kuhusiana na urejesho wa Israeli na Yerusalemu chini ya uongozi wa mfalme aliyepakwa mafuta na Mungu, ambaye atatawala kutoka Yerusalemu au Mlima Sayuni (mfano, **Isaya 60-62, 66; Yeremia 30-33; Ezekieli 34-37**). Ingawaje watu walikuwa wamerudi kutoka uhamishoni kule Babeli mnamo miaka 500 kabla ya Yesu, "wale watu walirudi katika mantiki ya kijografia, lakini ule unabii mkubwa wa urejesho haukuwa umetimia" (Wright 1996: 126). Ile dhamira ya urejesho wa Israeli na Yerusalemu ilichukuliwa hadi katika AJ, lakini waandishi wa AJ wanaitumia dhana ya urejesho kwenye *urejesho wa kiroho wa Yerusalemu mpya au ya mbinguni* kwa njia ya Yesu. Tunaliona hili katika ukweli kwamba **Gal 4:26** inazungumzia kuhusu *"Yerusalemu wa juu."* **Gal 4:27** kisha anaanza na neno "kwa maana" (Kiyunani = *gar*) na ananukuu **Isa 54:1** ambayo katika muktadha wa AK ulizungumzia kuhusu Yerusalemu kama iliyotekwa na maadui zake na kuwa mateka, ndipo ije kurejeshwa na Mungu. Kwa maneno mengine, Paulo anachukuwa andiko la AK kuwa ni Yerusalemu ya mwilini lakini anasema kwamba utimilifu wa kweli wa mstari huu ni wa rohoni, katika ile "Yerusalemu wa juu" na wazaliwa wake walio huru "wana wa ahadi."[18]

Hivyo ndivyo hasa AJ yote huitazama Yerusalemu. Unabii wote wa urejesho umetimilizwa *ndani ya Yesu* (**Luka 1:68; 2:36-38**). Sayuni mpya (ile Yerusalemu na Israeli iliyorejeshwa) haihusianishwi na mahali au ile Sheria ya Musa lakini na Kristo na watu wake. Kwa hivyo, **Ebr 12:18, 22** inasema kwamba ndani ya Kristo *"hatukufikilia mlima uwezao kuguswa . . . bali sisi tumeufikilia mlima Sayuni, na mji wa Mungu aliye hai, Yerusalemu wa mbinguni [m.y., ile Yerusalemu ya juu]."* Zaidi ya hapo, wakati Agano la Kale lilipokuwa bado linatumika, hata wakati ule wa huduma ya Yesu' duniani Yerusalemu iliitwa "mji mtakatifu" (**Isa 48:2; Dan 9:24; Neh 11:1, 18; Math 4:4; 27:53**). Hata hivyo, "baada ya kipindi kile, ule mtajo 'mji mtakatifu' hauonekani tena, kwa kuwa Mungu hakai tena kule Yerusalemu bali ndani ya kanisa; na siku ile ya Pentekoste Roho Mtakatifu hakulijaza hekalu au Yerusalemu lakini wale mitume na wale wote waliotubu na wakabatizwa (Matendo 2:1-4, 38-39). Ufafanuzi huu unathibitishwa katika Ufunuo ambapo Yohana anaielezea Yerusalemu mpya kama mji mtakatifu (21:2, 10; 22:19). Anaelezea kwamba hii ni 'ile kambi ya watakatifu na ule mji upendwao' (20:9) ambao Yesu anauita 'mji wa Mungu wangu' (3:12). Ule mji mtakatifu ndio ule Yerusalemu wa kiroho wa watakatifu." (Kistemaker 2000: 437)

Paulo anatumia hii taipolojia istiari katika **mst. 29-31**. Katika **mst. 29** anazungumza kuhusu wale wanaozaliwa kwa mwili wakiwatesa wale ambao wanazaliwa kwa Roho. Hilo ni dhahiri kwamba inasema kuhusu wakati Ishmaili "akimdhihaki" Isaka katika **Mwz 21:9**, kwa sababu katika **Gal 4:30** Paulo ananukuu **Mwz 21:10** pale ambapo Sara alimwambia Ibrahimu *"mfukuze mjakazi huyu namwanawe, maana mwana wa mjakazi hatarithi pamoja na mwana wa mwanamke aliye huru."* Ben Witherington anatoa hoja, "Kipekee ikumbukwe kwamba yule 'mwangalizi' [*paidagōgos*] alikuwa mtumwa, na hivyo Paulo hapa anatumia sitiari nyingne ya mtumwa kuelezea athari ya Sheria" (Witherington 1998: 338). Matumizi ambayo yako wazi kwa ajili ya kanisa ni "kutupa nje" Wayahudishaji na ye yote anayeongeza kitu chochote kwenye injili ya wokovu kwa neema ya Mungu peke yake kwa njia ya imani peke yake ndani ya Kristo peke yake.

Nyongeza hizi kwenye injili zaweza kuwa za aina yoyote: katika siku za Paulo, wale Wayahudishaji walikuwa wanataka imani ndani ya Yesu + tohara na kuitii Sheria ya Musa, ikiwa ni pamoja na kufuata siku maalum, miezi na nyakati, na miaka; katika wokovu wa Kikatoliki ni mchakato unaohusu neema ya Mungu na imani ya mtu + matendo mema, ubatizo, kushiriki sakramenti mbalimbali, maungamo, rehema, kuzishika amri, na kujiepusha na dhambi ya mauti; katika Upentekoste wa kimapokeo wokovu unahusisha imani + kunena kwa lugha; katika makanisa mbali mbali wokovu unahusisha imani + kutii amri na sheria mbali mbali. Haya masharti

[18] Yale matumizi ya kihistoria ya kiukombozi ya **Isa 54:1** yanaonyeshwa na ule ukweli kwamba muktadha wa kiujumla wa huo ukweli wa mstari huo unahusisha kutajwa kwa Ibrahimu na Sara katika **Isa 51:2**. Hapo ndipo mahali pekee katika AK ambapo Sara anatajwa nje ya Mwanzo. Zaidi ya hapo, kabla tu ya **Isa 54:1** ni habari inayohusu "Mtumishi aliyeteseka" (**Isa 51:13-53:12**), ambayo ni nukuu iliyo wazi inayomhusu Yesu Kristo na kile alichokitekeleza pale msalabani (ona Menn 2009-2018: 91-92).

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

ya ziada yanaweza kuwa mambo mazuri. Yanaweza kuwa mambo ambayo Wakristo wanapaswa kufanya. Kuyafanya hayo inaweza kuwa ushahidi wa wokovu wetu na kutokuyatenda yaweza kuwa ni ushahidi kuwa mtu hajaokoka (ona **Yak 2:14-26**). Lakini, wakati ambapo haya mashariti ya ziada yanaweza kuwa *ushahidi* wa wokovu, ufunguo ni kwamba hayawezi kuwa *masharti* ambayo kwayo tunapata wokovu.

Wokovu (m.y., kuhesabiwa kwetu haki na kuasiliwa) ni kipawa cha Mungu kwa neema peke yake, kwa njia ya imani peke yake, ndani ya Kristo peke yake. Matokeo ni kwamba ikiwa kweli tuko "ndani ya Kristo" na Kristo ni Bwana wa maisha yetu, basi tunahitajika kuisha kama inavyopasa. Ni kwa hayo Paulo anayazungumzia katika sehemu yote iliyobaki ya kitabu.

MASWALI YA KUJADILI

1. Mtu anawezaje kumpokea Roho Mtakatifu?

2. Utakaso ni nini"? Utafanyikaje?

3. Kuna uhusiano gani kati ya imani na matendo?

4. Agano la Ibrahimu ni lipi na ni kwa nini lilikuwa la muhimu? Agano la Ibrahimu lilitazamia nini hapo baadaye na ni nani ni uzao wa kweli wa Ibrahimu?

5. Ni nini umuhimu wa nia (m.y., *kwa nini* tunafanya kile tunachofanya)? Ni kwa jinsi gani nia ya mtu ya kufanya kitu fulani yaweza kufanya tendo lile lile kuwa ama Baraka au laana?

6. Ni yepi yalikuwa makusudi ya Sheria ya Musa? Ni mambo yepi ambayo sheria iliweza kuyafanya na yepi haikuweza kuyafanya?

7. Ni kwa namna gani kuwa "ndani ya Kristo" hubadilisha uhusiano wetu na Mungu, na Sheria, na wengine?

8. Ni kwa nini ile dhana ya "kuasiliwa" ni muhimu, na ina maanisha nini kwetu na kwa namna tunavyoishi?

9. Ni nini kazi ya Roho Mtakatifu katika maisha ya Mkristo?

10. Ni nini maana ya "kurudi nyuma kithiolojia au kiroho"? Ni kwa nini inaweza kuwa ni mbaya zaidi ya kurudi nyuma au kurudi kwenye dhambi fulani bayana?

11. Katika istiari ya Paulo, ni kwa vipi Hajiri, Ishmaili, na Yerusalemu ya kimaumbile kihalali yaweza kusemwa kwamba inaiwakilisha Agano la Musa, Israeli, ile sheria na utumwa na Sara, Isaka, na "Yerusalemu wa juu" kihalali iwakilishe lile Agano Jipya, kanisa, imani na uhuru? Kwa misingi ya istiari ya Paulo (na kwa misingi ya mjadala wote katika sura ya 3-4), kwa nini watu wengi hufikiri kuwa watapokea Baraka Fulani maalumu kwa kutembelea Israeli ya sasa na Yerusalemu, kubatizwa ndani ya mto Yordani, nk.?

E. <u>Gal 5:1-6:10—Uhuru katika Kristo:</u> Mliitwa katika uhuru, hivyo enendeni kwa Roho.

- **<u>5:1-26—</u>**<u>Mliitwa katika uhuru, hivyo msijiweke tena chini ya utumwa wa sheria au mwili lakini enendeni kwa Roho.</u>

    - **<u>5:1-6—</u>**<u>Msiwe chini ya sheria ya kutahiriwa, ambayo huonyesha kwamba umeiacha neema ya Roho kwa ajili ya utumwa wa sheria.</u>

        [1] Katika uungwana huo Kristo alituandika huru; kwa hiyo simameni, wala msinaswe tena chini ya kongwa la utumwa.
        [2] Tazama mimi Paulo nawaambia ninyi ya kwamba, mkitahiriwa, Kristo hatawafaidia neno.
        [3] Tena nawashuhudia kila mtu atahiriwaye, kwamba ni wajibu wake kuitimiza torati yote.
        [4] Mmetengwa na Kristo, ninyi mtakao kuhesabiwa haki kwa sheria; mmeanguka na kutoka katika hali ya neema. [5] Maana sisi kwa Roho tunalitazamia tumaini la haki kwa njia ya imani. [6] Maana katika Kristo Yesu kutahiriwa hakufai neno, wala kutokutahiriwa, bali imani

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

itendayo kazi kwa upendo.

Kifungu hiki kidogo kinaweka zile kanuni za msingi za imani yetu na maisha ambayo Paulo atayaeleza katika sehemu ya mbeleni ya **sura 5** na sehemu ya kwanza ya **sura 6**. Ile kanuni ya msingi ya imani yetu inatajwa katika **mst. 1**, *"Katika uungwana huo Kristo alituandika huru."* Uhuru huu unahusisha uhuru utokanao na mahangaiko ya kujaribu kutimiza ile sheria, uhuru kutoka katika mahangaiko ya kutaka kupata na kuendelea kuwa na upendeleo wa Mungu, na uhuru kutoka katika hatia na aibu ya dhambi zetu kwa sababu tunajua kwamba tumekubaliwa na Mungu kwa sababu ya kile alichokifanya Kristo kwa ajili yetu. Hivyo, inatuweka huru tuishi kama Mungu alivyotuumba kuishi, huru kuishi "maisha ya utele" (**Yohana 10:10**) yanayompendeza Mungu na yenye utoshelevu kwetu, yasiyotatizwa na dhambi na sheria na amri zilizowekwa na wanadamu ambazo huwafunga wengi. Hapa tena, kanuni hii huufanya Ukristo kuwa tofauti na dini nyingine yoyote duniani. Na pia inakwenda kinyume na "hali yetu ya kushindwa" ambayo kwayo tunafikiri kwamba tunaweza kupata na kuendelea kuwa na upendeleo wa Mungu kwa kufanya matendo fulani au kufuata jadi fulani badala ya au zaidi ya kutegemea kikamilifu katika kile ambacho Kristo amekifanya kwa ajili yetu.

Ndio maana Paulo anatusihi *"simameni, wala msinaswe tena chini ya kongwa la utumwa."* Kutaja kwake *"kongwa la utumwa"* kutufanye sisi kukumbuka kile ambacho Yesu alisema katika **Math 11:29-30**: *"Jitieni nira yangu, mjifunze kwangu; kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu; kwa maana nira yangu ni laini, na mzigo wangu ni mwepesi."* Kwa kutusihi sisi *"kusimama, wala tusinaswe tena chini ya kongwa la utumwa"* Paulo anazungumza kuhusu jinsi tunavyoishi maishi yetu, ikimaanisha, si kuishi maisha ya kushika sana sheria, amri na kanuni, lakini tuongozwe na Neno la Mungu kwa njia ya uongozi wa ndani wa Roho Mtakatifu.

Katika **mst. 2-4** Paulo anazungumzia kuhusu yale mashariti bayana ambayo wale Wayahudishaji walisema kwamba Mataifa walioamini walitakiwa kuyatimiza: tohara.[19] Dokezo la Paulo ni kwamba maisha yetu yanakuwa yana msingi ama katika neema au sheria, imani au matendo. Hakuna chaguo la tatu na hizi dhana mbili—neema/imani au sheria/matendo—haziwezi kuchanganywa. Ikiwa mtu atachagua wokovu kwa njia ya matendo na sheria, basi *"Kristo hatamfaidia neno"* (**mst. 2**). Zaidi ya hayo, **mst. 3** unadokeza kwamba mtu hawezi "kuamua na kuchagua" ni masharti gani ya sheria ayatii. Ikiwa unajiweka wewe mwenyewe chini ya masharti ya sheria una *"wajibu wa kuitimiza sheria yote"* (ona pia **Yak 2:10**). In **mst. 4** Paulo anaendelea kusema kwamba ye yote anayetafuta kuhesabiwa haki kwa njia ya matendo ya sheria *"ametengwa na Kristo"* na *"ameanguka na kutoka katika hali ya neema."*

Mstari 4, kama hiki kifungo kidogo chote, ni onyo. Haimaanisha kwamba mtu kwa wakati fulani atakuwa amepokea neema ya Mungu iokoayo lakini baadae akaipoteza ile neema iokoayo na kuwa asiyeokoka. Mahali pengine Paulo anaweka wazi kabisa kwamba ikiwa mtu yuko "ndani ya Kristo" kiukweli (m.y., kwa neema ya Mungu amehesabiwa haki na kuasiliwa) yeye huyo hawezi kuupoteza wokovu wake. Kwa mfano, **Rum 8:28-30** inazungumza kuhusu mnyororo usiokatika kutoka wakati ule Mungu alipotangulia kutuchagua hadi kutuita mpaka kutuhesabia haki kwetu na hadi kututukuza. **Filp 1:6** inasema kwamba *"Yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu."* **Efe 2:6** inasema kwamba wale ambao wameokoka na wako ndani ya Kristo wameinuliwa na kuketishwa pamoja naye katika ulimwengu wa Roho. **Efe 1:13-14** inaongezea kwamba wale ambao wameshaamini wametiwa muhuri na Roho Mtakatifu ambayo ndiye mwenye dhamana na mwenye kututhibitishia urithi wetu hadi siku ile ya ukombozi. Yesu mwenyewe alisema, *"Sitakupungukia kabisa, wala sitakuacha kabisa"* (**Ebr 13:5**).

Kwa kuwa wale ambao wako ndani ya Kristo kikweli, Paulo anasema kwamba kuacha kumtegemea Kristo kikamilifu kutampeleka mtu kwenye anguko la *kutokuielewa* neema yake. Hali hii ni kitu kama wale walio dhaifu katika imani katika **Warumi 14** na **1 Wakorintho 8**. Katika vifungu hivyo Paulo anasema kwamba, ndani ya Kristo, tuna uhuru wa kula chochote tutakacho. Hata hivyo, wale walio dhaifu wa imani hawajui kuhusu uhuru wetu ndani ya Kristo. Kwa hiyo, wanakuwa na shaka na kujikwaa na kujisikia kuhukumiwa wanapokula kinyume na ile sheria ya Musa ya vyakula au wanapokula nyama ambayo imetolewa dhabihu kwa sanamu za wapagani. Hawaioni ile furaha ya wokovu wao ambayo huja kwa njia ya kuijua neema ya Bwana siku kwa siku wanapoendelea kuisha maisha yao. Kama ambavyo John Piper anasema, "Ufunguo wa kupata uhuru uko katika kuokolewa na Mungu na juhudi yake ya kutujali katika maisha yetu hapa na sasa. Tuko huru wakati Mungu anakuja kutusaidia kwa uhuru na kwa furaha tunautegemea msaada wake badala ya kugeukia nira ya sheria." (Piper 1983b: n.p.) Kwa upande mwingine, Paulo pia analionya kanisa kwa sababu njia ya namna hiyo ni "njia pana iendayo upotevuni" (**Math 7:13**) ambayo ni kinyume na ile "njia nyembamba

[19] Ingawaje katika **Gal 2:3** lile swala la Tito kutokutahiriwa lilitajwa, tamko la kwanza la **Gal 5:2** ni kwamba tohara ilikuwa dai la msingi la wale Wayahudishaji ambalo lilikuwa likiligawa kanisa la Galatia.

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

iendayo uzimani" (**Math 7:14**), m.y., wokovu kwa neema ya Mungu kwa njia ya imani ndani ya Kristo peke yake. Wale Wayahudishaji wanaweza kuonekana kwa nje kuwa wameokoka lakini fundisho lao hudhihirisha kwamba kamwe hawakuwahi kuwa wamezaliwa mara ya pili kiukweli (ona **1 Tim 1:19-20; 1 Yohana 2:18-19**).

Paulo anayaleta maswala haya katika ufasaha mkuu zaidi katika **mst. 5-6**. Katika **mst. 5** anasema kwamba *"sisi kwa Roho tunalitazamia tumaini la haki."* Anatuambia kwamba kwa njia ya Roho (sio mwili) na kwa imani (sio kwa matendo ya sheria) wale walio ndani ya Kristo wana tumaini lililo thabiti. Haki yetu (kusimama bila hatia) mbele za Mungu ni hakika na salama kwa sababu imewekwa juu yetu na Kristo, sio kitu ambacho tunajitahidi kukipata kwa juhudi zetu wenyewe. Matokeo yake, tumaini letu la kupokea ule urithi litatimia kwa sababu, lenyewe pia, misingi yake ni katika kile ambacho Kristo amekifanya, sio juhudi zetu wenyewe. Hivyo, "tumaini la mwenye haki kwa dhahiri kabisa liko tofauti na lile la wale ambao wanaweza kutumaini katika ile haki ya kutahiriwa tu na vitendo maalumu vya kidini—ambavyo matokeo, yake huwaacha bila ya tumaini. Wanautumainia mwili na matendo. Wao waitarajie tu ile adhabu wanayoistahili chini ya laana ya sheria." (Riddlebarger 1998d: 6)

Katika **mst. 6** Paulo anahitimisha kifungu hiki kidogo kwa kutukumbusha kwamba *"kutahiriwa hakufai neno wala kutokutahiriwa."* Hapa tena, ni kitu kama ule mjadala wake wa kula chakula katika **Romans 14** na **1 Wakorintho 8**. Ile aina ya chakula unachokula haijalishi. Mambo haya yasiwe maswala ambayo kwayo baadhi ya Wakristo huhukumu Wakristo wengine. Jambo ambalo ni muhimu, kama John Piper alivyosema hapo awali, ni kukumbuka kwamba "sio hasa kile unachofanya bali ni kwa nia gani unakifanya. Kutahiriwa kwaweza kuwa 'kazi ya sheria' [**Gal 2:1-5**] au tendo la upendo ambalo hutiririka kutoka katika imani [**Matendo 16:3**]. Kwa wewe mwenyewe kujiweka chini ya sheria za vyakula yaweza kuwa kazi ya sheria [**1 Kor 8:7**] au tendo lililo huru la upendo litokanalo na imani [**Rum 14:21; 1 Kor 8:13**]." (Piper 1983a: n.p.) Maswala ni kwamba ni kwanini tunafanya kile tunachikifanya na ni nani tunayempa sifa.

Hili linatufikisha kwenye tamko la mwisho katika **mst. 6** ya kwamba jambo lililo muhimu kuliko yote ni *"imani itendayo kazi kwa upendo."* Hili ni matokeo ya wokovu upatikanao kwa imani tu ndani ya Kristo, kwa sababu *"imani itendayo kazi kwa upendo"* huelezea ile asili ya kile ambacho imani ya kweli iokoayo ni nini. Kama vile kutahiriwa—ikiwa kutafanyika kwa sababu ya kujaribu kupata upendeleo wa Mungu—ni ishara kwamba huyu mtu *haja*okoka, Paulo anasema kwamba *"imani itendayo kazi kwa upendo"* ni ishara kwamba mtu ameokoka. "Imani" ni zaidi ya "kuamini" kiakili katika kitu fulani. "Imani" kwa hakika inahusisha kipengele muhimu cha fundisho (ona, mfano, **Matendo 2:22-24, 32-36; Rum 1:1-4; Rum 10:9; 1 Kor 15:1-8**). Lakini imani yenye misingi katika kutegemea kile ambacho Kristo amekifanya kwa ajili yetu haimaanishi kwamba "sasa tunaweza kufanya chochote kile tutakacho." Imani ya kweli iokoayo huhusisha vipengele muhimu vya kitabia (ona, mfano, **Efe 2:8-10; Yak 2:14-20; Math 28:18-20; Yohana 14:23-24**) na vyenye kuleta matokeo au vipengele vya kuhamasisha kujitoa (ona, mfano, **Yohana 15:4-11, 12-15; 17:3; 21:15-17**). Kwa maneno mengine, imani ya kweli iokoayo, inahusisha maisha yetu yote na hujidhihirisha kwa njia ya upendo. Martin Luther anaiweka hivi, "Ni wazi kwamba imani lazima iwe aminifu. Ni lazima iwe imani ambayo hutendo matendo mema kwa upendo. Ikiwa imani haina upendo hiyo sio imani ya kweli. . . . Kufikiri, 'Ikiwa imani hutupa haki bila ya matendo, basi na tusifanye chochote,' ni kuidharau neema ya Mungu. Imani isiyotenda chochote si imani ya kutupatia haki. . . . Kwa ndani ina [imani inayotufanya tuhesabiwe haki] imani kumuelekea Mungu, kwa nje ina upendo kwa watu." (Luther 1535: re. Gal 5:6). "Imani iokoayo siku zote huamsha upendo na upendo huthibitisha imani iliyo kweli" (Piper 1983c: n.p.). Isipofanya hivyo, hiyo siyo imani ya kweli, ile iokoayo. Hivyo ndivyo ilivyo kwa sababu upendo unatoka kwa Mungu, Mungu ni upendo (**1 Yohana 4:7-8, 16**), na sisi yatupasa kuwa kama Yeye (**Rum 8:29; 1 Kor 15:49; 2 Kor 3:18**). Kwa kweli, *"Sisi twapenda kwa maana yeye alitupenda sisi kwanza"* (**1 Yohana 4:19**; ona pia **Efe 5:2**). "Ikiwa ye yote atauliza, 'Ni kwa namna gani ule ukweli kwamba Mungu anakupenda husababisha na wewe kuwapenda watu wengine?' jibu ni: Kule kuzaliwa upya ndiko kunakosababisha ule uhusiano. Kuzaliwa upya ni tendo la Roho Mtakatifu akiunganisha mwili wetu mfu, mioyo ya kiubnafsi na Mungu aliye hai, moyo wa upendo kiasi kwamba maisha yake yanakuwa maisha yetu na upendo wake unakuwa upendo wetu." (Piper 2009: 157) Hivyo, upendo ni ishara ya msingi ambayo hudhihirisha ikiwa kama mtu ameokoka kweli au la.

Vile ambavyo upendo ni kiini cha uhusiano wa Kikristo wenyewe (na kwenye Ukristo wenyewe) inaonekana katika njia zifuatazo:

- Upendo ni kiini kiasi kwamba Yesu alisema kwamba amri mbili, *"Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote,"* na *"Mpende jirani yako kama nafsi yako,"* ndizo za msingi katika Biblia (**Math 22:36-40; Marko 12:28-34; Luka 10:25-28**).
- Upendo ni kiini kiasi kwamba, *"yeye asiyependa hakumjua Mungu"* (**1 Yohana 4:8**), na *"Mtu akisema, 'Nampenda Mungu,' naye anamchukia ndugu yake, ni mwongo; kwa maana asiyempenda ndugu yake ambaye amemwona hawezi kumpenda Mungu ambaye hakumwona"* (**1 Yohana 4:20**).

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

- Upendo ni kiini kiasi kwamba umehusianishwa na msamaha wa dhambi zetu (**Luka 7:36-50; 1 Pet 4:8**).
- Upendo ni kiini kiasi kwamba lile "lengo" la mafundisho ya Ukristo ni *"upendo utokao katika moyo safi na dhamiri njema, na imani isiyo na unafiki"* (**1 Tim 1:5**).
- Upendo ni kiini kiasi kwamba ile sheria yote inatimilika katika tamko, *"mpende jirani yako kama nafsi yako"* (**Rum 13:8-10; Gal 5:14**).
- Upendo ni kiini kiasi kwamba ule usiku kabla Hajafa, "amri mpya" Yesu aliwapa wanafunzi wake ilikuwa *"Mpendane, kama vile nilivyowapenda ninyi"* (**Yohana 13:34; 15:17**).
- Upendo ni kiini kiasi kwamba *"upendo wa ninyi kwa ninyi"* ni ishara ambayo Yesu aliitoa ambayo kwayo *"watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu"* (**Yohana 13:35**).
- Upendo ni kiini kiasi kwamba ni *"njia iliyo bora"* (**1 Kor 12:31**). Mtu asipokuwa na upendo, yeye "si kitu" hata kama ananena kwa lugha za wanadamu na malaika, ana karama ya unabii, ana maarifa yote, na ana imani kiasi cha kuhamisha milima (**1 Kor 13:1-2**). Kama mtu hana upendo, "haimfaidii kitu" hata kama atatoa kila kitu alichonacho kuwasaidia maskini na hata akiutoa mwili wake uchomwe moto (**1 Kor 13:3**).
- Upendo ni kiini kiasi kwamba *"juhudi nyingi katika kupendana"* inahitajika ionyeshwe *"zaidi ya vingine vyote"* (**1 Pet 4:8**).
- Upendo ni kiini kiasi kwamba ni wa kwanza kuorodheshwa katika *"tunda la Roho"* katika **Gal 5:22-23** na unaweka pamoja kila kipengele kimojawapo cha *"tunda la Roho"* (kimsingi, lile *"tunda la Roho"* ni moja, si zaidi ya moja).
- Upendo ni kiini kiasi kwamba ni *"kifungo cha ukamilifu"* ambao unatakiwa uonyeshwe zaidi ya vitu vingine vyote (**Kol 3:14**).
- Upendo ni kiini kiasi kwamba Maandiko huuita *"sheria ya kifalme"* (**Yak 2:8**).
- Kilele cha upendo ni kujitoa dhabihu: *"Hakuna aliye na upendo mwingi kuliko huu, wa mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake"* (**Yohana 15:13**).
- Ile sheria ya upendo ni ya kiutendaji hasa: *"Basi yo yote myatakayo mtendewe na watu, ninyi watendeeni vivyo hivyo; maana hiyo ndiyo torati na manabii"* (**Math 7:12; Luka 6:31**).
- Mitume waliendelea kuwasihi waamini kwa misingi ya upendo na kuwahimiza kuonyesha upendo wao kwa wao zaidi na zaidi (**1 Kor 8:1; 16:14; 2 Kor 2:8; 8:24; Gal 5:6, 13; Efe 3:17-19; 4:2, 15; 5:2, 25, 28; Filp 2:1-2; Kol 2:2; 3:14; 1 Thes 3:12; 4:9; Flm 9; Ebr 10:24; 1 Pet 2:17; 4:8; 2 Pet 1:7; 1 Yohana 4:7-11; 2 Yohana 5**).

Katika **Gal 5:13–6:10** Paulo atafafanua kwa undani *"imani itendayo kazi kwa upendo"* ikoje katika hali ya kimatendo.

- **5:7-12—**Msiwafuate wale ambao mafundisho yao hayatoki kwa Bwana.

  7 Mlikuwa mikipiga mbio vizuri; ni nani aliyewazuia msiitii kweli? 8 Kushawishi huku hakukutoka kwake yeye anayewaita ninyi. 9 Chachu kidogo huchachusha donge zima. 10 Nina matumaini kwenu katika Bwana, ya kwamba hamtakuwa na nia ya namna nyingine. Lakini yeye anayewafadhaisha atachukuwa hukumu yake, awaye yote. 11 Nami, ndugu zangu ikiwa ninahubiri habari ya kutahiriwa, kwa nini ningali ninaudhiwa? Hapo kwazo la msalaba limebatilika! 12 Laiti hao wanaowatia mashaka wangejikata nafsi zao!

Mistari hii sita hufanya kama aina fulani ya maoni marefu yaliyo kwenye mabano kabla ya Paulo kuanza wazo lake kuu na mjadala kuhusu uhuru wetu ndani ya Kristo na asili ya imani ya kweli iokoayo. Mistari hii hudokeza kwamba wale Wagalatia walianza vema. *"Wakipiga mbio vizuri"* na *"wakiitii kweli"* (**mst. 7**) anafikia kutaja tena ile kanuni ya *"imani itendayo kazi kwa imani." "Mkipiga mbio vizuri"* na *"mkiitii kweli"* huenda sambamba na hudhihirisha kwamba imani ya kweli iokoayo, iko hai na ni imani itendayo kazi. Si imani iliyoko kwenye ufahamu tu lakini ni imani inayowekwa kwenye matendo ya maisha yetu ya kila siku. Ni kama vile ambavyo Paulo alivyosema katika **Filp 2:12-13**, *"12 Basi wapendwa wangu, kama vile mlivyotii siku zote, si wakati mimi nilipokuwapo tu, bali sasa zaidi sana mimi nisipokuwepo, utimizeni wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka. 13 Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema."* Tambua kwamba Paulo anasema *"utimizeni"* wokovu wenu, sio *"tendeni kazi kwa ajili ya"* wokovu wenu (ona pia **Yak 2:14-26**).

Paulo tena anaweka wazi kwamba lile fundisho la walimu wa uongo halikutoka kwa Mungu (**mst. 8**) lakini lina athari kama ya chachu, m.y., linaenea katika mwili wote mpaka kanisa lote linanajisiki (**mst. 9**). Hata

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

hivyo, anauelezea ujasiri wake kwamba wale Wagalatia hawataanguka kutoka katika njia sahihi bali wataendelea kuwa waaminifu katika injili ya kweli; kwa upande mwingine, Yule mwalimu wa uongo atahukumiwa na Mungu kwa fundisho lake la uongo (**mst. 10**).

Mstari 11-12 ni mwitikio wa Paulo kwa kile ambacho kinaonekana kuwa shambulio dhidi yake binafsi kutoka kwa Wayahudishaji. Wale Wayahudishaji inavyoonekana walikuwa wakisema kwamba Paulo hakuwa akipinga tohara (ona **Matendo 16:3** ambapo alimtahiri Timotheo kwa sababu za manufaa). Madai kama hayo yatakuwa yanatoka nje ya muktadha kabisa wa kile ambacho Paulo alikuwa akikisema. Wale Wayahudishaji walikuwa wameipatia tohara wajibu na maana ambayo kamwe Paulo hakuwahi kuifundisha wala kuiruhusu. Dokezo lake katika **mst. 11** ni kwamba "ikiwa kweli ninafundisha tohara kama wale Wayahudishaji wanavyofanya, basi ni kwa nini ninashambuliwa na wao? Kwa hakika, nafasi yao inaondoa ule utoshelevu wa kile ambacho Kristo alikifanya msalabani."

Katika **mst. 12** anatoa maoni "makali" dhidi ya wapinzani wake kwa matokeo, kwa kuwa tohara ni muhimu kiasi hicho kwao basi wasiishie hapo bali waendelee mbele zaidi katika hilo mpaka wajihasi wenyewe! Hii si kuwa na roho ya kikatili, kwa kuwa katika **Marko 9:43, 45, 47** Yesu said, *"[43] Na mkono wako ukikukosesha ukate; ni afadhali kuingia katika uzima u kigutu, kuliko kuwa na mikono miwili na kwenda zako jehanum, kwenye moto usiozimika. . . . [45] Na mguu wako ukikukosesha, ukate; ni afadhali kuingia katika uzima u kiwete, kuliko kuwa na miguu miwili na kutupwa katika jehanum. . . . [47] Na jicho lako likikukosesha, ling'oe, ilitupe; ni afadhali kuingia katika ifalme wa Mungu, una chongo, kuliko kuwa na macho mawili, na kutupwa katika jehanum."* Zaidi ya hayo, katika **Filp 3:2** Paulo anawaita walimu wa uongo kama hao "tohara potofu" au "kuatilika." Neno lake ya Kiyunani ni *katatomē* ambalo humaanisha "ukataji, uchinjaji" (Zodhiates 1993: *katatomē*, 847). Zodhiates anasema, "Paulo anawaita wale walimu wa Kiyahudi 'wachinjaji,' kwa sababu baada ya kuja kwa Kristo walifundisha kwamba tohara ya nje ya mwili ilikuwa ni lazima kwa ajili ya kupata wokovu wakati ambapo wakati huo huo walikuwa fukara wa tohara ya moyoni" (Ibid.; ona pia Danker 2000: *katatomē,* 528 [lile neno hutumika kwa "wale ambao kutahiriwa huleta matokeo ya uharibifu (kiroho)"]). Kile ambacho Paulo anasema katika **Gal 5:12** kimsingi ni, "yale mafundisho ya wale Wayahudishaji hupelekea kwenye kuchinjwa kiroho; kwa hiyo, kwa kuwa kukata mwili ni muhimu sana kwao, basi na waendelee kijitendea kimwili kile ambacho mafundisho yao kitafanya kiroho kwa ye yote anayeyaamini na kuyafuata."[20]

- **5:13-15—**Msiugeuze uhuru wenu kuwa fursa ya mwili; badala yake, mpendane ninyi kwa ninyi (ambalo huitimiza sheria).

  [13] Maana ninyi, ndugu, mliitwa mpate uhuru; lakini uhuru wenu usiwe sababu ya kuufuata mwili, bali tumikianeni kwa upendo. [14] Maana torati yote imetimilika katika neno moja, nalo ni hili, "UMPENDE JIRANI YAKO KAMA NAFSI YAKO." [15] Lakini mkiumana na kulana, angalieni msije mkaangamizana.

Katika mistari hii Paulo anachagua lile eneo lenye msukumo mkubwa zaidi katika mjadala aliouanza katika **mst. 1-6** kuhusiana na namna ambavyo tunapaswa kuishi maisha yetu katika uelewa wa ukweli kwamba wokovu wetu na maisha hutegemea imani ndani ya Kristo moja kwa moja na sio katika matendo ya sheria. **Mstari 1** ulikuwa umeanza, *"Ilikuwa ni kwa ajili ya uhuru Kristo alituweka huru"*; **mst. 5** ulikuwa umesema kuhusiana na ukweli kwamba maisha yetu sasa ni *"kwa Roho, kwa njia ya imani"*; na **mst. 6** alikuwa ametamatisha kwa kutaja umuhimu wa ujumla wa *"imani itendayo kazi kwa upendo."* Dhamira hizi zitaendelezwa na kuelezewa katika **Gal 5:13–6:10**.

Katika **mst. 13** Paulo anarudia kwamba injili inatuita kwenye uhuru. Halafu tena anaelezea kwamba uhuru huu katika njia ya pande mbili: *"uhuru wenu usiwe sababu ya kuufuata mwili, bali tumikianeni kwa upendo."* Hili hujumuisha kwenye maelezo ya kile ambacho *"imani itendayo kazi kwa upendo"* humaanisha. Ile sehemu ya kwanza ya maelezo (*"uhuru wenu usiwe sababu ya kuufuata mwili"*) hushughulikia ule ukweli kwamba uhuru wa Wakristo hauwezi kuwa kisingizio cha kuhalalisha tabia za dhambi. Lile neno "mwili" linatumika kwa namna mbali mbali tofauti katika muktadha tofauti. Wakati mwingine linamaanisha ubinadamu wetu, wakati mwingine humaanisha maumbile ya mwili wetu. Katika muktadha huu, "mwili" humaanisha "ile hulka ya kibinadamu na uwezo wa asili, mwelekeo, na uasilia. Kwa maneno mengine, 'mwili' wangu maana yake ni vile nilivyo kama mwanadamu ukiondoa mabadiliko mengine ambayo yanaweza kuwa yametokea kwa njia ya kiungu au matokeo ya kiuumbaji. Kwa kuwa nina hulka ya uasi wa dhambi, niliye kinyume na Mungu na

[20] Hoja ya Paulo inaonekana katika AK. **Kumb 23:1** inasema, *"Aliyejeruhika konde, au aliyekatika tupu lake, asiingie mtu huyo katika mkutano wa Bwana."*

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

kila kitu kuhusu Yeye na viwango vyake vya thamani, ile dhana ya ‘mwili’ kwa kawaida itakuwa na kidokezo hasi. Inamaanisha madhaifu yangu ya kimaumbile, uovu, na hali ya uasi. Tunaweza kufafanua dhana ya Paulo ya ‘mwili’ kwa usahihi katika muktadha kama ‘hulka ya kibinadamu ya dhambi.’” (Crabtree 2001: n.p.) Paulo anadokeza kwamba injili ni uhuru *kutoka* katika dhambi, si uhuru wa *kutenda* dhambi. Alidokeza vivyo hivyo katika **Rum 6:1-2**: *“[1] Tuseme nini basi? Tudumu katika dhambi ili neema izidi kuwa nyingi? [2] Hasha! Sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi?”*

Yesu alisema, *“Yesu akawajibu, Amin, amin, nawaambia, kila atendaye dhambi ni mtumwa wa dhambi”* (**Yohana 8:34**; ona pia **Tito 3:3**). Yesu alikuwa akisema kwamba tabia ya kutenda dhambi humtumikisha Yule ambaye anatenda dhambi. Sababu ni kwamba dhambi yenyewe ni aina ya nguvu, na iko hai (**Mwz 4:7** [*dhambi iko, inakuotea mlangoni, nayo inakutamani wewe”*]; ona pia **Rum 6:12; 7:8, 11**). Zaidi ya hayo, ile nguvu iliyo hai ya dhambi inaishi ndani yetu (**Rum 7:17, 20-21, 23**). Inakaa ndani ya “mioyo” ya watu, m.y., ndani ya utu wetu wa ndani, msingi wa sisi ni nani (**Mwz 8:21; Math 12:34; 15:18-19; Marko 7:20-23; Luka 6:45**). Hili hufahamika kama nguvu ya “dhambi ikaayo ndani.” Paulo anaiita “sheria” ambayo imo ndani yetu (**Rum 7:21, 23, 25**). Anaiita ile dhambi ikaayo ndani kuwa ni sheria iliyo ndani yetu kwa sababu “ni kanuni yenye nguvu sana ambayo hutenda kazi ndani mwetu” ambayo hutulazimisha na kutuhimiza kufanya kulingana na vile inavyotaka, na kila dhambi tuifanyayo “huiongezea nguvu ile kanuni na kuiimarisha ile tabia ya dhambi” (Owen 1979: 7, 27). Dhambi ikaayo ndani lengo lake ni kututawala sisi (**Mwz 4:7**); inatawala na kutamani (**Rum 6:12**); hutenda visivyo haki (**Rum 6:13**); inaweza kuwa bwana wetu (**Rum 6:14**); inachukuwa fursa na kutengeneza tamaa ya kila aina (**Rum 7:8**); inadanganya na kuua (**Rum 7:11**); inapigana vita na kutufanya sisi kuwa wafungwa (**Rum 7:23**).

Hata kama ile sheria ya dhambi ikaayo ndani mwetu imo ndani mwetu, nguvu ya dhambi juu yetu imeshavunjwa na Kristo (ona **Rum 6:6-22**). Sasa neema inatawala kupitia Kristo (**Rum 5:21**); tumewekwa huru kutoka katika dhambi (**Rum 6:7, 18, 22**); dhambi haina tena nguvu ya kututawala sisi (**Rum 6:14**). Badala yake, Mungu amewapa Wakristo nguvu kubwa zaidi—Roho Mtakatifu. Kwa ngvuvu za Roho Mtakatifu hatuhitaji tena kutii ule ushawishi wa dhambi uliomo ndani yetu bali sasa tuna uwezo wa kuzikataa tamaa za kutenda dhambi na kuisha kwa kufuatana na mapenzi ya Mungu (**Rum 6:17-18; 7:6; 8:12-14**). Dokezo la Paulo hapa ni kwamba kuutumia uhuru wetu ndani ya Kristo kuitii ile “sheria ya ndani” a dhambi ni kinyume kabisa na kule kutenda kwa uhuru katika imani. Itaturudisha tena katika utumwa kama kujaribu kupata haki au utakaso kwa njia ya kujitiisha kwa ile “sheria ya nje” ya amri na kanuni ambavyo kungetuweka katika utumwa. Hayo yote yako kinyume na injili na pia yako kinyume na kile ambacho imani ya kweli iokoayo humaanisha.

Kifungu cha pili cha maneno cha **mst. 13**, *“bali tumikianeni kwa upendo,”* hutupa ule upande “chanya” wa uhuru ndani ya Kristo na maana ya imani ya kweli iokoayo. Ona kitendawili cha ule uhuru ndani ya Kristo: uhuru wetu si wa kujisukuma wenyewe na taama zetu lakini ni uhuru wa kuwatumikia wengine kwa upendo kama vile Kristo alivyowatumiki wengine (ona **Yohana 13:3-17**). Ni kwa nini kuwatumikia wengine kwa upendo ni uhuru bali kuutumikia mwili ni utumwa? “Kwa sababu *upendo* unahamasishwa na ile furaha ya kushirikishana *utoshelevu* wetu, bali yale *matendo ya mwili* huhamasishwa na ile tamaa ya kuujaza *utupu* wetu. Maana ya ‘mwili’ katika kitabu cha Wagalatia si ile sehemu ya mwanadamu ya maumbile yake, bali ni nafsi ya mtu ambayo hujisikia kuwa tupu sana na hutumia ile namna iliyomo katika uwezo wake kuujaza ule utupu. Ikiwa ni ya kidini, inaweza kutumia sheria; ikiwa si ya kidini, inaweza kutumia unywaji wa pombe. Lakini jambo moja ni hakika: mwili hauko huru. Unatumikishwa na tamaa moja isiyo na manufaa baada ya nyingine katika juhudi yake ya kuujaza utupu ambao ni Kristo peke yake anaweza kuujaza. . . . Tunapopenda hatutumikishwi kutumia vitu au watu ili kuujaza utupu wetu. Upendo ni kutiririka kwa utoshelevu wetu. Kwa hiyo, upendo ndiyo tabia pekee ambayo tunaweza kutenda kwa uhuru. Wakati Mungu anatuweka huru kutoka katika hatia na hofu na ulafi na kutujaza na uwepo wake unaotosheleza, nia pekee inayobaki ni ile furaha ya kushirikishana utoshelevu wetu.” (Piper 1983c: n.p.) Ndiyo maana **1 Kor 13:5** inasema kwamba upendo *“hautafuti mambo yake.”*

Mstari 14 unafupisha kwamba sheria yote inatimizwa na lile tamko, *“umpende jirani yako kama nafsi yako.”* “‘Mpende jirani yako kama nafsi yako’ sio amri ya wewe kujipenda mwenyewe. Ni amri ya kuuchukuwa ule upendo wako wa asili ambao tayari unao wa kujipenda na kuufanya kipimo cha kuwapenda wengine.” (Ibid.) Ili tuweze kufanya hivyo kikamilifu tutahitaji kutumia kiwango cha muda ule ule, fikra, nguvu, na pesa kufanya vitu kwa ajili ya manufaa ya wengine kama tunavyotumia kwa ajili ya manufaa yetu wenyewe. Huu ni witu ulio mkuu sana—lakini hili ndilo lile ambalo Yesu alilifanya kwa ajili yetu, na sisi tunapaswa kufananishwa na mfano wake (**Rum 8:29**). Hii ndiyo maana ya injili—na maana ya imani ya kweli iokoayo—inavyomaanisha katika maisha yetu. **Mstari 15** unatupa mbadala wake wa hili, ambao ni, mkilana ninyi kwa ninyi mtamalizana ninyi kwa ninyi. Hiyo ndiyo sura ya kile ambacho wanyama wa mwituni hufanyiana wanapokuwa na njaa. Hata hivyo, ndani ya Kristo hatuko katika njaa bali tumehesabiwa haki, tumeasiliwa, na

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

kujazwa na Roho Mtakatifu.

Kwa ujumla, mistari hii hutukumbusha kwamba Kristo kimsingi hutubadilisha. “Msalaba hutuweka huru kutoka katika nguvu ya dhambi, hutuliza ghadhabu ya Mungu, husafisha uchafu wa dhambi na hatia, humpatanisha mwamini na Mungu, na kuupata ushindi wa kidunia dhidi ya adui wote waangamizaji wa kiroho” (Demarest 1997: 196). Mtu anapomjia Kristo, yeye anapokea moyo mpya (**Ezek 36:26; 2 Kor 3:3**), nia ya Kristo (**1 Kor 2:16**), na Roho wa Kristo (**Ezek 36:26; Yohana 14:17**). Kuokoka na kuunganika na Kristo huwapa Wakristo uhusiano wa karibu sana wa kibinafsi na Mungu kwa njia ya Kristo: tunaweza *“kukikaribia kiti cha neema kwa ujasiri”* (**Ebr 4:16**; ona pia **Ebr 7:19**) kwa sababu Kristo yuko “ndani” ya mwamini (**Yohana 14:20; 17:23; Rum 8:10; Gal 2:20; Efe 3:17; Kol 1:27; 1 Yohana 3:24; Ufu 3:20**) na waamini wako “ndani ya Kristo” (**Rum 8:1; 12:5; 16: 6, 7, 9-10; 1 Kor 1:2, 30; 4:10, 15; 15:18, 22; 2 Kor 1:21; 5:17; 12:2; Gal 1:22; 3:28; 6:15; Efe 1:3; 2:6, 10; Filp 1:1; Kol 1:2; 1 Thes 2:14; 4:16; 1 Tim 3:13; 2 Tim 3:12; Flm 23; 1 Pet 5:14**). Kuokoka na kuunganishwa na Kristo huwapa Wakristo nia mpya na sababu ya kuishi. Anavyovithamanisha Kristo na kuvipa kipaumbale vinakuwa ndivyo tunavyovithamanisha na kuvipa kipaumbele; anatenda kazi ndani yetu na kupitia sisi ili atufanye sisi kuwa kama yeye (**Rum 8:29; Filp 2:12-13**). Kuokoka na kuunganishwa na Kristo hutengeneza kizazi kipya cha watu (**Yohana 3:3; Rum 6:4; 2 Kor 5:17; Gal 6:15**): tumeasiliwa katika familia ya Mungu kama watoto wake (**Yohana 1:12; Rum 8:14-17, 23; 9:4; Gal 3:26; 4:5-7; Efe 1:5; 2:19; 1 Yohana 3:1**) na kuwa na uhusiano wa karibu sana kati ya sisi kwa sisi kama ndugu kaka na dada (mfano, **Math 12:50; Matendo 1:16; 6:3; 11:29; 12:17; 16:40; 18:18; 21:7, 17; Rum 14:10; 1 Tim 5:1-2**). Kwa hiyo, sisi hatuko tena chini ya sheria ya nje au kutumikishwa na ile nguvu ya dhambi ikaayo ndani bali tunaongozwa na Neno la Mungu kwa njia ya Roho Mtakatifu. Maisha yetu yanaendeshwa na *“imani itendayo kazi kwa upendo”* ambayo hujidhihirisha *“tunapotumikiana kwa upendo”* kwa *“kuwapenda jirani yetu kama nafsi zetu.”* Hivi ndivyo injili na ile imani ya kweli iokoayo ilivyo kadiri tunavyoiishi katika maisha halisi.

- **<u>5:16-26—</u>**<u>Matendo ya mwili na tunda la Roho hupingana.</u>

  16 Basi nasema, enendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili. 17 Kwa sababu mwili hutamani ukishindana na Roho, na Roho kushindana na mwili; kwa maana hizi zimepingana, hata hamwezi kufanya mnayotaka. 18 Lakini mkiongozwa na Roho, hampo chini ya sheria. 19 Basi matendo ya mili ni Dhahiri, ndiyo haya, uasherati, uchafu, ufisadi, 20 ibada ya sanamu, uchawi, uadui, ugomvi, wivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, 21 husuda, ulevi, ulafi, namambo yanayofanana na hayo, katika hayo nawaambia mapema, kama nilivyokwisha kuwaambia ya kwamba watu watendao mambo ya jinsi hiyo hawataurithi ufalme wa Mungu.
  22 Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu,
  23 upole, kiasi; juu ya mambo kama haya hakuna sheria. 24 Na hao walio katika Kristo Yesu wameusulubisha mwili na tamaa zake.
  25 Tukiishi kwa Roho, na tuenende kwa Roho. 26 Tusijisifu bure, tukichokozana na kuhusudiana.

Kwa kuanza na neno “Basi,” neno linalotofautisha, hiki kifungu kidogo kikuu kinaanza pale ambapo **mst. 15** umeachilia. Kinatuonyesha namna *“kwa njia ya upendo [tunaweza] kutumikiana”* badala ya *“kuangamizana.”* Kifungu hiki kidogo kinaonyesha ule utofauti ulioko kati ya kuishi kwa kuufuata mwili kulivyo ukilinganisha na kuishi kwa kumfuata Roho.

Tumedokeza hapo juu kwamba “mwili” humaanisha ile hali yetu, “ya asili,” ya zamani ya dhambi ambayo inahusisha ile nguvu ya dhambi ikaayo ndani. **Mistari 16-17** inatujulisha kwamba tunapokuja kwa Kristo Mungu haiondoi asili yetu ya kale bali hutupatia kitu kipya na chenye nguvu zaidi—Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu anapokelewa kwa imani kama sehemu ya kuzaliwa upya kwetu (**Gal 3:2-5, 14;** ona pia **Ezek 36:27; Yohana 3:5-8; 14:16-20; 2 Kor 3:3; Gal 4:6; Tito 3:5-7**). Roho hutumia Neno la Mungu na Mwili wa Kristo ili kutuwezesha sisi kuipinga ile nguvu ya dhambi inayokaa ndani na kuijenga asili mpya, ambayo inaendelea kuwa kama Kristo (m.y., mchakato wa utakaso).[21] Kwa hiyo, ndani ya kila Mkristo kuna mgogoro

[21] “Ile hali ya kuhuisha au kufanya upya ya Roho Mtakatifu wa Mungu ni mfano wa tohara katika Agano la Ibrahimu na Agano la Musa. Tohara ilikuwa ni ile ishara ya nje, inayoonekana, ya kuwa mtu alikuwa amechaguliwa kupokea bar aka za Mungu kama mtoto wa Ibrahimu. Chini ya Agano Jipya–Injili–pia kuna ishara ya nje inayoonekana, ya kuwa mtu amechaguli wa kupokea Baraka za Ibrahimu. Lakini tohara ya kimwili siyo hiyo ishara, kwa sababu ile ishara ya kweli ya kwamba mtu ni mrithi wa urithi wa kweli haifanywi kwa mikono ya binadamu, bali na mikono ya Mungu. Ile tohara ya kweli ni alama inayobaki katika utu wetu wa ndani–‘mioyoni’ mwetu kwa njia ya kazi ya Roho wa kiungu inayotubadilisha.” (Crabtree 2001: n.p.)

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

wa ndani, kwa sababu ni Wakristo pekee walio na asili mbili (mwili na roho).[22]

Huu mgogoro wa ndani kati ya mwili na Roho ndilo somo la hii sehemu ndogo yote. Kuhusiana na huu mgogoro wa ndani, Kim Riddlebarger anatupa dokezo hili muhimu: "Mara nyigni Wakristo wanaambiwa kwamba yale mapambano dhidi ya dhambi na utambuzi wowote wa kukosa ushindi, au kushindwa kuwa na maendeleo endelevu, ni sababu zinazofanya kutilia shaka uhakika wa wokovu wao, au upendeleo wa Mungu kwao. Lakini kama Paulo anavyoweka wazi, ni Mkristo tu, ndiye ambaye ana Roho wa Mungu ndiye anayepitia mapambano kati ya Roho na mwili au 'dhambi ikaayo ndani.' Wasio Wakristo wao wako 'katika mwili' tu, hivyo Roho wa Mungu haamshi migogoro ya aina hiyo ndani yao. Kwa hiyo mapambano dhidi ya dhambi huenda ndiyo ishara iliyo wazi kabisa kwamba mtu amebadilishwa! . . . Ndio maana ni lazima tupate uhakika wetu wa wokovu na upendeleo wa Mungu kwetu sisi kimsingi kutoka katika ahadi ambazo tumepewa katika Maandiko, badala ya kujaribu kupata uhakika kutoka katika maendeleo yetu wenyewe katika utakatifu. Baadhi ya wale ambao wameendelea sana katika utakaso kuwazidi wengine ndio hao hao ambao hawaridhishwi na maendeleo ambayo wanayafikia katika maisha yao ya Kikristo. . . . Ingawaje tutakuwa na maendeleo kwa hakika, ni vigumu sana wakati mwingine kuyapima." (Riddlebarger 1998e: 3) John Piper anaongezea, "Migogoro ndani ya nafsi yako si yote ni mibaya. Ingawaje tunaitamani ile siku ambayo mwili wetu utakuwa mfu kabisa na mioyo yetu itajazwa matamanio safi ya upendo tu, hata hivyo kuna kitu ambacho ni kibaya zaidi ya ile vita iliyo ndani yetu kati ya mwili na Roho; ambacho ni, kutokuwa na vita kwa sababu mwili unaendesha ngome na maeneo ya ulinzi. Mungu asifiwe kwa ajili ya vita iliyoko ndani! Kujisikia swari katika dhambi ni mauti. Roho amekusudia kufanya mapambano dhidi ya mwili. Hivyo jipe moyo ikiwa nafsi yako hujisikia kama uwanja wa mapambano wakati mwingine. Ishara ya kwamba wewe unaye Roho si ile hali ya kutokuwa na tamaa mbaya, bali ni ya kuwa uko katika mapambano nazo!" (Piper 1983d: n.p.)

Kuhusiana na mambo yaliyo bayana yahusuyo huu mgogoro wa ndani, **mst. 16-17**, na **24** huzungumza kuhusu "tamaa" za mwili na ule mwili "unavyosababisha tamaa zake" dhidi ya Roho. Yale maneno kwa Kiyunani ni ile nomino *epithumia* na kitenzi *epithumeō,* ambayo mara kwa mara hutafsiriwa kama "tamaa mbaya" kwa kuwa yanamaanisha tamaa yenye nguvu, shauku, uchu, na ashiki (Danker 2000: *epithumeō, epithumia,* 371-72; Zodhiates 1993: *epithumeō, epithumia,* 627). Lile neno "shauku" (Kiyunani = *pathēmasin*) in **mst. 24** ni sawa na *epithumia*. Hii "tamaa mbaya" haimaanishi tu ile hamu ya kufanya tendo la zinaa au tamaaa ya kimwili bali kwa tamaa zote za dhambi za asili yetu iliyoanguka. Matumizi ya maneno haya yako sawa na ile hali ya asili inayotenda kazi, yenye nguvu ya dhambi ikaayo ndani. **Mstari 19-21** hutoa mifano ya hizi shauku na tamaa mbaya. Paulo hatupi orodha yote, iliyokamilika, ya hizo tamaa za mwili bali ni kama mifano inayowakilisha. Fahamu kuwa shauku, tamaa, na ashiki zilizoorodheshwa katika **mst. 19-21**, zinapotenda kazi kikamilifu, matokeo yake ni kuumana na kulana ambako Paulo amekutaja katika **mst. 15**. Fahamu pia kwamba zile shauku na tamaa za mwili wa dhambi hujidhihirisha katika maeneo yote ya mtu, katika utu wa ndani wa mawazo na utu wa nje, wa kimatendo, kingono (uovu, uchafu, ashiki); kidini (ibada ya sanamu, uchawi); kimahusiano (uadui, ugomvi, hasira kali, mabishano, mafarakano, matengano, karamu za ulevi); na kibinafsi (wivu, hudusa, ulevi). Paulo anahitimisha kwamba *"watu watendao mambo ya jinsi hii hawataurithi ufalme wa mbinguni"* (**Gal 5:21**). Lile neno "kutenda" (Kiyunani = *prassontes*) humaanisha matendo yanayofanywa kwa kurudiarudia au kitabia (Zodhiates 1993: *prassō,* 1209). Kwa maneno mengine, maisha ya mtu yana mfumo wa mwenendo wa kidunia wenye ubinafsi; sio maisha ambayo yana misingi katika upendo wa Mungu na ule upendo wa mmoja kwa mwingine. Kama ambavyo *"imani itendayo kazi kwa upendo"* (**Gal 5:6**) ni ishara kwamba mtu amezaliwa mara ya pili na yuko ndani ya Kristo, vivyo hivyo maisha ambayo yanaongozwa na *"zile tamaa za mwili"* ni ushahidi kwamba mtu hajazaliwa mara ya pili na hayuko ndani ya Kristo. Ndiyo maana, anapozungumza kuhusu huu mgogoro wa ndani baina ya mwili na Roho katika **Romans 8**, Paulo alisema, *"Kwa kuwa nia ya mwili ni mauti . . . [7] kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haiitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kutii. [8] Wale waufuatao mwili hawawezi kumpendeza Mungu"* (**Rum 8:6-8**).

Mstari 22-26 unapingana na kuruhusu "mwili" utawale mawazo yetu na matendo kwa kutuonyesha upande mwingine wa namna ya kuishi (ano jinsi **mst. 22** tena unaanza na neno "Lakini"). Huku ni *"ku[ishi] kwa Roho"* na *"ku[enenda] kwa Roho"* (**mst. 24**). **Gal 5:6** ilikuwa imekazia umuhimu wa *"imani itendayo kazi kwa upendo."* **Gal 5:14** imejadili hilo kwa kusema, *"Umpende jirani yako kama nafsi yako."* Njia pekee ya kufanya lolote kati ya hayo mambo ni kuishi na kuenenda kwa Roho. Kuishi na kuenenda kwa Roho huhusiana na kuwa na *"tunda la Roho"* (**mst. 22-23**). Paulo anatofautisha wazi wazi lile *"tunda la Roho"* na yale *"matendo ya mwili"* (**mst. 19**): "'Matendo ya mwili' ni kile unachofanya wakati 'unapotaka kutosheleza zile tamaa za mwili.' 'tunda la Roho' ni kile ambacho hutokea katika maisha yako wakati una-'enenda katika Roho.'" (Piper 1981:

[22] Jambo hili halifanani bali ni mfano wa Yesu ambaye alikuwa na asilimbili, ya kibinadamu na kiungu.

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

n.p.) Kuishi na kutembea kwa Roho na kuishi kwa kufuata tamaa za mwili ndio machaguo mawili pekee. Paulo anaonyesha katika **mst. 16** ambapo anasema kwamba tunapotembea kwa Roho *hatutazitimiza* tamaa za mwili (ona pia **Rum 8:1-14**).

Je, kuishi na kuenenda katika Roho ni nini? **Gal 5:18** inazungumzia kuhusu *"kuongozwa na Roho."* Roho anaonekana kimatendo, mwenye kuanzisha; Mkristo hufuata uongozi Wake. **Mstari 17** (ESV) huzungumza kuhusu *"matakwa ya Roho yako kinyume na [matakwa ya] mwili."* Jambo hili huonyesha kwamba Roho ana yale ambayo ni matakwa yake. Roho hupandikiza matakwa yake katika fahamu zetu ili kubadilisha "mioyo" yetu, m.y., "utu wetu wa ndani," ambao ndio sisi hasa. Roho hutenda kazi ili kutubadilisha "uhalisia wa utu wa ndani katika ujumla wake unabainishwa kwa njia ya: yale maarifa na kuelewa uhalisia nilionao; zile imani ninazozishikilia; ule utambuzi, mitazamo, na mwenendo ulio ndani yangu; misimamo ambayo nimeifanya; vile viwango vya kuthamanisha ninavyovisimamia; zile tamaa na shauku ambazo zinanisukuma; na vile vipaumbele ambavyo hupata ndani ya mawazo yangu, mwenendo, vitendo, na tamaa. Kwa kifupi, utu wangu wa ndani ni ujumla wa kila kitu cha maisha yangu ya nafsi na uzoefu." (Crabtree 2001: n.p.) Anaweza kufanya haya moja kwa moja lakini kwa kufanana hasa hufanya hili kwa kupitia uwezo wa neema: Neno la Mungu; Mwili wa Kristo; maombi; na Sakramenti. "Kuenenda kwa Roho ni kushiriki katika ule uwezo wa neema—Neno na Sakramenti—pamoja na mambo kama maombi na ushirika, ambavyo matokeo yake ni kukua kwa neema na ujuzi wa Bwana Yesu Kristo na kuendelea kufananishwa na sura yake." (Riddlebarger 1998e: 2)

Mstari 16 na **25** huzungumza kuhusu "kuishi" na "kuenenda" kwa Roho. Hapa wajibu wa Mkristo umetiliwa mkazo, ikimaanisha, tunapaswa kufuata kimatendo, kutii, na kuishi sawa sawa na imani yetu na tamaa ambazo zimepandikizwa ndani yetu na Roho Mtakatifu. Jack Crabtree anaandika kwa muhtasari, "Shauku tofauti zenye hisia kali ni lazima zitasababisha matendo tofauti yenye hisia kali. Kile Paulo anachomaanisha hapa, kwa hiyo, pale anaposema 'enenda kwa Roho' ni hiki: kuenenda kwa Roho ni ile hali ya kujiendesha mwenyewe kiasi kwamba maisha yako na matendo yako unayaishi kwa kufuata zile shauku na tamaa ambazo Roho wa Mungu amezipandikiza kimiujiza ndani ya moyo (mdhanifu) wa wale ambao ni warithi wa uzima wa milele. Kwa maneno mengine 'kuenenda kwa Roho' ni kujitahidi kuwa mwema kwa kukubaliana na ile njaa na kiu ya kuwa mwema kibinafsi kama vile Roho wa Mungu alivyoumba katika mioyo ya wale Aliowachagua." (Crabtree 2002: n.p.) Au, kama Piper anavyoiweka, "*Kuenenda kwa Roho ni kile tunachofanya wakati yale matakwa yanayozalishwa na Roho yana nguvu kuliko yale matakwa yanayozalishwa na mwili*" (Piper 1981: n.p.).

Ili tuweze kufanya hili, ni lazima tuwe katika uhusiano wa karibu, wa kibinafsi na Mungu ndani ya Kristo, kwa Roho, kwa njia ya imani. Yesu alilizungumza hili katika **Yohana 15:5** ambapo alisema, *"Akaaye ndani yangu nami ndani yake, huyo huzaa sana."* Kwa hiyo, ku "enenda kwa Roho" yamaanisha ile hali ya kuendelea kujiunganisha na Kristo ili kwamba tupokee, tujue na kuyatendea kazi mawazo yake, viwango vyake vya kuthamanisha, mienendo yake, na tamaa ambazo zimepandikizwa ndani yetu na Roho Matakatifu. Matokeo yake ni kwamba tuta *"zaa matunda mengi,"* ambayo ni *"tunda la Roho."* Tunafanya hivi—na kwa njia hiyo Roho anatawala juu ya miili yetu—kwa imani. **Gal 2:20** inasema, *"Uhai nilio nao sasa katika mwili, <u>ninano katika imani ya Mwana wa Mungu</u>, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu."*[23] **Gal 3:5** vivyo hivyo anasema, *"Basi, yeye awapaye Roho na kufanya miujiza kati yenu, je! Afanya hayo kwa matendo ya sheria, <u>au kwa kusikia kutokanako na imani</u>?"* **Gal 5:5** anaongezea, *"Maana sisi <u>kwa Roho tunalitazamia tumaini la haki kwa njia ya imani</u>."* Piper anaiweka hivi: "*Unaenenda kwa Roho wakati moyo wako umeegemea ahadi za Mungu*. . . . Kukaa katika ahadi za Mungu ndio njia ya Roho. . . . Kwa kutafakari juu ya kuaminika na uthamani wa ahadi za Mungu mpaka hapo mioyo yetu itakapo kuwa huru mbali na wasiwasi wote na hatia. Hivi ndivyo Roho Mtakatifu anavyotujaza na kutuongoza. . . . Roho anafanya kazi yake kuu ndani yetu na kupitia sisi kwa kusikia kwa njia ya imani tu. Tunasafishwa kwa imani peke yake. Namna ya kuenenda kwa Roho ili usifanye zile tamaa za mwili ni kusikiliza zile ahadi tamu za Mungu na kuziamini, na kuzifurahia, na kutulia katika hizo." (Piper 1983d: n.p.). anapendekeza hatua zifuatazo ili atusaidie kuenenda kwa Roho tukiwa tunajielewa na kujua kwamba tunafanya hivyo: (1) *Tambua* kwamba sisi hatuwezi kufanya lililo jema bila ya kuwezeshwa na Roho Mtakatifu; (2) *Omba* kwamba Mungu atatufanya kuujua uongozi wa Roho na kuenenda katika njia zake; (3) *Tegemea* kwa imani kwamba Roho kwa kweli atatuokoa kutoka katika nguvu ya dhambi kama alivyoahidi na atatenda kazi ndani yetu na kupitia sisi sawa sawa na mapenzi yake; (4) *Tenda* kwa namna ile ambayo unajua kwamba ni sawa; na (5) *Mshukuru* Mungu kwa kila ubora ulioupata au tendo lolote jema lililofanyika. (Piper 1981: n.p.) Kwa kutulia katika ahadi za Mungu na kufanya mambo haya tunaweza kuwa na uhakika kwamba tunaenenda kwa Roho.

[23] Tambua kwamba lile neno "mwili" katika mstari huu halimaanishi ule utu wa kale, wa asili ya dhamba bali mwili wake.

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

Maeneo mengine mawili ya kuenenda kwa Roho inabidi yatajwe:

- Kwanza, **mst. 24** unasema kwamba *"hao walio wa Kristo wameusulibisha mwili pamoja na mawazo yake mabaya na tamaa zake."* **Gal 2:20** ilishasema, *"Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena bali Kristo yu hai ndani yangu."* Tofauti ni kwamba **Gal 2:20** inazungumzia kuhusu kile kinachotokea tunapomjia Kristo kwa imani. Utu wetu wa kale umesulibiwa pamoja na yeye (**Rum 6:5-6**), tunmezikwa pamoja naye (**Rum 6:4**), na tumefufuliwa pamoja naye kwenye maisha yetu mapya ndani yake (**Rum 6:8, 11; Efe 2:5-6**). Sasa tukiwa tumo ndani ya Kristo, sisi sio ambao tunasulibishwa (hali tukiwa hatufanyi chochote), lakini sisi wenyewe tuna usulibisha "mwili" (wetu wa kale, asili ya dhambi na nguvu ile ya dhambi iliyomo ndani mwetu). Paulo anaazima kutoka kwa Yesu' matumizi ya tamathali za usemi katika mazungumzo: *"Mtu ye yote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake kila siku, anifuate"* (**Luka 9:23**; ona pia **Math 10:38; 16:24; Marko 8:34; Luka 14:27**). Tunausulibisha mwili kwa kumsikiliza Roho, kumtegemea Roho, na kutii, kuishi, na kuenenda kwa Roho badala ya kusikiliza, kutii na kuenenda kwa kufuata tamaa za mwili. Tunafanya haya siku kwa siku katika maamuzi yetu yote ya kimaadili tunayoyafanya.
- Pili, **mst. 25** unasema, *"Tukiishi kwa Roho, na tuenende kwa Roho."* **Mstari 16** pia ulishasema ku-*"enenda kwa Roho."* Hata hivyo, maneno yaliyotumika kwa "enenda" katika mistari miwili ni tofauti. Lile neno linalotumika kwa kawaida la "enenda" limetumika katika **mst. 16**, lakini katika **mst. 25** lile neno (Kiyunani = *stoicheō*) huzungumza kuhusu "kuchukuliwa katika mkondo fulani" au "kushikilia kwenye, kukubaliana na, kufuata au kupatana na mtu au kitu ambacho kinakubalika kama kipimo cha mwenendo wa mtu" (Danker 2000: *stoicheō,* 946). Crabtree anadokeza kwamba ku-"enenda kwa Roho" kunaweza kutafsiriwa "enenda kwa mwafaka na zile tamaa ambazo Roho anazitengeneza ndani ya wale Aliowachagua" (Crabtree 2001: n.p.).

"Kuusulibisha mwili" na "kuenenda pamoja au na mwafaka na Roho" ni kama pande mbili za toba: tunageuka *kutoka* katika mabaya na kugeuka *kuelekea* mema. Yote ni muhimu. Hivyo, tunahitaji kuwa wasio na huruma ("sulibisha"!) katika kugeuka kutoka katika dhambi na uovu wakati wowote ule shauku zetu, tamaa na vishawishi vinapoinua vichwa vyao vibaya. Vile vile, ni lazima tuwe na nidhamu katika kumfuata Roho. Tunahitaji *"kufikiri"* mambo ya Roho (**Rum 8:5-6**), *"yatafuteni yaliyo juu"* (**Kol 3:1-2**), na *"yatafakarini haya"* (**Filp 4:8**). Tunahitaji kudumu katika kutumia njia ya neema kama vile kujifunza Neno, maombi, na kanisa. Kwa kifupi, Roho anataka kutawala maisha yetu yote—muda wetu, pesa, kile tunachosoma na kuangalia, mahusiano yetu na wengine, n.k. Kwa njia hii, *"hatutatimiza tamaa za mwili"* (**Gal 5:16**).

Maeneo mengine mawili ya *matokeo* ya kuenenda kwa Roho inabidi pia yatajwe:

- Kwanza, **Gal 5:18** inasema, *"Mkiongozwa na Roho, hampo chini ya sheria"* (ona pia **Gal 5:23**). Huu waraka wote umekuwa mjadala dhidi ya wale ambao wangeuweka Ukristo chini ya sheria. Hapo awali, Paulo alidokeza kwamba, ndnai ya Kristo, sisi hatuko tena chini ya laana ya sheria kwa sababu *"Kristo . . . alifanyika laana kwa ajili yetu"* (**Gal 3:13**), na hatutumikishwi tena na sheria kwa sababu Kristo ametuweka sisi huru (**Gal 5:1**). Hapa Paulo amekuwa akizungumzia kuhusu *"kuenenda kwa Roho"* dhidi ya kutimiza *"tamaa za mwili."* Katika **mst. 17** mtu wa mwilini anataka kuyafanya matendo ya mwili, lakini sheria inapinga na kuzuia hilo *"hata hamwezi kufanya mnayotaka."* Hata hivyo, sheria haipingani na kile ambacho mtu "*anayeongozwa na Roho*" hutamani kukifanya, hivyo mtu anayeongozwa na Roho anaweza kufanya *chochote atakacho* (m.y., *"juu ya mambo kama haya hakuna sheri,"* **mst. 23**). Sababu ni kwamba Roho huingiza ndani "shauku na matamanio" mapya ndani ya mioyo yetu na, *ili mradi tu mtu anamtii na kumfuata Roho*, hizo shauku na matamanio mapya vyote vitakuwa ni kwa ajili ya kumwinua Mungu.
- Pili, lile *"tunda la Roho,"* ambalo ni matokeo ya kuishi na kuenenda kwa Roho, ni umoja ingawa lina vipengele mbalimbali. Hii huonyesha hali ya umoja katika kusudi na mwelekeo wa maisha ya mtu, ambayo humtukuza Mungu ndani ya Kristo (**Yohana 16:14-15**; ona **1 Kor 6:20**). Matumizi ya umoja pia huonyesha kuwa tunda lote kwa pamoja hukua pamoja na hivyo lote linapaswa kuonekana wakati mtu anapokua katika Kristo. Kila kipengele cha tunda kinajitegemea. Ule ukweli kwamba tunda la Roho huongozwa na upendo hudokeza kwamba tunda jingine (furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi) huuelezea upendo au maisha anayoishi mtu kwa *"imani itendayo kazi kwa upendo."* Kwa hakika, kule kukua kwa pamoja kwa kila kipengele cha tunda ni ishara kwamba ni vya Roho. Kwa upande mwingine, mtu asiyeongozwa na Roho anaweza kuwa na baadhi ya sifa hizi (mfano, amani, au furaha) kutoka katika tabia zake za asili au juhudi lakini wakati huo huo akatambulika kuwa yu ana kiburi au hasira au tamaa mbaya au kukosa kiasi. Ndiyo maana Yesu alisema kwamba mti unajulikana na kuhukumiwa kwa matunda yake (**Math 7:16-18; 12:33; Luka 6:43-45**).

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

Matumizi ya neno "tunda" ni mfano wa kukua kwa mmea. Hilo hudokeza kwamba kukua na kuwa kama Kristo, kama mti au mmea, ni jambo linalofanyika kwa hatua, lakini kukua huko kutakuwa kusikoepukika. Zaidi ya hayo, tunda la Roho ni la milele—vile vipengele vya tunda ni badiliko la moyo na mwenendo wa mtu. Lakini hata kama ni vya milele vitasababisha kuleta mabadiliko ya nje ya tabia ya mtu katika maeneo yote ya maisha. Hivyo, kama vile *"matendo ya mwili"* yanavyohusisha na kuathiri maeneo yote ya maisha, vivyo hivyo pia *"tunda la Roho"* huhusisha na kuathiri maeneo yote ya maisha. Hata hivyo, matokeo ya hayo mawili, yote ndani ya mtu na miongoni mwa watu, yatakuwa tofauti kabisa.

Hatimaye, **mst. 25-26** hutupa muhtasari unaohitimisha kifingu hiki kidogo chote. **Mstari 25** unatuambia kwamba *"tukiishi kwa Roho,"* m.y., ikiwa tumebadilishwa, tumehesabiwa haki, na kupokea maisha yetu mapya kwa njia ya Roho, hivyo yatupasa *"kuenenda kwa Roho,"* m.y., kusikia, kuelewa, kutii na kukiishi kile ambacho Roho anatuambia. Katika **mst. 26** Paulo anatofautisha hili na "kujisifu, kushindana na kuoneana wivu" kati ya mtu na mwingine. Mambo haya yote hutuweka sisi wenyewe kuwa katika kiini, ama kwa kujiinua wenyewe (kujisifu), kuwapinga wengine (kushindana), au kutaka kuwa kama wengine (kuona wivu). Au kulifikiria hilo kwa namna nyingine, kwa kujisifu au kushindana tunajifikiria sisi wenyewe kuwa *bora* kuliko wengine, lakini kwa kuona wivu tunajifikiria kuwa sisi tuko *vibaya* kuliko wengine. Kwa njia ye yote ile ambayo mtu atalitazama, Roho Mtakatifu hawi kile kiwango ambacho sisi twataka kukikubali, kukifuata na kukitii. Mtu ananyeenenda kwa Roho hashawishiwi na hisia za kuwa juu ya au chini ya bali hafanyi *"lolote kwa majivuno, bali kwa unyenyekevu, [wa]anamhesabu mwenzake kuwa bora kuliko nafsi yake"* (**Filp 2:3**). Wakati **mst. 19-21** huenda umetoa mifano zaidi ya picha ya *"matendo ya mwili"* kuliko unavyofanya **mst. 26**, kujisifu, kushindana, na wivu hudhihirisha kwamba *"tamaa za wmili"* zinaweza kuwa ngumu sana kuzieleza. Tunaweza kujaribu kutetea mambo haya. Kwa kweli, labda tuwe makini sana twaweza pia tukashindwa kuona kwamba tumeanguka na kuwa mawindo ya tamaa za mwili. Maisha yetu ni mapambano ya kiroho. Njia pekee itakayotufanya tushinde ni kwa kumtegemea Roho Mtakatifu siku kwa siku.

- **<u>6:1-10—</u>**<u>Matumizi yaliyo bayana ya *"imani itendayo kazi kwa upendo"* na *"kuenenda kwa Roho."*</u>

Wakati ambapo tunda la Roho (**Gal 5:22-23**) ni *matokeo* yaliyo bayana ya kuenenda kwa Roho, yaliyobaki katika mjadala wa Paulo wa "*imani itendayo kazi kwa upendo*" na "*kuenenda kwa Roho*" zimekuwa ni kanuni za kiujumla. Alitoa mifano bayana ya *"matendo ya mwili"* ni yepi katika **Gal 5:19-21** na **26**. Mfano pekee ulio bayana alioutoa mapema unaohusu "*imani itendayo kazi kwa upendo"* na *"kuenenda kwa Roho"* ulikuwa kuwakumbuka maskini (**Gal 2:10**). Na sasa Paulo anatoa mifano bayana ya *"imanai itendayo kazi kwa upendo"* na *"kuenenda kwa Roho."*

- **<u>6:1-5—</u>**<u>Mchukuliane mizigo.</u>

[1] Ndugu zangu, mtu akighafilika katika kosa lolote, ninyi mlio wa Roho mrejezeni upya mtu kama huyo kwa roho ya upole, ukijiangalia nafsi yako usije ukajaribiwa wewe mwenyewe. [2] Mchukuliane mizigo na kuitimiza hivyo sheria ya Kristo. [3] Maana mtu akijiona kuwa ni kitu, naye si kitu, ajidanganya nafsi yake. [4] Lakini kila mtu na aipime kazi yake mwenyewe, ndipo atakapokuwa na sababu ya kujisifu ndani ya nafsi yake tu, wala si kwa mwenzake. [5] Maana kila mtu atalichukua furushi lake mwenyewe.

Mstari 1 unapingana na tabia ya kujigamba, majivuno, na wivu iliotajwa katika **Gal 5:26** na kutaja mwitikio ulio sahihi ambao Wakristo wanapaswa kuwa nao wakati wengine wanapotenda dhambi, ikimaanisha, kumrejeza mtu kama huyo katika roho ya upole.[24] Hili hutiririka kimatiki na kiasilia kutoka katika injili ya neema sio matendo ambayo Paulo ameielezea katika waraka huu wote: "Wakristo ambao huenenda kwa Roho wanapaswa kuwa radhi kuwasaidia wale ambao wanashindana na dhambi kwa kuwa wao, miongoni mwa watu wote wanapaswa kuelewa kwamba ikiwa Mungu alikuwa mwenye neema kwao, na kuwaita kwenye imani ndani ya Yesu Kristo ingawaje walikuwa wenye dhambi wasiostahili, hivyo, na wao pia, wanapaswa kuwa na neema kwa wengine ambao wameitwa na Kristo katika ufalme wake wa neema kwa njia ya injili ya Kristo aliyesulibiwa." (Riddlebarger 1998f: 2) Kwa kweli, tunavyowachukulia wengine (hasa hasa Wakristo wengine)

[24] Mstari unasema kwamba wale ambao ni "wa rohoni" wamrejeshe mtu huyo. "Hilo humaanisha kwamba unapaswa 'kuongozwa na Roho' (5:18), 'kuenenda kwa Roho' (5:16, 25), 'kuzaa matunda ya Roho' (5:22). Haimaanishi Ukristo wa ngazi ya juu, bali maisha ya Kikristo ya kawaida yaliyojaa Roho. Watu wa Rohoni ni watu wa kawaida ambao humtegemea Roho asiye wa kawaida." (Piper 1983e: n.p.)

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

wanaotenda dhambi hudhihirisha kama sisi tunaielewa injili au la.

Hili linaweza kuwa tatizo kubwa katika makanisa mengi. Mara nyingi, kimbilio la kwanza (badala ya kuwa kimbilio la mwisho) la viongozi wengi wa makanisa ni kwatenga watu ambao wametenda dhambi fulani (kama vile kupata mimba nje ya ndoa). Maadili ya kanisa lazima yazingatiwe, lakini mara nyingi mwenendo wa viongozi wa kanisa ni wa kutokusamehe na wenye ukali badala ya huruma na upole. Mara nyingi hawaonyeshi tunda la Roho au kutambua kwamba mtu yule aliyetenda dhambi anaweza kuhitaji msaada ambao mahali pekee unapoweza kupatikana ni katika familia ya kanisa lenye upendo. Lengo lao sio kurejesha, bali kuadhibu.[25]

Inafurahisha kwamba katika **mst. 1** Paulo anatumia maneno *"mtu huyo"* kwa ajili ya mtu aliyetenda dhambi. Anayatumia maneno hayo katika maeneo mengine mawili katika AJ akimzungumzia mtu ambaye ametenda dhambi kubwa, yule mwanaume katika **1 Kor 5:1** ambaye amekuwa akilala na mke wa baba yake. Kanisa la Korintho halikutaka kufanya chochote kuhusiana na tatizo hilo, kwa hiyo katika **1 Kor 5:5** Paulo alisema, *"Nimeamua kumtolea Shetani mtu huyo, ili mwili uadhibiwe, ili na Roho iokolewe katika siku ya Bwana Yesu."* Ona hapa kusudi kubwa la "kumtoa mtu huyu kwa shetani" (m.y., kumtenga) lilikuwa ni la namna ya kurejesha: *"ili na Roho yake iokolewe katika siku ya Bwana Yesu."* Mtu yule bila shaka alitubu na kuzaa matunda ya toba ya kweli kwa sababu **2 Kor 2:6-8** inatueleza, *"[6] Yamtosha mtu wa namna hii adhabu ile aliyopewa na walio wengi; [7] hata kinyume cha hayo, ni afadhali mmsamehe na kumfariji, mtu kama huyo asije akamezwa katika huzuni yake ipitayo kiasi. [8] Kwa hiyo nawasihi kumthibitishia upendo wenu."* Kwa maneno mengine, kule kuadibisha kulipata matokeo yaliyokusudiwa, hivyo Paulo anasema kwamba kanisa limrudishe katika ushirika, na kumsamehe na kumtia moyo, na kumthibitishia upendo wao kwake.

Mstari 1 na **4** inatusihi kila mmoja wetu *"kujiangalia nafsi zetu wenyewe, tusije tukajaribi"* pia *"na kuipima kazi yake."* Kwa kuwa hili liko katika muktadha wa dhambi na majaribu, kile ambacho Paulo anakifanya ni kurudia kuisema ile kanuni ya Yesu katika **Math 7:2-5** that *"hukumu ile mhukumuyo, ndiyo mtakayohukumiwa; na kipimo kile mpimiacho, ndicho mtakachopimiwa. [3] Basi, mbona wakitazama kibanzi kilicho ndani ya jicho la ndugu yako, na boriti iliyo ndani ya jicho lako mwenyewe huiangalii? [4] Au utamwambiaje nduguyo, Niache nikitoe kibanzi katika jicho lako; na kumbe! Mna boriti ndani ya jicho lako mwenyewe? [5] Mnafiki wewe, itoe kwanza ile boriti katika jicho lako mwenyewe; ndipo utakapoona vema kukitoa kile kibanzi katika jicho la ndugu yako."*

Mstari 2 unaendelea na kujenga hoja zaidi juu ya wazo la **mst. 1** wakati unapotuambia kwamba *"mchukuliane mizigo, na kuitimiza hivyo sheria ya Kristo."* Mzigo ni "chochote kile ambacho kinatishia kuiporomosha ile furaha ya imani yetu—iwe ni sikitiko ambalo linatishia kutufanya sisi tuutilie mashaka wema wa Mungu [mfano, ugonjwa, au kukosa ajira, ao kufiwa na yule umpendaye, au upweke, au kukataliwa], au dhambi ambayo inatishia kutukokota katika hatia na hukumu" (Piper 1983e: n.p.). Kuchukuliana mizigo tena ni matokeo ya kawaida na kimantiki yatokanayo na injili na asili ya kanisa. Ndiyo matokeo ya kawaida na kimantiki yatokanayo na injili kwa kuwa Kristo ameuchukuwa mzigo wetu—ule mzigo wa dhambi yetu pamoja na aibu yake na hatia na adhabu ambayo kamwe hatungeweza kuilipa. Dhabihu yake kwa ajili yetu ni mfano wetu wa namna tunavyopaswa kuwatendea wengine. Kama alivyosema katika **Yohana 13:34-35**, *"[34] Amri mpya nawapa, Mpendane, Kama vile nilivyowapenda ninyi, nanyi mpendane vivyo hivyo. [35] Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi."* Kuchukuliana mizigo pia ni matokeo ya kawaida na kimantiki ya asili ya kanisa. Waamini wote wameasiliwa katika familia ya Mungu (**Rum 8:15, 23; 9:4; Gal 4:5; Efe 1:5; 2:19**). Kwa hiyo, kanisa ni familia (**Math 12:49-50; 2 Kor 6:18; Gal 6:10; Efe 2:19; 1 Tim 3:15; 5:1-2; Ebr 3:6; 1 Pet 4:17**). Dhati Lewis anaiweka namna hii, "Kanisa si *kama* familia; *ni* familia. . . . Jambo hili linaweza kuonekana katika ukweli kwamba neno *mwanafunzi*, ambalo lilitumika sana katika nyakati za awali za Agano Jipya, linapotea baada ya kitabu cha Matendo. Nafasi yake inachukuliwa na neno *ndugu* katika sehemu ya Biblia iliyoendelea." (Lewis 2015: n.p.) Kwa kweli, kanisa kama familia au watu walio katika nyumba moja ni moja kati ya utambulisho wa kanisa ulio katika kiwango cha juu sana katika AJ. Umuhimu wa hili ni kwamba *wanafamilia huhudumiana*. Tunahitaji kujiuliza, "Je ninamuona kaka na dada yangu ndani ya Kristo kama kaka na dada *halisi*" na "Je watu wote ndani ya kanisa letu hujisikia kama wao ni wapendwa na washiriki wa familia yenye upendo na kujali?" Kwa kifupi, tunawatendea kaka na dada zetu ndani ya Kristo kwa upendo ule ule, kujali na *kimatendo* katika kuchukua mizigo yao kama ambavyo tungewatendea kaka na dada wa kidunia?

Katika **mst. 2** Paulo anazungumza kuhusu *"sheria ya Kristo."* Hii na **1 Kor 9:21** ndiyo mahali pekee penye matumizi bayana ya kifungu hicho cha maneno katika AJ. Hata hivyo, *"sheria ya Kristo"* inajitokeza bila kutajwa katika AJ yote NT. "Sheria ya Kristo" si tu kwamba ni mafundisho ya Yesu bali pia mafundisho ya

[25] Kanuni za kuadibisha ndani ya kanisa zimejadiliwa katika Menn 2017: 9-12. Kanuni na mwongozo wa kiutendaji wa msamaha na upatanisho zimeonyeshwa katika Menn 2007-2017.

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

waandishi wa AJ (ona, mfano, **Yohana 14:24-26; 16:12-15; 17:8, 18-20; 1 Kor 14:37; Gal 1:11-12; Efe 2:20; 1 Thes 2:13; 2 Thes 2:15; 3:6, 14; Ebr 2:3; Ufu 1:11**). Sheria ya Kristo inahusisha "kanuni za kiujumla na pia maagizo yaliyofafanuliwa zaidi" (Moo 1984: 30). Hii si "mkusanyiko wa sheria uliopangwa kwa mfumo maalumu au mtiririko wa amri na makatazo, bali ni mkusanyika wa mafundisho ya mitume na uongozi wenye ushawishi wa Roho Mtakatifu. Upendo ndicho kiini kwa sheria hii, na kuwa ni muendelezo wenye nguvu wa sheria ya Musa, kwa wengi kwa kuainisha sheria za Musa zinachukuliwa na kuingizwa katika 'sheria ya Kristo.' . . . Pia linajitokeza katika ule muktadha ([Gal] 5:16-26) ambao ni wa Roho Mtakatifu kusababisha uzalishaji wa tunda. Pamoja na hayo ule umuhimu wa Roho katika mafundisho ya Paulo kuhusiana na maana ya kuishi kama Mkristo, hili husisitiza kwa nguvu kwamba ushawishi wa uongozi wa Roho ni kipengele muhimu cha sheria hii ya Kristo." (Moo 1993: 368-69) Kwa kifupi, "Sheria ya Kristo si kwamba haiko wazi au dhahiri. Imewekwa wazi katika kuarifu na ule umuhimu, ambao unapewa usemi thabiti katika mafundisho ya kimaadili ya Yesu (mfano, ile Hotuba ya Mlimani) na katika nasaha sa kitume za kuishi kwa kwenda sawa na muungano wetu na Kristo (mfano, Efe. 4-6; Kol. 3, n.k.)." (Irons 2002: n.p.)

Sheria ta AK kamwe haingeweza kufanya kile ambacho Yesu na sheria ya Kristo vinaweza kufanya (**Gal 2:16; 3:2-5, 11, 21**; ona also **Matendo 15:10-11; Rum 8:1-4**). "Ule mkusanyiko wa sheria zilizopangwa haukuweza kusababisha mtu kupata haki, na kwa kweli ulichochea dhambi tu na kusababisha mauti (Rum. 7:5, 8-10; 2 Kor. 3:6)" (Ibid.). Yesu peke yake ndiye aletaye "uzima" (**Yohana 3:36; 4:14; 5:24; 6:40, 68: 10:10; 11:25; 14:6; 20:31**). Alisema kwamba ikiwa tuta "kaa" au "tutaendelea ndani ya" neno lake, basi *"mtaifahamu kweli, na hiyo kweli itawaweka huru"* (**Yohana 8:31-32**). Neno lake hutubadilisha kutoka "ndani-nje" kuwa katika sura ya Kristo mwenyewe (ona **Rum 8:29; 12:2**). John Piper anaiweka hivi, "Musa alitupa sheria lakini hakuweza kuibadilisha mioyo yetu ili kwamba tuweze kutii bila shida. Kiburi chetu na uasi havikuchukuliwa mateka na Musa. Lakini pale Kristo anapotuita sisi kuitii sheria yake ya upendo, anajitoa yeye mwenyewe kwetu kumchinja yule joka wa kiburi chetu, kubadilisha mioyo yetu, kututia nguvu kwa Roho wake, na kuitimiza sheria yake." (Piper 1983e: n.p.) Kwa hiyo, "Pale waandishi wa Agano Jipya walipokabiliwa na maswala ya kimaadili katika makanisa mbali mbali ambayo waliyaandikia, ingalikuwa ni rahisi sana kuziendea Amri Kumi. Hilo silo walilolifanya. Hebu tutamke ukweli huu kama sheria ya dole gumba: msingi wa kufanya maamuzi ya kimaadili katika Agano Jipya si Musa katika mlima Sinai bali Kristo wa Kalvari. . . . Katika kutatua matatizo ya kimaadili, kwa hakika maswala yote ya kufanya maamuzi (ya kimaadili au mengineyo), swali ambalo tunapaswa kujiuliza sisi wenyewe ni, 'Ni mwenendao gani wa kimatendo au kitabia unakubaliana na injili?'" (Goldsworthy 2000: 96) Hivyo, kuongozwa na, kuishi ndani ya, na kuenenda kwa Roho Mtakatifu ni kutii na kuitimiza sheria ya Kristo.

Mstari 3-4, kama ile sehemu ya mwisho ya **mst. 1**, inakazia kujitathmini. **Mstari 3** unamaanisha kwamba baadhi yetu hatutaki kuchukuwa mizigo ya wengine kwa sababu tunafikiri tuko juu ya hali hiyo na hatutaki kujishusha ili tuwasaidie wengine (hasa hasa wengine ambao wako katika mtego wa dhambi). Kile ambacho **mst. 1, 3-4** unakisema ni "Usijilinganishe na wengine; jilinganishe na Kristo tu." Injili inadhihirisha kwamba sisi hatuna uwezo wowote na sio bora kuliko wengine. Kwa sababu ninajua kwamba bila ya Kristo siwezi kufanya kitu *chochote* (**Yohana 15:5**), ninaweza kuibeba mizigo ya wengine kwa uhuru, bila ya kujionyesha kuwa mimi ni bora, bila majivuno, katika roho ya upendo na huruma.

Inaweza kuonekana kwamba kutajwa kwa "kujisifu" katika **mst. 4** kunakinzana na **Gal 5:26** ambayo inasema hatupaswi kuwa watu wa kujifisu. Hilo si sahihi. Dokezo lililo katika **mst. 4** si kujilinganisha wewe mwenyewe na wengine, kitu ambacho kinaweza kupelekea kujisifu ikiwa utafikiri kwamba wewe u bora kuliko wengine. Badala yake, jitazame wewe na kisha umtazame Kristo. Ukifanya hivyo, utaona kuwa sababu yako pekee ya kujisifu iko *"katika msalaba wa Bwana Yesu Kristo"* (**Gal 6:14**; ona pia **Rum 15:17-18; 1 Kor 1:31**). Vivyo hivyo, **mst. 5** (*"Maana kila mtu atalichukuwa furushi lake mwenyewe"*) haukinzani na **mst. 2** (*"Mchukuliane mizigo"*). **Mstari 5** unazungumzia kuhusu hukumu. Sisi wote tumewekwa katika mazingira fulani na kupewa majukumu fulani katika maisha haya. Tutatakiwa kutoa hesabu mbele za Mungu siku ya hukumu kwa kile tulichokifanya. Hatuwezi kuhamisha hesabu yetu kwa watu wengine. Katika **mst. 2** "Wakristo wanaagizwa kusaidiana kubeba chini ya mabadiliko ya maisha. Katika [**mst. 5**] Wakristo wanaambiwa kwamba kila mtu atimize majukumu yake ya maisha yampasayo; hawana haki ya kukwepa, tarajia wengine kuyatimiza." (Zodhiates 1993: *phortion,* 1452) Kwa hahika, ikiwa "*tutachukuliana mizigo*" sasa kwa hiari na kwa furaha, basi tunaweza kuingojea kwa hamu hukumu kwa sababu tumekuwa "watumwa wema na waaminifu" (**Math 25:21, 23**) ambao wame *"itimiza ile sheria ya Kristo."*

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

- **6:6-10—**Unavuna kile upandacho, hivyo na tuwatendee watu wote mema kwa namna tunavyoweza.

> ***6 Mwanafunzi na amshirikishe mkufunzi wake katika mema yote. 7 Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi; kwa kuwa cho chote apandacho mtu, ndicho atakachovuna. 8 Maana yeye apandaye kwa mwili wake, katika mwili wake atavuna uharibifu; bali yeye apandaye kwa Roho, katika Roho atavuna uzima wa milele. 9 Tena tusichoke katika kutenda mema; maana tutavuna kwa wakati wake, tusipozimia roho. 10 Kwa hiyo kadiri tupatavyo nafasi na tuwatendee watu wote mema; na hasa jamaa ya waaminio.***

Kanuni kuu ya maelekezo katika kifungu hiki kidogo ni *"cho chote apandacho mtu, ndicho atakachovuna"* (**mst. 7**). Kanuni hii ni muhimu sana kiasi kwamba Paulo anaitangulizia amri (*"Msidanganyike"*) na kauli (*"Mungu hadhihakiwi"*). Kanuni hii inapatikana katika Biblia yote (ona, mfano, **Ayu 4:8; Mith 1:31; 11:18, 25; 14:14; 21:13; 22:8; Yer 17:10; Hos 8:7; 10:12-13; Marko 4:24; Luka 6:37-38; 2 Kor 9:6; Efe 6:8; Yak 3:18**). Iko sambamba na kauli ambayo imerudiwa kwamba Mungu anawahukumu watu na mataifa na huwalipa "sawa sawa na matendo yao [au "njia" au "kazi"]" (**Wamz 1:6-7; 9:22-24, 56-57; 2 Sam 12:9-12; 1 Falm 2:32-33; 1 Falm 20:35-42; 1 Falm 21:17-19; 2 Chron 6:23, 30; Ayu 34:11; Zab 18:24; 31:23; 62:12; Mith 24:12; Mhu 12:13-14; Isa 59:18; Yer 17:10; 25:14; 32:19; Ezek 7:3, 8-9, 20, 23-24, 27; 9:10; 11:21; 16:43, 59; 18:30; 22:31; 24:14; 33:20; 35:6, 11, 15; 39:24; Hos 12:2; Joel 3:5-7; Obad 15; Zek 1:6; Math 16:27; 25:14-30; Luka 12:47-48; Yohana 5:28-29; Rum 2:1-6; 12:19; 1 Kor 3:8, 11-15; 2 Kor 5:10; 11:15; Gal 6:7-8; Efe 6:8; Kol 3:25; 2 Tim 4:14; Ebr 10:26-27; 1 Pet 1:17; 2 Pet 2:20-22; Yuda 14-15; Ufu 2:23; 14:13; 20:11-13; 22:12**). Kanuni hii inahusiana na swala la msingi linaloonekana katika waraka huu tangu hapo nyuma, ambalo ni, wokovu kwa neema kwa njia ya imani ikipingana na wokovu kwa amri, sheria na matendo. Sababu ya hili ni: "Matendo ni kielezo cha hali ya kiroho ya moyo wa mtu. . . . Hata hivyo hukumu haiko katika kutafuta uwiano kati ya matendo mema na matendo mabaya. Badala yake, matendo yanaonekana kama ushahidi usio na makosa wa uaminifu wa moyo; yanadhihirisha kuamini au kutoamini, uaminifu au kutokuwa na uaminifu. Hukumu inadhihirisha kama uaminifu wa watu umekuwa kwa Mungu na kwa Mwana Kondoo au kwa maadui wa Mungu." (Ngundu 2006: 1576)

Mistari hii inatumia kanuni ya kupanda na kuvuna katika maeneo matatu: Huduma ya Kikristo (**mst. 6**); Utakatifu wa Kikristo (**mst. 8**); na utumishi wa Kikristo (**mst. 9-10**):

- Huduma ya Kikristo. **Mstari 6** unasema kwamba kanisa lina wajibu wa kutoa vitu kwa wale ambao wanalilisha kiroho (ona pia **Math 10:9-10; Luka 10:7; 1 Kor 9:7-14; Rum 15:27; 1 Tim 5:17-18**). Umuhimu wa wajibu wa kanisa kuwapatia mahitaji viongozi wazuri unaonekana katika **1 Tim 5:18**, ambayo inamnukuu Musa (ona **Kumb 25:4**) na Yesu (ona **Math 10:10; Luka 10:7**). AJ halisemi kiwango au njia fulani bayana ambayo kanisa linapaswa kuitumia katika kumlipa mchungaji. Kutokana na **1 Tim 5:18** *kiwango* cha fidia kwa sehemu kinategemea jinsi yule kiongozi wa kanisa anavyoitenda kazi yake (m.y., *"atawalaye vema"* and *"mchapakazi"*), lakini itatofautiana kati ya mahali pamoja na mahali pengine kwa kutagemea na mazingira ya mahali husika. Hili linaweza kupelekea matumizi mabaya kwa viongozi wa kanisa na wale washirika pia: viongozi wa kanisa wanaweza kuwa wenye tamaa, wanaolipwa zaidi na wavivu; washirika wanaweza kuwa wachoyo na wenye madai mengi. Kwa hiyo, ni muhimu kwa viongozi wa kanisa na washirika kuona kwa pamoja, kuwa na ile *"nia ya Kristo"* (**1 Kor 2:16**), na kuongozwa na kuenenda kwa Roho.
- Utakatifu wa Kikristo. **Mstari 8** unawekea nyama ile kanuni ya kupanda na kuvuna, kwa upande hasa na chanya. "Kupanda katika mwili" ni kutendea kazi zile "tamaa za mwili" kama ilivyojadiliwa katika **Gal 5:16-21**; "kupanda katika Roho" ni kuongozwa, kuishi, na kuenenda kwa Roho kama ilivyojadiliwa katika **Gal 5:16-18, 22-25**. Mstari huu unadokeza kwamba *wakati wote* sisi tunapanda ama kwa mwili au kwa Roho. Katika maisha hakuna kisichofungamana na upande fulani. Swala si tu kule kufanya matendo mema dhidi ya matendo mabaya. Zile *nia* zinazosababisha kufanya yale tunayoyafanya ni za umuhimu mkubwa. Kumbuka kile John Piper alichosema hapo awali: jambo lililo muhimu zaidi "si hasa kile ambacho unakifanya kama ambavyo ni kwa roho gani unafanya kile unachokifanya. Kutahiriwa kunaweza kuwa 'tendo la sheria' [**Gal 2:1-5**] au tendo la upendo ambalo linatiririka kutoka katika imani [**Matendo 16:3**]. Kujiweka wewe mwenyewe chini ya masharti ya chakula inaweza kuwa 'tendo la sheria' [**1 Kor 8:7**] au tendo huru la upendo ambalo linatiririka kutoka katika imani [**Rum 14:21; 1 Kor 8:13**]. Kufundisha Shule ya Jumapili, kuhubiri, kupinga utoaji-mimba, migomo, maandamano ya kupinga nguvu za nyukliya, kujihusisha katika uchangaji na kutoa chakula jijini, ajira yako—haya yote *yaweza* kuwa 'matendo ya sheria' ambayo tunafanya kwa nguvu zetu, ili kuupata upendeleo wa Mungu [m.y., 'kupanda kwa mwili'],

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

au yanaweza kufanywa kwa hali ya unyenyekevu kwa kuitegemea ile nguvu ambayo Mungu anatupatia bure ili kwa kila kitu yeye awe ndiye mwenye kutukuzwa [m.y., 'kupanda katika mwili']. Ule uamuzi wa laana au baraka unategemea ile *namna* ambayo wewe unatii [au, mtu anaweza kusema, *kwa nini* unatii] na ni nani anayepata sifa." (Piper 1983a: n.p.) Kwa kusema hayo ikiwa mtu atapanda katika Roho mtu *"atavuna uzima wa milele,"* **mst. 8** unadokeza kwamba kwa namna ile mtu anavyoishi kuna *matokeo ya milele*, si matokeo katika maisha haya hapa duniani. Wakristo wanahitaji kujua hili. "Kilicho hatarini katika kifungu hiki ni uzima wa milele; sio tu kutakaswa, bali pia wokovu hapo mwishoni. Kama unakwenda mbinguni au kama unakwenda jehanamu inategemea kwa namna fulani kama utazimia moyo katika kufanya mema au hapana." (Piper 1983f: n.p.) Sababu ni kama alivyosema Onesimus Ngundu hapo juu, "Matendo [m.y., vile namna unavyoyoyaishi maisha yako] ni kielezo cha hali ya kiroho ya moyo wa mtu" (Ngundu 2006: 1576).

- Utumishi wa Kikristo. Katika **mst. 9-10** fokasi inahama kutoka katika utakatifu wa binafsi kwenda katika kuwatumikia wengine kwa kuwatendea mema. Hili linaweza kuwa la kuchosha, lakini katika **mst. 9** Paulo anatutia moyo kwa kutukumbusha tena kuhusu ile kanuni ya kupanda na kuvuna: *"tutavuna kwa wakati wake."* Hataji mavuno bayana ambayo tutayavuna: inaweza kuwa katika maisha haya; inaweza kuwa katika uzima wa milele; au inaweza kuwa kote. Anaongezea tahadhari muhimu kwamba tutavuna *"tusipozimia roho."* Hii inakumbushia kile ambacho Yesu alikisema katika **Ufu 2:7, 11, 17, 26; 3:5, 12, 21** anapotoa ahadi kwa yule ambaye "atashinda." Ku- "shinda" maana yake ni kuwa mwaminifu—kupenda na kutumikia—wakati wote hadi mwisho. Ni "pamoja na sasa katika kushinda kwa kuutunza ushuhuda wa kiaminifu wa [kanisa] katika kukabiliana na majaribu (mfano, [Ufu] 2:9-11, 13; 3:8; 12:11); katika kuzishinda nguvu za uovu (mfano, [Ufu] 6:8 ikihusiana na 6:9-11); katika kuitiisha dhambi katika maisha ya washirika wake (ona [Ufu] chaps. 2-3); na katika kuanza kutawala juu ya mauti na shetani kwa kujifananisha na Yesu (cf. [Ufu] 1:5–6, 18). Ustahimilivu wa kanisa, tena, ni sehemu ya mchakato wa ushindi." (White 2000: 175) **Mstari 10** unakumbushia kwamba Wakristo wanahitajika kutumika na kuwatendea watu wote mema, waaminio na wasioamini. Hata hivyo, kwa sababu sisi tu familia (*"jamaa ya waaminio"*) tunapaswa kuwatendea mema hasa hasa kaka na dada katika Kristo (ona pia **1 Thes 3:12**).

MASWALI YA KUJADILI

1. "Uhuru" ndani ya Kristo maana yake ni nini? Uhuru kutoka katika nini? Uhuru kwenda kwenye nini?

2. Je, "haki tuliyohesabiwa" ina maana gani na kwa nini ni muhimu?

3. Watu wengi wanasema wanaamini katika wokovu kwa neema ya Mungu kwa imani lakini wanataabika kufanya matendo ya mwili ili kuupata na kuudumisha upendeleo wa Mungu kiasi kwamba hawapati *uzoefu* wa neema ya Mungu. Tunawezaje kuwasaidia watu kama hao kuelewa kile ambacho wokovu kwa neema kwa njia ya imani humaanisha na wapate uzoefu wa neema ya Mungu wanapoendelea na maisha yao?

4. Elezea asili ya imani ya kweli, iokoayo? Inahusisha nini?

5. Je, upendo unahusianaje na imani?

6. Je, upendo una umuhimu kiasi gani katika Ukristo? Ni kwa nini? Je makanisa yetu na Wakristo duniani kote hutambulika kama mahali na watu wa upendo? Kama sivyo, ni kwa nini? Kama sivyo, ni kitu gani tunaweza kufanya kuhusiana na hili?

7. Je, ile nguvu ya "dhambi ikaayo ndani" ni nini? Tunawezaje kuishinda?

8. Ni kwa nini "kutumikiana kwa upendo" ni uhuru, sio utumwa? Kwa upande mwingine, ni kwa nini kutumikia zile "tamaa za mwili" ni utumwa, sio uhuru?

9. Mtu anapokea nini, na anawekwa huru mbali na nini, anapounganika na Kristo kwa imani?

10. Ni kwa nini ule "mgogoro wa ndani" kati ya mwili na roho katika maisha ya Mkristo ni kitu kizuri?

11. Je, Roho Mtakatifu anatamani kubadilisha nini katika maisha ya Wakristo? Anatumia nini katika kufanya hivyo?

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

12. Je, “kuenenda kwa Roho” ni nini? Tunawezaje kufanya hivyo?

13. Ni kwa nini ni muhimu “tunda la Roho” liwe katika umoja, sio katika wingi, ingawaje “tunda la Roho” lina vipengele mbali mbali tofauti?

14. Ni kwa namna zipi ambazo kwazo sisi kama mtu binafsi na makanisa tunaweza “kuchukuliana mizigo” na kwa njia hiyo kuitimiza sheria ya Kristo?

15. “Kuchukuliana mizigo” ni namna ya kimantiki na ya kawaida ambayo ni matokeo ya ukweli kwamba AJ hulielezea kanisa kama familia, na familia huhudumiana. Je, huwa ninawaona kaka na dada katika Kristo kama kaka na dada *halisi*? Je, Wakristo wengi (na makanisa) huwatendea kaka na dada zetu katika Kristo kwa upendo ule ule, na kuhusika na misaada ya *kimatendo* katika kuchukua mizigo yao kama ambavyo wangewafanyia kaka na dada wa kimwili? Je, watu wote waliomo kanisani hujisikia kama wao ni wapendwa wa familia yenye upendo na kujali? Kama sivyo, ni nini tunaweza kufanya ili kubadilisha mambo ili kwamba, kama watu binafsi na makanisa, tuwe tunaenenda katika Roho kama familia?

16. “Sheria ya Kristo” ni nini?

17. Ni kwa nini ile kauli “Mungu atatuhukumu kwa matendo (au kazi)” inakubaliana na wokovu kwa neema peke yake kwa njia ya imani peke yake badala ya wokovu kwa matendo ya sheria?

18. Kanuni ya “kupanda na kuvuna” inatumikaje katika huduma ya Kikristo, utakatifu wa Kikristo, na utumishi wa Kikristo?

F. <u>Gal 6:11-18—Muhtasari na hitimisho:</u> <u>Wale wanaotaka kutahiriwa ni wanafiki na hawafanyi hayo kutoka katika nia njema kamwe; rehema na neema ya Mungu iwe juu ya wale ambao husikia kutukuka katika msalaba wa Kristo tu.</u>

[11] Tazameni ni kwa herufi gani kubwa nimewaandikia kwa mkono wangu mimi mwenyewe! [12] Wote watakao kuonekana ni wazuri kwa mambo ya mwili, ndio wanaowashurutisha kutahiriwa; makusudi wasiuziwe kwa ajili ya msalaba wa Kristo, hilo tu. [13] Kwa maana hata wao wenyewe waliotahiriwa hawaishiki sheria; bali wanataka ninyi mtahiriwe, wapate kuona fahari katika miili yenu. [14] Lakini mimi, hasha, nisione fahari juu ya kitu chochote ila msalaba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambao kwa huo ulimwengu umesulibishwa kwangu, na mimi kwa ulimwengu. [15] Kwa sababu kutahiriwa si kitu, wala kutokutahiriwa, bali kiumbe kipya. [16] Na wote watakaoenenda kwa kanuni hiyo, amani na iwe kwao na rehema, naam, kwa Israeli wa Mungu. [17] Tangu sasa mtu asinitaabishe; kwa maana nimechukua mwilini mwangu chapa zake Yesu. [18] Ndugu zangu, neema ya Bwana wetu Yesu Kristo na iwe pamoja na roho zenu. Amina.

Maoni ya Paulo katika **mst. 11** kuhusu *“ni kwa herufi gani kubwa nimewaandikia kwa mkono wangu mimi mwenyewe”* yanakubaliana na kile alichokisema katika **Gal 4:15** kuhusiana na namna Wagalatia *“wangeng’oa macho yao, wakampa yeye.”* Ilionyesha kwamba udhaifu wake wa mwili ulikuwa ni tatizo lililohusiana na macho (ambalo linaweza kuwa ndilo *“mwiba katika mwili”* wa Paulo uliotajwa katika **2 Kor 12:7-10**). Kipande kilichobaki cha sehemu hii ya kuhitimisha si tu kinafupisha vipengele muhimu vya kile alichokijadili katika waraka huu wote lakini pia kina taarifa muhimu zinazothibitisha.

Katika **mst. 12-13** Paulo anarudi kwenye swala kuu ambalo lilimsukuma kuandika waraka huu: wale Wayahudishaji na mafundisho yao ya kwamba kuwa Mkristo ilimaanisha kumuamini na kumtegemea Yesu peke yake ilikuwa haitoshi, bali mtu anahitaji kumwamini Yesu + kutahiriwa, kutii ile Sheria ya Musa, n.k. Paulo anadokeza kwamba wale Wayahudishaji ni wanafiki: wao wenyewe kamwe hawakuitimiza ile Sheria. Wao walikuwa kama Mafarisayo ambao kwao Yesu alisema katika **Math 23:4**, *“Wao hufunga mizigo mizito na kuwatwika watu mabegani mwao; wasitake wenyewe kuigusa kwa kidole chao”* (ona pia **Luka 11:46**). Zaidi ya hayo, walikuwa wakihubiri hitaji la kutahiriwa ili kwamba *“makusudi wasiuziwe kwa ajili ya msalaba wa Kristo.”* Kwa asili, msingi wa theolojia yao ulikuwa ni *wakidunia*: wao waliweka msingi katika kujali usalama wao wa kimwili na maslahi yao. Kama ilivyo, msingi wa theolojia yao ulikuwa moja kwa moja kinyume na kile ambacho Kristo alisema alipowaambia wanafunzi wake, *“Msiwaogope wauuao mwili, wasiweze kuiua na roho; afadhali mwogopeni yule awezaye kuuangamiza mwili na roho pia katika jehanum”* (**Math 10:28; Luka 12:4**), and *“Likumbukeni lile neno nililowaambia , ‘Mtumwa si mkubwa kuliko Bwana wake.’Ikiwa waliniudhi mimi,*

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

watawaudhi ninyi" (**Yohana 15:20**).

Mistari hii miwili inaibua swala jingine muhimu ambalo Paulo pia alilijadili hapo awali katika ule waraka. Mahususi, mistari hii kwa mara nyingine inaonyesha kwamba Ukristo haufanani na dini nyinginezo zote hapa duniani. Kwa asili yake, Ukristo sio dini ya utaratibu fulani maalum wa kutekeleza mambo fulani kwa nje, bali ni kitu fulani cha ndani na cha kiroho. Utaratibu fulani wa kutekeleza mambo fulani kwa nje ni zile ishara zinazoonekana za nje za neema ya kiroho ya ndani ambayo Bwana anatupatia. Ukiristo ni wa kiungu (kile ambacho Mungu amekifanya kwa ajili yetu), sio wa kibinadamu (kile tunachokifanya kwa ajili ya Mungu). Watetezi wote wa dini zote ambazo zimeanzishwa na wanadamu wanafokasi katika matendo ya wanadamu, sio katika msalaba wa Kristo. Paulo anatoa kauli katika **1 Kor 1:23**, *"Bali sisi tunamhubiri Kristo, aliyesulibiwa; kwa Wayahudi ni kikwazo kwa Wayunani ni upuuzi."* Wale Wayahudishaji walikuwa wakijitahidi kuukwepa ule msalaba wa Kristo. Hata hivyo, ikiwa hakuna msalaba, hakuna injili. Kila wakati tunapouangalia msalaba, tunapaswa kufikiri, "Mimi niko hapa, na nimeokoka tu, kwa sababu *yako*." Ndio maana Paulo alisema kwamba hakuweza kamwe kujisifu kwa kitu chochote *"ila msalaba wa Bwana wetu Yesu Kristo"* (**mst. 14**).

Kuna maana ya kimatendo ya hiki ambacho Paulo anakigusia juujuu anaposema kwamba kwa njia ya msalaba *"ulimwengu umesulibishwa kwangu na mimi kwa ulimwengu"* (**mst. 14**). Kwa kusema hivyo, Paulo anakataa "vipimo vya dunia, viwango vya dunia na utambulisho wake wa kiakili wa vile namna dunia inafikiri kuhusiana na maswala ya dhambi na neema—kwa maneno mengine, anapinga zile 'kanuni za msingi za dunia' ambazo zilikuwa zikitetewa na wale Wayahudishaji ambazo kwazo inaeleweka kwamba watu wanakwenda mbinguni kwa 'kuwa wema,' na wanajiepusha na jehanamu kwa kutofanya chochote kibaya." (Riddlebarger 1998g: 6) Paulo anaelewa utii kamili kwa Yesu ulimaanisha nini. Anaujua ukweli wa kile ambacho Yesu alisema, *"Kama mngekuwa wa ulimwengu, ulimwengu ungewapenda walio wake; lakini kwa kuwa ninyi si wa ulimwengu, bali mimi naliwachagua katika ulimwengu, kwa sababu hiyo ulimwengu huwachukia"* (**Yohana 15:19**). Yakobo alielezea ufahamu huo huo katika **Yak 4:4**, *"Hamjui ya kwamba kuwa rafiki wa dunia ni kuwa adui wa Mungu? Basi kila atakaye kuwa rafiki wa dunia hujifanya kuwa adui wa Mungu."*

Paulo aliuthibitisha uhalisia wa dunia kusulibia kwake na yeye kwa dunia kwa lile badiliko kubwa la maisha lililotukea alipomjia Kristo. Kabla hajamjia Kristo, alikuwa tajiri na mwenye nguvu, mtesaji wa Wakristo (**Matendo 7:58-8:1; 9:1-2; 22:3-5, 20; Filp 3:4-6; 1 Tim 1:13**). Hata hivyo kutoka wakati ule alipookoka, Mungu alimwonyesha *"yalivyo mengi yatakayompasa kuteseka kwa ajili ya jina langu"* (**Matendo 9:16**). Na kuteseka aliteseka. Alitoka katika ile hali ya kuwatesa Wakristo na kuwa mteswaji (na mwishowe kukatwa kichwa) kwa sababu alikuwa Mkristo (ona **2 Kor 11: 23-33**). Hivyo, katika **mst. 17** anasema, *"Nimechukuwa mwilini mwangu chapa zake Yesu."* Hizi "*chapa zake Yesu"* ni hasa nishani za heshima.

Mstari 15 unarudia kile kifungu kidogo kuhusu yale ambayo Paulo aliyasema katika **Gal 5:6** ya kuwa asili ya Ukristo sio utaratibu fulani maalum wa kutekeleza mambo fulani kwa nje. Hata hivyo, katika **mst. 15** anabadilisha maelezo ya asili ya Ukristo kutoka *"imani itendayo kazi kwa upendo"* kuwa *"kiumbe kipya"* (ona pia **2 Kor 5:17**). *"Imani itendayo kazi kwa upendo"* na *"kiumbe kipya"* ni kama pande mbili za sarafu moja: *"imani itendayo kazi kwa upendo"* huudhihirisha uhalisia mpya wa sisi ni nani na nini kwa dunia; *"kiumbe kipya"* huelezea ule uhalisia mpya wa sisi ni nini na nani katika Kristo. Tunaitwa *"kiumbe kipya"* kwa sababu tunaunganishwa na Kristo kwa njia ya kuzaliwa upya (**Yohana 3:3, 5, 7**). Hilo hubadilisha Wakristo. Mtu anapomjia Kristo, anapokea moyo mpya (**Ezek 36:26; 2 Kor 3:3**), nia ya Kristo (**1 Kor 2:16**), na Roho kutoka kwa Kristo (**Ezek 36:26; Yohana 14:17**). Hivi humpa Mkristo uhusiano wa karibu, wa kibinafsi na Mungu kwa njia ya Kristo (**Ebr 4:16**; ona pia **Ebr 7:19**) na sababu na njia mpya ya kuishi. Kwa sababu Kristo yuko ndani yetu na tuna moyo mpya, nia mpya, na Roho mpya, anavyovithamanisha, na kuvipa kipaumbele vinakuwa tunavyovithamanisha na kuvipa kipaumbele. Anatenda kazi ndani yetu na kupitia sisi ili atufanya kuwa kama yeye mwenyewe (**Rum 8:29; Filp 2:12-13**). Kuokoka na kuunganishwa na Kristo huumba mtu mpya (**Yohana 3:3; Rum 6:4; 2 Kor 5:17; Gal 6:15**); waaminio wameasiliwa katika familia ya Mungu kama watoto wake (**Yohana 1:12; Rum 8:14-17, 23; 9:4; Gal 3:26; 4:5-7; Efe 1:5; 2:19; 1 Yohana 3:1**) na wanakuwa na uhusiano wa ndani sana kati ya wao kwa wao kama kaka na dada (mfano, **Math 12:50; Matendo 1:16; 6:3; 11:29; 12:17; 16:40; 18:18; 21:7, 17; Rum 14:10; 1 Tim 5:1-2**). Siku moja, Kristo atarudi na kuifanya upya dunia yote na uumbaji wote; Wakristo watapokea miili mipya ya utukufu na watairithi mbingu mpya na nchi mpya (**Rum 8:18-23; 1 Kor 15:35-57; 2 Pet 3:3-13; Ufu 21:1-11**). Ndani ya Kristo sisi kwa hakika tu, *"viumbe wapya."* Hakuna dini nyingine duniani inayoweza kufanya hivyo.

Katika **mst. 16** Paulo anasema, *"Na wote watakaoenenda kwa kanuni hiyo, amani na iwe kwao, na rehema, naam, kwa Israeli wa Mungu."* "Kanuni" ambayo anaizungumzia ni imani na kumtegemea Kristo peke yake na kwa kupitia hiyo tuna *"enenda kwa Roho."* Yesu anaahidi, *"Amani nawaachieni; amani yangu nawapa; niwapavyo mimi sivyo kama ulimwengu utoavyo"* (**Yohana 14:27**). Vivyo hivyo Paulo anaomba kwamba *"Amani na iwe kwao na rehema."* Tutambue kuwa kanisa litaiona Amani na rehema tukienenda kwa

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

kanuni; Amani na rehema haviwezekani tukiachana na hiyo.

Paulo tena akaendelea kusema *"na kwa Israeli wa Mungu."* Kifungu hiki cha maneno *"Israeli wa Mungu"* ni tafsiri zaidi ya "*kiumbe kipya"* (**mst. 15**) na *"na wote watakaoenenda kwa kanuni hiyo"* (**mst. 16**). Kwa maneno mengine, Paulo anazungumza kuhusu kanisa—waaminio wa Kiyahudi na Kiyunani wakiwa wameungana katika imani. Shauku yake yote katika waraka mzima ilikuwa ni kuhusu umoja wa kanisa (ona **Gal 3:28**) ambalo ndilo mbegu ya kweli ya Ibrahimu (**Gal 3:29**). Kwa hiyo, hakuna msingi kupendekeza kwamba Paulo anabadilisha fokasi yake na kuwatenga kwenye kundi la peke yake ama taifa la Israeli au Wakristo wa Kiyahudi peke yake (ona Beale 1999b: 204-33; Köstenberger 2001: 3-24; Longenecker 1990: 298-99; Robertson 2000: 38-46).[26] Bernard Ramm anafupisha, "Ikiwa usemi huu ulimaanisha wale Wayahudi, au hata Wakristo wa Kiyahudi basi moja kwa moja angekuwa amejichanganya yeye mwenyewe. Watu wa kweli wa Mungu sio wale Wayahudishaji ambao matakwa yao yalikuwa kuwatahiri waongofu wao, bali wale ambao huona utukufu juu ya msalaba na ni viumbe wapya ndani ya Kristo. Zaidi ya hayo, ile amani na rehema inayoombwa kwa Mungu katika kifungu hiki *kwa misingi ya amri hii* inaombwa kwa Mungu juu ya wale ambao huenenda kwa hiyo (na kama madai ya ujenzi ya Kiyunani) juu ya Israeli wa Mungu. Haiepukiki kwamba wale *Israeli wa Mungu* maana yake ni wale watu wa kweli wa Mungu (kinyume na wale Wayahudishaji) ambao huona fahari katika msalaba na kuhesabu kuzaliwa upya kama tendo la kuokoa la Mungu na sio kutahiriwa." (Ramm 1970: 263-64)[27]

Paulo anahitimisha waraka huu katika **mst. 18** kwa kuwaita wasomaji wake "ndugu zangu" na kuwaombea "neema" ya Bwana Yesu Kristo kuwa juu yao. Hili linakubalika, kwa kuwa amekuwa akijadiliana nao kwamba ni ile injili ya kweli peke yake inayotuunganisha kama kaka na dada bila ya kujali mazingira tuliyotokea, badala ya kutugawa. Alianza waraka huu kwa "neema" (**Gal 1:3**), na waraka wote umekuwa shangwe ya umuhimu, ulazima, na ukuu wa neema. Hivyo, kumalizia kwake kutukumbushe kwamba kuanzia mwanzo hadi mwisho, msingi wa maisha yetu na kile ambacho yanaakisi ni *"neema ya Bwana wetu Yesu Kristo."*

MASWALI YA KUJADILI

1. Ni utaratibu gani maalum wa kutekeleza mambo fulani kwa nje kidini ambao makanisa yetu wanao? Ni nini wajibu wa kimsingi wa taratibu hizo?

2. "Ulimwengu umesulibishwa kwangu, na mimi kwa ulimwengu" maana yake ni nini? Je, unafikiria kwamba hili ni jambo ambalo ni halisi kimatendo katika maisha ya wengi wanaodai kuwa ni Wakristo? Kama sivyo, nini kifanyike ili jambo hili liwe halisi?

3. Kuwa "kimbe kipya" humaanisha nini"?

4. Paulo aliwaombea wawe na "Amani na rehema" wale "wanaoenenda kwa kanuni" (m.y., wana imani na wanamtegemea Kristo peke yake kupitia yeye *"tunaenenda kwa Roho"*). Je, unafikiri kwamba Wakristo wengi hujikia kuwa na amani mara kwa mara, mara kwa mara ni wapatanishi, na mara kwa mara huonyesha rehema? Kama si hivyo, ni kwa nini, nini kifanyike ili wawe watu wa amani na rehema?

BIBLIOGRAFIA

Anselm of Canterbury. 1903. *Cur Deus Homo.* Translated by Sidney Norton Deane. Chicago: Open Court. Online: http://www.ccel.org/ccel/anselm/basic_works.i.html.

Bauckham, Richard. 1978. "The Sonship of the Historical Jesus in Christology." *Scottish Journal of Theology* 31: 245-60.

Beale, G. K. 1999a. *The Book of Revelation* (NIGTC). Grand Rapids, MI: Eerdmans.

_____. 1999b. "Peace and Mercy Upon the Israel of God: The Old Testament Background of Galatians 6, 16b." *Biblica* 80: 204-33. Online: https://www.bsw.org/biblica/vol-80-1999/peace-and-mercy-upon-the-israel-of-god-the-old-testament-background-of-galatians-6-16b/320/.

[26] Hata kisarufi, Kiyunani neno *kai*, ambalo kwa kawaida hutafsriwa "na" (kama iko hapa) linaweza kuwa na ile maana ya "hata," au "ambayo ni," au "ikimaanisha" ikiwa muktadha unaruhusu, kama ilivyo hapa; ona, kwa mfano, **Yohana 1:16; 1 Kor 3:5; 8:12; 15:38** (Swavely 2015: n.p.; LaRondelle 1983: 108).

[27] Menn 2009-2018: 49-59 anajadili kwa kirefu namna ambavyo kanisa ni Israeli mpya wa kweli wa kiroho.

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

Belleville, Linda. 1986. "'Under Law': Structural Analysis and the Pauline Conception of Law in Galatians 3:21–4:11." *Journal for the Study of the New Testament* 26: 53-78.

Bonhoeffer, Dietrich. 1997. *Letters and Papers from Prison,* enlarged edition. Edited by Eberhard Bethge. New York: Touchstone.

Bordow, Todd. 2018. "Not Under the Law – Galatians 3." Online: http://kingdomkompilations.com/sermons/not-under-the-law-galatians-3/.

Burdick, Donald. 1981. "James." In *The Expositor's Bible Commentary,* ed. Frank Gaebelein, 159-205. Grand Rapids: Zondervan.

Carson, D. A., and Douglas Moo. 2005. *An Introduction to the New Testament.* Grand Rapids: Zondervan.

Crabtree, Jack. 2001. "The Tao of Faith: A Reconsideration of Taoist Evangelicalism." Online: https://gutenberg.edu/2001/02/the-tao-of-faith/.

Danker, Frederick, ed. 2000. *A Greek-English Lexicon of the New Testament and Other Early Christian Literature*. Chicago: The University of Chicago Press.

Demarest, Bruce. 1997. *The Cross and Salvation.* Wheaton, IL: Crossway. Preview online: https://books.google.com/books?isbn=1433519577.

Garlington, Don. 1997. "Role Reversal and Paul's Use of Scripture in Galatians 3.10-13." *Journal for the Study of the New Testament* 65: 85-121.

Goldsworthy, Graeme. 2000. *Preaching the Whole Bible as Christian Scripture.* Grand Rapids, MI: Eerdmans. Preview online: https://books.google.com/books?isbn=0802847307.

Irons, Lee. 2002. "Married to Another." Online: https://www.csmedia1.com/cpcnewhaven.org/married-to-another.pdf.

Keller, Timothy. 2008. *The Reason for God: Belief in an Age of Skepticism.* New York: Dutton. Preview online: https://books.google.com/books?isbn=0525950494.

_____. Not dated. "The Gospel—Key to Change." Online: https://www.cru.org/content/dam/cru/legacy/2013/01/Gospel_KeytoChange_TimKeller.pdf.

Kistemaker, Simon. 2000. "The Temple in the Apocalypse." *Journal of the Evangelical Theological Society* 43: 433-41. Online: http://www.etsjets.org/files/JETS-PDFs/43/43-3/43-3-pp433-441_JETS.pdf.

Köstenberger, Andreas. 2001. "The Identity of the Israel of God in Galatians 6:16." *Faith & Mission* 19: 3-24. Online: http://www.mountain-retreat.org/archives/galatians_6.pdf.

Ladd, George Eldon. 1959. *The Gospel of the Kingdom.* Grand Rapids: Eerdmans.

LaRondelle, Hans. 1983. *The Israel of God in Prophecy: Principles of Prophetic Interpretation.* Berrien Springs, MI: Andrews University Press.

Lewis, Dhati. 2015. "The Church Is Not Like A Family." Online: http://www.vergenetwork.org/2017/03/14/the-church-is-not-like-family/?inf_contact_key=563a07f48051945f93bdc050b4bbef102519cd85d688856b793a9898205d2ff9.

Longenecker, Richard. 1990. *Galatians* (WBC 41). Nashville: Thomas Nelson.

Lusk, Rich. 2003. The Galatian Heresy: Why We Need To Get It Right," *Theologia.* Online: http://hornes.org/theologia/rich-lusk/getting-the-galatian-heresy-right.

Luther, Martin. 1535. *A Commentary on St. Paul's Epistle to the Galatians.* Translated and abridged by Theodore Graebner. Online: http://www.ccel.org/ccel/luther/galatians.i.html.

Luther, Martin. 1979. *Commentary on Galatians.* Grand Rapids: Kregel.

Marshall, I. Howard, Stephen Travis, and Ian Paul. 2002. *Exploring the New Testament: A Guide to the Letters and*

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

Revelation. Downers Grove, IL: InterVarsity.

McClelland, Scott. 1989. "Galatians." In *Evangelical Commentary on the Bible,* ed. Walter Elwell, 998-1019. Grand Rapids: Baker.

Menn, Jonathan. 2007-2017. *Forgiveness and Reconciliation.* Online: http://www.eclea.net/courses.html#forgive.

_____. 2009-2018. *Biblical Theology*. Online: http://www.eclea.net/courses.html#theology.

_____. 2010-2017. *Biblical Eschatology.* Online: http://www.eclea.net/courses.html#eschatology.

_____. 2015-2020. *Christianity and Islam: The Essentials.* Online: http://www.eclea.net/courses.html#islam.

_____. 2017. *The Church: Its Nature, Mission, and Purpose.* Online: http://www.eclea.net/courses.html#church.

_____. Not dated. Gen 15:1-18-"The Greatest Prophecy in the Bible." Online: http://www.eclea.net/sermons.html#ot.

Mikolaski, Samuel. 1970. "Galatians." In *The New Bible Commentary: Revised,* 3rd ed., ed. D. Guthrie and J. A. Motyer, 1089-11104. Carmel, NY: Guideposts.

Moo, Douglas. 1984. "Jesus and the Authority of the Mosaic Law." *Journal for the Study of the New Testament* 20: 3-49. Online: www.djmoo.com/articles/jesusandauthority.pdf.

_____. 1985. *James* (TNTC). Grand Rapids: Eerdmans.

_____. 1989. "James." In *Evangelical Commentary on the Bible,* ed. Walter Elwell, 1150-62. Grand Rapids: Baker.

_____. 1993. "The Law of Christ is the Fulfillment of the Law of Moses: A Modified Lutheran View" In *The Law, the Gospel, and the Modern Christian: Five Views,* 319-76. Grand Rapids: Zondervan. Online: http://static.squarespace.com/static/537a4700e4b0cc86709d564c/t/538e0c5ce4b038079b6ca505/1401818204280/fulfillmentoflaw.pdf.

Ngewa, Samuel. 2006. "Galatians." In Africa Bible Commentary, ed. Tokunboh Adeyemo, 1413-24 (Nairobi: Word Alive).

Ngundu, Onesimus. 2006. "Revelation." In *Africa Bible Commentary,* ed. Tokunboh Adeyemo, 1543-79. Nairobi: WordAlive. Preview online: https://books.google.com/books?isbn=031087128X.

Ouedraogo, Adama. 2006. "Prophets and Apostles." In *Africa Bible Commentary,* ed. Tokunboh Adeyemo, 1434. Nairobi, Kenya: WordAlive. Preview online: https://books.google.com/books?isbn=031087128X.

Owen, John. 1979. *Indwelling Sin in Believers.* Grand Rapids: Baker.

Piper, John. 1981. "Let us Walk By the Spirit"—Gal 5:25. Online: https://www.desiringgod.org/messages/let-us-walk-by-the-spirit.

_____. 1983a. "Christ Redeemed Us From the Curse of the Law"—Gal 3:10-14. Online: https://www.desiringgod.org/messages/christ-redeemed-us-from-the-curse-of-the-law.

_____. 1983b. "For Freedom Christ Has Set Us Free"—Gal 5:1-5. Online: https://www.desiringgod.org/messages/for-freedom-christ-has-set-us-free.

_____. 1983c. "Freed to Love"—Gal 5:13-15. Online: https://www.desiringgod.org/messages/freed-to-love.

_____. 1983d. "The War Within: Flesh Versus Spirit"—Gal 5:16-18. Online: https://www.desiringgod.org/messages/the-war-within-flesh-versus-spirit.

_____. 1983e. "The Law of Christ: Bearing Each Other's Burdens"—Gal 6:1-5. Online: https://www.desiringgod.org/messages/the-law-of-christ.

_____. 1983f. "Do Not Grow Weary in Well-Doing"—Gal 6:6-10. Online: https://www.desiringgod.org/messages/do-not-grow-weary-in-well-doing.

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

_____. 2009. *Finally Alive.* Geanies House, Fearn, Ross-shire, Scotland: Christian Focus.

Platt, David, and Tony Merida. 2014. *Exalting Christ in Galatians* (C-CEC). Nashville: Holman Reference).

Powlison, David. 1995. "Idols of the heart and 'Vanity Fair.'" *Journal of Biblical Counseling* 13: 35-50. Online: http://docplayer.net/63071701-Idols-of-the-heart-and-vanity-fair.html.

Ramm, Bernard. 1970. *Protestant Biblical Interpretation: A Textbook of Hermeneutics,* 3rd ed. Grand rapids: Baker. Online: http://www.glasovipisma.pbf.rs/phocadownload/knjige/bernard%20ramm%20protestant%20biblical%20interpretation.pdf.

Riddlebarger, Kim. 1998a. "Baptized into Christ"—Gal 3:26–4:7. Online: http://kimriddlebarger.squarespace.com/an-exposition-of-galatians/.

_____. 1998b. "The Law Does Not Nullify the Promise"—Gal 3:15-25. Online: http://kimriddlebarger.squarespace.com/an-exposition-of-galatians/.

_____. 1998c. "What Has Happened to All Your Joy?—Gal 4:8-20. Online: http://kimriddlebarger.squarespace.com/an-exposition-of-galatians/.

_____. 1998d. "It Is for Freedom"—Gal 5:1-6. Online: http://kimriddlebarger.squarespace.com/an-exposition-of-galatians/.

_____. 1998e. "Live By the Spirit"—Gal 5:16-26. Online: http://kimriddlebarger.squarespace.com/an-exposition-of-galatians/.

_____. 1998f. "A Man Reaps What He Sows"—Gal 6:1-10. Online: http://kimriddlebarger.squarespace.com/an-exposition-of-galatians/.

_____. 1998g. "May I Never Boast"—Gal 6:11-18. Online: http://kimriddlebarger.squarespace.com/an-exposition-of-galatians/.

_____. 2003. "Does the Promise Come by Faith or Works?" Online: http://www.mountain-retreat.org/sermons/does-the-promise-come-by-faith-or-works.html.

_____. 2017. "No Other Gospel, Galatians 1:1-9." *RPM* 20: n.p. Online: https://thirdmill.org/articles/kim_riddlebarger/kim_riddlebarger.Gal.01.html.

Robertson, O. Palmer. 2000. *The Israel of God: Yesterday, Today, and Tomorrow.* Phillipsburg, NJ: P&R.

Silva, Moisés. 2007. "Galatians." In *Commentary on the New Testament Use of the Old Testament,* ed. Beale, G. K., and D. A. Carson, 785-812. Grand Rapids, MI: Baker Academic. Preview online: https://books.google.com/books?isbn=1441210520.

Sproul, R. C. 2002. *Saved from What?* Wheaton, IL: Crossway. Preview online: https://books.google.com/books?isbn=1433515911.

_____. 2019. "What Does 'Simul Justus et Peccator' Mean?" Online: https://www.ligonier.org/blog/simul-justus-et-peccator/.

Stott, John. 1986. *The Cross of Christ.* Downers Grove: InterVarsity. Online: https://korycapps.files.wordpress.com/2012/11/j-stott-cross-of-christ.pdf.

Swavely, Dave. 2015. "'The Israel of God' in Galatians 6:16. Online: http://www.thewaywithwords.net/2015/04/the-israel-of-god-in-galatians-616.html.

Westminster Confession of Faith. 1647. Online: https://www.ligonier.org/learn/articles/westminster-confession-faith/.

White, R. Fowler. 2000. "Agony, Irony, and Victory in Inaugurated Eschatology: Reflections on the Current Amillennial-Postmillennial Debate." *Westminster Theological Journal* 62: 161-76.

Williamson, Paul. 2007. *Sealed with an Oath: Covenant in God's Unfolding Purpose* (NSBT 23). Nottingham, England:

Copyright © by Jonathan Menn 2020. All rights reserved.

Apollos. Preview online: https://books.google.com/books?isbn=0830826246.

Witherington, Ben. 1998. *Grace in Galatia.* Grand Rapids: Eerdmans.

Wright. N. T. 1996. *Jesus and the Victory of God.* Minneapolis, MN: Fortress. Preview online: https://books.google.com/books?isbn=1451414978.

_____. 2000. "The Letter to the Galatians: Exegesis and Theology." In *Between Two Horizons: Spanning New Testament Studies and Systematic Theology,* ed. Joel Green and Max Turner, 205-36. Grand Rapids: Eerdmans. Online: https://ntwrightpage.com/2016/07/12/the-letter-to-the-galatians-exegesis-and-theology/.

Zodhiates, Spiros. 1993. *The Complete Word Study Dictionary: New Testament,* Ufu. ed. Chattanooga, TN: AMG.

MWANDISHI

Jonathan Menn anaishi Appleton, WI, USA. Alipokea shahada ya kwanza elimu ya siasa (B.A. in political science) kutoka Chuo kikuu cha Wisconsin-Madison, ambapo alitunukiwa shahada ya heshima kutokana na kufaulu kwa viwango vya juu, mnamo mwaka wa 1974, akajumuika na Phi Beta Kappa ambayo ni taasisi ya heshima katika kijamii. Baadae akapata J.D. ambayo ni shahada ya juu ya sheria kutoka Shule ya sheria, Cornell magna cum laude, mnamo mwaka wa 1977, na akajumuishwa kwenye "Order of the Coif legal honor society" ambayo ni taasisi inayoheshimika katika jamii inayofanya kazi za kisheria. Akaitumia miaka 28 iliyofuata akifanya kazi za uanasheria, kama wakili, wa huko Chicago na baadaye kama mmiliki mwenza wa Shirika la mawakili liitwalo Menn Law Firm kule Appleton, WI. Akawa muamini na mfuasi wa Yesu Kristo tangu mwaka wa 1982. Alifundisha masomo ya Biblia darasa la watu wazima kwa miaka kadhaa. Kukua kwa pendo lake katika Thiolojia na Huduma vilimfanya aende akatafute Shahada ya Uzamili ya mambo ya Mungu (Master of Divinity) katika chuo cha Trinity Evangelical Divinity School huko Deerfield, IL. Alipokea shahada yake ya M.Div. kutoka kwa TEDS, summa cum laude, mnamo Mei 2007. Kati ya mwaka 2007 – 2013 alikuwa mkurugenzi wa Afrika Masahariki wa huduma ya Equipping Pastors International (EPI). Na sasa Jonathan ni mkurugenzi wa huduma ya kuwawezesha viongozi wa kanisa Afrika Mashariki Equipping Church Leaders East Africa. (ECLEA). Kwa ujumla, kazi zake za mafundisho aliyoandika ya masomo ya Bibilia, yanapatikana kwenye: **www.eclea.net**. Unaweza kuwasiliana na Jonathan kupitia na anuani hii: **jonathanmenn@yahoo.com**.